# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Thelathini – Tarehe 15 Mei, 2020**

*(Bunge Lilianza Saa Nane Kamili Mchana)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Tisa, Kikao cha Thelathini.

Katibu!

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**MASWALI NA MAJIBU**

*(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)*

Na. 277

**Ujenzi wa Daraja la Mto Ruvuma**

**MHE. MARTIN M. MSUHA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani juu ya ujenzi wa daraja la mto Ruvuma linalounganisha Vijiji vya Lusonga na Lihale?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martin Mtonda Msuha, Mbunge wa Mbinga Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)* umepanga kufanya usanifu wa kina daraja la Mto Ruvuma ikiwa ni hatua muhimu za kuanza ujenzi wa daraja hilo. Usanifu huo utawezesha kutambua mahitaji halisi ya gharama za ujenzi wa daraja ili kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Na. 278

**Mizigo na Vyakula Kunuswa na Mbwa Bandarini**

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB** aliuliza:-

Serikali haina dini lakini imekuwa ikiheshimu sana madhehebu ya dini, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa hili. Hivi karibuni katika Bandari ya Dar es Salaam wananchi waliokuwa wakisafiri kutoka Dar es Salaam kwenda Zanzibar

walikutana na kadhia kubwa sana ya mizigo, watoto wao na vyakula vya watoto kunuswa na mbwa:-

(a) Je, ni sababu gani iliyosababisha mizigo, watoto wadogo na vyakula vyao kunuswa na mbwa?

(b) Je, Bandari ya Dar es Salaam haina *x-ray* mashine na ulinzi wa kutosha?

(c) Je, ni lini tabia hiyo itakoma?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub Mb, (BLW) lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, zoezi la ukaguzi wa mizigo kwa kutumia mbwa wa kunusa linafanyika katika bandari ya Dar es Salaam katika maeneo mbalimbali ikiwemo eneo la huduma ya abiria. Zoezi hili linafanyika sambamba na ukaguzi wa mashine *x-ray baggage scanner* na ukaguzi mwingine wa kawaida *(physical inspection).* Ukaguzi wa mizigo kwa kutumia mbwa wa kunusa hulenga kubaini nyara za serikali na madawa ya kulevya na hufanyika kwa mizigo ambayo haiwezi kukaguliwa katika midaki ya kukagua mizigo *(x-ray baggage scanner).* Mizigo inayokaguliwa kwa mbwa haihusishi watu na vyakula, ambao hukaguliwa katika midaki.

(b) Mheshimiwa Spika, Bandari ya Dar es Salaam inazo mashine za ukaguzi wa mizigo za *x-ray* na pia ulinzi ni wa kutosha.

(c) Mheshimiwa Spika, Ukaguzi wa mizigo hususan mizigo ambayo haiwezi kukaguliwa katika midaki ya mizigo magetini yenye viashiria vya kuwa na nyara na madawa ya kulevya utaendelea kufanyika kwa lengo la kubaini, kuzuia na kudhibiti uhalifu bandarini.

Na. 279

## Wananchi Waliopisha Ujenzi wa Barabara ya Bulamba – Kisorya

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI** aliuliza:-

Wananchi wa Kijiji cha Nambaza walizuiwa kuendeleza maeneo yao ili kupisha upanuzi wa barabara ya Bulamba – Kisorya yenye urefu wa km 50 lakini tangu mwaka 2014 hadi leo wananchi hao hawajalipwa fidia.

(a) Je, ni lini Serikali itawalipa wananchi hao?

(b) Kuna maeneo mengine kama Busambara, Bumerwa wananchi wameshalipwa fidia zao, wakati wananchi zaidi ya 80 wa Nambaza hapohapo hawajalipwa na shauri lao limeshafikia hadi Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na hatima yao haijulikani. Je, Serikali inatoa kauli gani?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi, Mbunge Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Bulamba – Kisorya (km 50) ni sehemu ya barabara ya Nyamuswa – Bunda – Bulamba – Kisorya – Nansio (km 121.9) ambayo ujenzi kwa sehemu ya Bulamba – Kisorya (km 50) unaendelea. Uthamini wa mali kwa sehemu ya Bulamba – Kisorya ulifanyika mwaka 2015 kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007 na Kanuni zake za mwaka 2009 na kwa kuzingati Sheria ya Ardhi Na. 4 Kifungu Na. 179 ya mwaka 1999 na Kanuni za Ukadiriaji Fidia GN.78 (2001).

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Barabara ya Mwaka 2007 imeongea upana wa eneo la hifadhi ya barabara kutoka mita 45 hadi mita 60, yaani mita 22.5 hadi mita 30

kutoka katikati ya barabara kila upande. Hivyo, eneo la hifadhi ya barabara liliongezwa kutoka mita 22.5 hadi 30 kila upande kwenye barabara yote likiwepo eneo la Nambaza bado haijafidiwa. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kutwaa eneo hilo la nyongeza la jumla ya mita 15. Aidha, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mali pamoja na ardhi vilivyomo ndani ya eneo lililoongezeka baada ya Sheria ya Barabara ya Mwaka 2007 havijaathiriwa na ujenzi unaoendelea.

Mheshimiwa Spika, napenda kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* ilitenga fedha kwa ajili ya kufidia waathirika wa ujenzi wa barabara hii katika makundi mawili. Makundi hayo ni waathirika wa maeneo ya barabara ya Mchepuo *(By pass)* na waathirika wa maeneo ambayo barabara imehamia kutoka barabara ya zamani *(re-alignment)* inayohusisha maeneo ya Busambara na Bumera. Wananchi wote walioguswa na barabara hiyo walilipwa fidia zao.

Na. 280

**Tatizo la Maji Mkoa wa Geita**

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza tatizo la majisafi na salama katika Mkoa wa Geita?

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika; kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagula, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika; katika kuhakikisha tatizo la maji Mkoa wa Geita linamalizika, Serikali inatekeleza miradi ya maji katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo yenye gharama ya shilingi 56,000,258,658.00. Utekelezaji wa miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali na inatarajiwa kunufaisha wakazi wapatao

264,352 hivyo kuongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji kufikia asilimia 67 ifikapo mwezi Juni 2020 kutoka asilimia 56 ya sasa.

Mheshimiwa Spika; vilevile, Serikali itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali katika Mkoa wa Geita na maeneo mengine nchini kwa lengo la kuhakikisha huduma ya maji inawafikia wananchi wote.

Na. 281

**Hitaji la Mabwawa ya Maji – Mbulu Vijijini**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza:-

Serikali iliahidi kuchimba Mabwawa ya Mifugo na Umwagiliaji katika kata na Vijiji vya Dirim, Esketch, Mungu wa Mono, Maretadu chini na Yayeda chini:-

Je, ni lini Serikali itachimba mabwawa hayo?

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea kufanya utafiti na utambuzi katika maeneo mbalimbali nchini ili kubaini maeneo yote yanayofaa kujengwa mabwawa kwa ajili ya kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua yatakayotumika kwa kilimo cha umwagiliaji. Maeneo hayo ni pamoja na Kata na Vijiji vya Dirim, Esketch, Mungu wa Mono, Maretadu chini na Yayeda chini.

Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali vya ndani na nje kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwa ni pamoja na miradi ya mabwawa ya kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua.

Mheshimiwa Spika, Ili kuhakikisha ujenzi wa mabwawa ya umwagiliaji unatekelezwa Serikali itashirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu pamoja na Vyama vya Wamwagiliaji kuandaa maandiko ya kuomba fedha katika taasisi mbalimbali za fedha pamoja na kuomba mikopo kutoka taasisi za kifedha kama vile Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(TADB)* ili kujenga na kukamilisha ujenzi wa mabwawa ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali itashirikiana na wadau wakiwemo wakulima, Halmashauri za Wilaya, Sekta binafsi, Taasisi za fedha na washirika wa maendeleo ili kupata fedha za kujenga na kukamilisha ujenzi wa mabwawa ya kilimo cha umwagiliaji baada ya kukamilisha utafiti na utambuzi wa mabwawa hayo kwa ajili ya ujenzi.

Na. 282

**Ununuzi wa Korosho kwa Mfumo wa Stakabadhi Ghalani**

**MHE. HAMIDU H. BOBALI** aliuliza:-

Mfumo wa ununuzi wa Korosho kwa kutumia stakabadhi ghalani umekuwa na changamoto ya kuwanyima wakulima taarifa sahihi ya bei kutokana na kukosekana kwa mwakilishi wa wakulima katika maeneo ambayo minada hiyo inaendeshwa:-

Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuweka utaratibu madhubuti utakaoziba mianya yote inayosababisha wakulima kuporwa fedha zao kwa kutoshiriki kwenye mnada?

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali, Mbunge wa Jimbo la Mchinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tangu kuanza kwa mfumo wa stakabadhi ghalani katika msimu wa mwaka 2007/2008,

Korosho ghafi zimekuwa zikiuzwa kwa njia ya minada na Serikali kupitia Bodi ya Korosho imekuwa ikiratibu uendeshwaji wa minada hiyo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Aidha kabla ya kuanza kwa msimu Bodi ya Korosho hutoa mwongozo wa uendeshwaji wa msimu husika ikiwemo ratiba ya minada kwa kila Chama Kikuu cha Ushirika.

Mheshimiwa Spika, ratiba za minada huandaliwa kwa makubaliano na vyama vikuu ambapo kila chama kikuu hupendekeza siku na mahali mnada utakapofanyika. Kila mnada unaofanyika kunakuwa na wakulima, pamoja na wadau wengine ikiwa ni pamoja na Mamlaka za Wilaya husika, Mrajisi wa Vyama vya Ushirika, Bodi ya Korosho na minada inaendeshwa na Vyama Vikuu. Aidha, katika minada hiyo, Bodi ya Korosho huwa inatoa mwenendo wa bei katika soko la dunia ambapo wakulima huambiwa mwenendo wa bei kabla ya kuamua kuuza au kutouza korosho zao.

Mheshimiwa Spika, kigezo kikubwa katika upangaji wa ratiba za minada ni kuangalia mahali/sehemu ambapo kuna uwakilishi wa wakulima wa kutosha na panapoweza kufikika kwa urahisi na wanunuzi. Aidha, katika utekelezaji wa taratibu hizo Wakulima wa eneo husika ndio wamekuwa wakifanya maamuzi ya aidha kuuza ama kutokuuza korosho husika kwa niaba ya wakulima wote walio chini ya chama kikuu husika. Kwa mfano msimu wa 2019/2020 wakulima wa Kibiti Mkoani Pwani walikataa kuuza korosho zao kutokana na bei ndogo iliyotolewa kwenye minada hiyo.

Na. 283

## Huduma za Afya kwa Wazee

**MHE. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Mara zote Serikali imekuwa ikitoa wito wa huduma za wazee kwa bure na uhitaji mkubwa wa wazee ni huduma za kibingwa na endelevu na huduma hizi mara nyingi hupatikana maeneo ya mijini huku wazee wengi wakiwa wanaishi vijijini:-

(a) Je, kwa nini Serikali isiwe na mpango mbadala wa kufikisha huduma maalum za wazee kwa mfumo wa *Mobile*?

(b) Je, kuna Chuo cha Madaktari wa Tiba kwa Wazee na kama hakuna Serikali ina mpango gani?

(c) Je, kwa nini Serikali isiwe na mpango maalum wa kuwaondolea maumivu na kusendeka wazee hawa?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati (Viti Maalum) lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo kwa mfano *(Helpage International)* imeanza kutoa huduma tembezi *(Mobile)* katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Halmashauri za Morogoro, Gairo, Kilosa, Malinyi, Mlimba, Mvomero na Ifakara Mji. Pia, huduma hizi zinatolewa Halmashauri ya Magu Mkoani Mwanza, Korogwe Mji na Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe Mkoani Tanga.

Hata hivyo, huduma hii itaendelea kuenezwa katika halmashauri zingine nchini. Huduma hii inajumuisha kuwapima wazee *(Screening)* na tiba kwa magonjwa wanayokutwa nayo. Taarifa za awali zinaonesha kuwa Wazee wengi wanaugua magonjwa yasiyo ya kuambukiza yakiwemo Kisukari, Shinikizo la juu la damu, Saratani na mengine. Mbali ya kuwafikishia wazee huduma hizi karibu na wanapoishi, matokeo ya zoezi hili yataipa Wizara taarifa muhimu zitakazoiwezesha kupanga mipango ya kuboresha huduma kwa Wazee kwa ufasaha zaidi.

(b) Mheshimiwa Spika, hakuna chuo maalum kwa ajili ya madaktari wa Tiba kwa Wazee. Serikali imewekeza dirisha maalum la tiba kwa wazee, Mpango wa Serikali ni kutoa

udhamini kwa madaktari wanaoomba kusomea ubobezi kwenye Tiba ya wazee *(Getriatic Medicine).* Aidha, kwenye baadhi ya Mitaala ya kozi za afya kuna huduma za wazee.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa mwongozo wa kisera wa mwaka 2016 wa tiba shufaa yaani "*Paliative Care*" ambao katika mwongozo huo unabainisha utoaji wa huduma hizo kwa watu wenye usendeka kuanzia ngazi ya jamii mpaka Taifa. Aidha, kwa mwaka Serikali hutenga fedha kwa ajili ya manunuzi ya dawa za maumivu *Morphine powder* kwa wastani wa kilo 50.

Vilevile, Serikali kupitia hospitali za kanda na hospitali maalum nne ambazo ni *Ocean Road, KCMC*, Bugando, Mbeya *Zonal* na Hospitali ya Benjamini Mkapa zimeanzisha *(compounding area)* kwa ajili ya "*Morphine solution*" ili kuziwezesha hospitali zinazozunguka kanda hizo iwe rahisi kupata huduma hii.

Na. 284

**Serikali Kudhibiti Bidhaa za Mitandaoni**

**MHE. ZUBEDA H. SAKURU** aliuliza:-

Hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la wafanyabiashara hasa katika mitandao ya kijamii ambao wanauza vipodozi na dawa mbalimbali za matumizi ya binadamu:-

Je, Serikali inadhibiti kwa kiwango gani matumizi ya bidhaa ili kuzuia madhara kwa watumiaji wake?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Napenda kujibu Swali la Mheshimiwa Zubeda Hassan Sakuru, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *TMDA* na *TBS* zimechukua hatua zifuatazo kudhibiti uingizwaji na utumiaji wa vipodozi na dawa mbalimbali kama ifuatavyo:-

(a) Vipodozi na madawa yote hutakiwa kusajiliwa kabla ya kibali cha kuingiza nchini kutolewa. *TMDA* ilifungua ofisi saba (7) za Kanda katika mikoa ya Arusha (Kanda ya Kaskazini), Dar es Salaam (Kanda ya Mashariki), Dodoma (Kanda ya Kati), Mbeya (Kanda ya Nyanza za Juu Kusini), Mtwara (Kanda ya Kusini), Mwanza (Kanda ya Ziwa) na Tabora (Kanda ya Magharibi), kwa lengo la kuimarisha ukaguzi.

(b) Wakaguzi wa *TMDA* na *TBS* wamewekwa katika vituo vya forodha vya Namanga, Holili, Horohoro, Tunduma, Sirari, Kasumulu, Mutukula, Rusumo, Bandari ya Dar es Salaam, Bandari ya Mwanza, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Kambarage Nyerere na vituo vingine vya forodha vilivyoko katika Mkoa wa Dar es Salaam kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa bidhaa ikiwa ni pamoja na vipodozi na madawa yanavyoingizwa nchini. Aidha, kwenye vituo vingine vya forodha ukaguzi hufanywa na wakaguzi walio chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na halmashauri.

(c) Taasisi Hizi zimekuwa zikitoa elimu kwa umma juu ya matumizi sahihi ya vipodozi na Madawa na madhara ya utumiaji Usiofaa kwa makundi mbalimbali ya wadau na wananchi. Njia zinazotumika katika kuelimisha jamii ni kama ifuatavyo:- Mihadhara, Matangazo mafupi ya Redio, Mafunzo kwa njia ya Mada, Maonesho, Huduma kwa Wateja Aidha, vipeperushi mbalimbali vinavyoonesha orodha ya vipodozi visivyofaa kwa matumizi ya binadamu na madhara kwa watumiaji vimekuwa vikitolewa wakati wa elimu kwa umma na kwa wananchi.

(d) Mheshimiwa Spika, Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sura 219 inatoa adhabu ya kifungo au kulipa faini au adhabu zote mbili kwa pamoja kwa yeyote anayekamatwa akiingiza nchini vipodozi na dawa zisizofaa

kwa matumizi ya binadamu. Sambamba na adhabu hii, vilevile mtuhumiwa anapaswa kugharamia uteketezaji wa vipodozi na dawa zote zilizokamatwa na wakaguzi.

Na. 285

**Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Afrika**

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI** aliuliza:-

Serikali inatekeleza programu ya Urithi wa Ukombozi wa Afrika *(The African Liberation Heritage Programme*) chini ya *UNESCO:-*

Je, ni lini Serikali itaingiza katika utekelezaji huo Kituo cha Masonya kilichokuwa Kambi ya Wapigania Uhuru wa Msumbiji FRELIMO ambacho kina miundombinu na kumbukumbu nyingi za historia ya ukombozi?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhandisi Ramo Matala Makani, Mbunge wa Tunduru Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo inaratibu utekelezaji wa Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Afrika.

Mheshimiwa Spika, Programu hii ni ya Afrika nzima na kwa sasa imeanza kutekelezwa katika Nchi za Kusini mwa Afrika. Aidha, Programu hii ilipitishwa katika Mkutano Mkuu wa *UNESCO* mwaka 2005 na kuidhinishwa katika Mkutano wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi za Umoja wa Afrika mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, kazi iliyofanyika katika utekelezaji wa programu hii ni pamoja na kubainishwa na kutambuliwa kwa nyaraka, vitu, mahandaki, majengo, maeneo na Kambi

zilizotumiwa na Wapigania uhuru kutoka vyama mbalimbali vya Ukombozi. Eneo la Masonya lililopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ni sehemu ya maeneo yaliyotambuliwa na Wizara kwa minajili ya kutunza na kuhifadhi historia ya ukombozi wa Afrika. Eneo hili lilitumika kama Kambi ya Wapigania uhuru wa chama cha *FRELIMO* kutoka Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kazi ya kubainishwa kwa maeneo haya yaliyotumiwa wakati wa harakati za kutafuta uhuru wa Afrika likiwemo eneo la Masonya, Serikali kupitia Wizara yangu inaandaa Muswada wa Sheria kwa lengo la kuyalinda/kuyahifadhi maeneo hayo ili yasiathiriwe na ujenzi mbalimbali unaondelea nchini. Aidha, Wizara inaendelea na ukarabati mkubwa wa majengo yaliyokuwa Makao Makuu ya Kamati ya Ukombozi ya Umoja wa Afrika, jijini Dar es Salaam.

Na. 286

## Miradi ya *REA III* Magu

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha miradi ya *REA III* katika Vijiji vyote vilivyobaki katika Wilaya ya Magu hususan Kijiji cha Mahaha ambapo Waziri wa Nishati alizindua kwa nguzo nane.

**WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bonaventura Desdery Kiswaga, Mbunge wa Magu kama ifuatavyo:-

Serikali kupitia *REA* inatarajia kukamilisha kusambaza umeme kwenye vijiji vilivyobaki vya Wilaya ya Magu kupitia Mradi wa *REA* Awamu ya Tatu mzunguko wa pili unaotarajiwa kuanza Mwezi Julai, 2020. Aidha, vijiji 22 vya Mahaha, Bugabu, Nyanguge, Bundilya, Wambiza, Kitongo, Itandula, Ndagalu, Sese, Itumbili, Mashineni, Kisesa ‘A’, Igekemaja, Kipeja, Ihushi,

Nyalikungu, Matela, Muda na Langi vinatarajiwa kupatiwa umeme kupitia Mradi wa REA Awamu ya Tatu mzunguko wa kwanza unaoendelea.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kupeleka umeme katika vijiji hivyo 22 vya Wilaya ya Magu inahusisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 33 umbali kilomita 12.59, msongo wa kilovoti 0.4 urefu wa kilomita 90, ufungaji wa transfoma 41 za KVA 50 pamoja na kuwaunganishia huduma ya umeme wateja wa awali 1,558. Gharama ya mradi ni shilingi Bilioni 4.13.

Mheshimiwa Spika, kijiji cha Mahaha kilipatiwa umeme kupitia utekelezaji wa mradi wa *REA III* mzunguko wa kwanza na kiliwashwa umeme Mwezi wa Oktoba 2019. Pamoja na kijiji cha Mahaha vijiji vingine vya Nobhola, Kabale na Nyasato ambavyo vimepitiwa na njia ya umeme msongo wa kilovoti 33 vimewashiwa umeme na kuunganisha wateja wa awali 63 kupitia transfoma mbili (2) za KVA 50. Vijiji vilivyobaki vitapelekewa umeme ifikapo Juni, 2021.

**SPIKA:** Katibu!

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 - Wizara ya Fedha na Mipango

**SPIKA:** Moja kwa moja nakukaribisha Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa hotuba yako.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti iliyochambua bajeti za mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2020/2021 naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na

Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2019/2020 na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu saba ya Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema pamoja na kituwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu kwa Taifa na leo amenipa kibali kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Mpango na Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa moyo wa dhati kabisa napenda kutoa shukrani zangu kwa kiongozi wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kusimamia Wizara ya Fedha na Mipango kwa kipindi chote cha muhula wa kwanza wa Serikali yake. Ni heshima kubwa kwangu kufanya kazi chini ya Kiongozi Mkuu wa Nchi huyu ambaye ana upeo mkubwa sana, mchapakazi, mwenye uzalendo wa kweli na ambaye ameistaajabisha dunia kwa kutekeleza mambo makubwa ya kimaendeleo kwa kipindi kifupi.

Mheshimiwa Spika, itoshe tu kusema namshukuru sana naendelea kumuombea afya njema yeye na familia yake ili kazi kubwa aliyoianza ya kuwaletea maendeleo makubwa wananchi wa Watanzania iweze kukamilika. Ahadi yangu kwa Mheshimiwa Rais na Watanzania ni kuwa nitaendelea kuchapa kazi katika kipindi chote cha utumishi wangu ili kuenzi nafasi hii adhimu niliyokabidhiwa ya kutoa mchango wangu kwa mama Tanzania.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda nitumie jukwaa hili kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna alivyojitoa katika kuwahudumia Watanzania. Nimefurahi kufanya kazi chini yao ni ninawasihi

Watanzania kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia wasaidizi hawa waandamizi wa Mheshimiwa Rais ambao ni makini na wenye mapenzi ya dhati na nchi yao. Tuendelee kwa pamoja kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu ili waendelee kuwa na afya njema na pia hekima na busara katika kazi zao za kumsaidia Kiongozi Mkuu wa Nchi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kusimamia mhimili huu wa Bunge kwa umahiri mkubwa sana. Aidha, ninakupongeza pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuongoza vyema majadiliano ya Bajeti za Wizara mbalimbali. Naomba pia nitumie fursa hii kuishukuru kipekee Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, kwa maoni, ushauri na mapendekezo mazuri waliyotupatia wakati wa kuchambua mapendekezo ya bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, nakiri kwamba mimi binafsi pamoja na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Mbunge na Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara yetu na Taasisi zake, tumejifunza mambo mengi mazuri kutokana na hoja na ushauri kwa Kamati hii nyeti. Vilevile napenda nitumie fursa hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wote wa Serikali ya Awamu ya Tano kwa kusimamia majukumu ya Wizara zao vizuri na kupelekea kupatikana kwa mafanikio makubwa katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 mpaka mwaka 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitumia nafasi hii kumpongeza sana Comredi Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Aidha, natoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kumpoteza Mheshimiwa Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga aliyekuwa Mbunge wa kuteuliwa CCM na Waziri wa Katiba na Sheria; Mheshimiwa Rashid Ajali Akbar aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini CCM; Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Pangalile Rwakatale aliyekuwa Mbunge Viti Maalum CCM na Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa *(Senator)*

aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Sumve CCM. Tunawaombea ili wapate rehemu kwa Mungu wapumzike kwa amani. Amina.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji Mbunge makini wa Kondoa na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa msaada anaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Nampongeza sana kwa uchapakazi na kujitoa kwake na napenda niwaombe wananchi wa Jimbo la Kondoa wamrejeshe kwa kishindo mama huyu hodari katika Bunge lijalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nawashukuru sana Watumishi wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu ambaye pia ni mlipaji Mkuu wa Serikali Bwana Doto James, Naibu Makatibu Wakuu, Amina Shaaban, Bwana Adolf Ndunguru na Bi. Mary Maganga kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Vilevile nawashukuru Wakuu wa Mashirika na Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Watumishi wote wa Taasisi hizo kwa ushirikiano walionipatia katika kipindi chote cha utumishi wangu kama Waziri wa Fedha na Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nijielekeze kwenye hoja yangu. Nitaanza kwa kuelezea mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara kwa mwaka 2019/2020, maeneo ya kipaumbele pamoja na mikakati mbalimbali ambayo itatekelezwa na Wizara kwa mwaka 2020/2021. Aidha, nitawasilisha Mpango na Bajeti ya mwaka 2020/2021 kwa mafungu saba ya Wizara, ambayo ni Fungu 7 – Ofisi ya Msajili wa Hazina, Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha, Fungu 13 – Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu, Fungu 21 – HAZINA, Fungu 22 – Deni la Taifa na Huduma Nyingine, Fungu 23 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali na Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ni kama

inavyooneshwa katika hotuba yangu kuanzia ukurasa wa tano hadi ukurasa wa nane.

Mheshimiwa Spika, naomba kulielekeza Bunge lako Tukufu kwa ufupi juu ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Machi, 2020 pamoja na Mpango na Bajeti kwa mwaka 2020/2021. Maelezo ya kina yapo katika hotuba yangu ukurasa wa nane hadi wa ukurasa wa 33.

Mheshimiwa Spika, kwanza Kubuni na Kusimamia Utekelezaji wa Sera za Uchumi Jumla. Pato la Taifa limekua kwa asilimia 7.0 katika mwaka 2019, kama ilivyokuwa mwaka 2018. Sekta zilizoongoza katika ukuaji ni pamoja na uchimbaji wa madini na mawe asilimia 17.7, ujenzi asilimia 14.1, sanaa na burudani asilimia 11.2 na usafirishaji na uhifadhi wa mizigo asilimia 8.7. Sekta zilizokuwa na mchango mkubwa katika pato la Taifa kwa mwaka 2019 ni: Kilimo (asilimia 26.6); Ujenzi (asilimia 14.3); Biashara na Matengenezo (asilimia 8.8); Viwanda (asilimia 8.5) na Usafirishaji na Uhifadhi wa Mizigo (asilimia 6.9). Aidha, mfumuko wa bei umeendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja ambapo kwa mwezi Machi, 2020, mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.4*. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi wa awali, shabaha za uchumi jumla katika mwaka 2020/2021 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pato halisi la Taifa linatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 4 mwaka 2020; mfumuko wa bei kubaki katika wigo wa tarakimu moja; nakisi ya bajeti ya Serikali kufikia asilimia 2.8; mapato ya ndani asilimia 14.5 ya Pato la Taifa; na mapato ya kodi asilimia 12.5 ya Pato la Taifa. Matarajio haya yameshuka kutokana na athari za mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu (unaosababishwa na Virusi vya *Corona*) kwenye sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pili ni Uandaaji, Utekelezaji na Usimamizi wa Mikakati, Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Bajeti ya Serikali. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020, Wizara

ilifanikiwa kuandaa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/2021; kuandaa taarifa ya Hiari ya Nchi Kuhusu Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 *(SDGs)*; kuunda mfumo wa kitaasisi wa ufuatiliaji na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030 pamoja na mfumo wa awali *(prototype)* wa Kanzidata ya Kuhifadhi na Kutoa Taarifa za Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Wizara imechukua hatua za kimkakati za kuimarisha ukusanyaji wa mapato kama inavyoonekana katika hotuba yangu ukurasa wa 11 hadi wa 14. Hatua hizo zimeiwezesha Serikali kukusanya mapato ya ndani ya jumla ya shilingi trilioni 16.06 katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, sawa na asilimia 92.4 ya lengo. Mapato ya ndani yameongezeka kutoka shilingi trilioni 14.07 hadi shilingi trilioni 16.06, sawa na asilimia 14.2 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, kati ya Julai, 2019 na Machi, 2020, Wizara imefanikisha upatikanaji wa fedha za misaada na mikopo nafuu ya jumla ya shilingi trilioni 2.04 sawa na asilimia 93 ya lengo la kipindi hicho la shilingi trilioni 2.78. Aidha, Wizara imefanikisha mkopo wa kiasi cha shilingi trilioni 3.44 kutoka katika soko la ndani, sawa na asilimia 101.5 ya lengo la kukopa shilingi trilioni 3.39 na mkopo wa shilingi trilioni 1.82 kutoka soko la nje sawa na asilimia 78.66 ya lengo la kukopa shilingi trilioni 2.32.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2020, jumla ya shilingi trilioni 24.69 zilitolewa kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 1.16 zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kielelezo na shilingi bilioni 597.54 kwa ajili ya kulipa madai yaliyohakikiwa.

Aidha, jumla ya shilingi bilioni 33.98 sawa na asilimia 84.95 ya bajeti iliyotengwa zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi 18 ya kimkakati inayotekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ni kubuni, kuunda na kusimamia mifumo ya usimamizi wa fedha na mali za Umma. Wizara imeboresha Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali kwa kuongeza huduma kwa njia ya simu za kiganjani *(GePG application mobile)* na kwa kuunganisha mfumo huo na mifumo ya Mamlaka ya Mapato Tanzania ya ukusanyaji wa mapato. Utekelezaji wa jukumu la kubuni, kuunda na kusimamia mifumo ya usimamizi wa fedha na mali za Umma umefafanuliwa kwa kina katika hotuba yangu ukurasa wa 14 hadi ukurasa wa 15.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Sekta ya Fedha; hadi kufikia mwezi Machi, 2020, Wizara imefanikiwa kukamilisha uandaaji wa Kanuni za Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018 ambapo zilianza kutumika rasmi mwezi Novemba, 2019. Aidha, Wizara imeanza kutekeleza Mpango Maalum wa Elimu kwa Umma kuhusu sekta hii ili kujenga uelewa kwa wananchi. Vile vile, Wizara imekamilisha kuandaa Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha pamoja na Kanuni za Kumlinda Mtumiaji wa Huduma za Fedha. Ukurasa wa 16 mpaka wa 17 wa hotuba yangu unaainisha kwa kina kazi nyingine zilizofanyika katika kutekeleza jukumu hili muhimu kwa uchumi wetu kati ya Julai, 2019 na Machi, 2020.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Deni la Serikali; hadi kufikia mwezi Machi 2020, Serikali ilifanikiwa kulipa deni lake lote lililoiva lenye thamani ya shilingi trilioni 6.19. Kati ya kiasi hicho, Deni la Ndani ni shilingi trilioni 4.06 ikijumuisha riba shilingi trilioni 1.09 na mtaji shilingi trilioni 2.98. Aidha, Deni la Nje ni shilingi trilioni 2.13 ikijumuisha riba ya shilingi bilioni 636.75 na mtaji shilingi trilioni 1.49*. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi; hadi kufikia mwezi Machi, 2020, Wizara imefanikisha kutungwa kwa Kanuni za Sheria ya Ubia ya Mwaka 2020 na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 37. Aidha, Wizara imeendelea kupokea, kuchambua na kutoa ushauri kwa Mamlaka za Serikali zinazotekeleza miradi ya *PPP* ipatayo 10 ambayo ipo katika hatua za awali za kutafuta

wabia, washauri elekezi, kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021, Wizara inatarajia kukamilisha taratibu za kuanzisha Kituo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi –*(PPP Center)*.

Mheshimiwa Spika**,** Ofisi ya Msajili wa Hazina imeendelea kutekeleza jukumu lake la Usimamizi wa Taasisi na Mashirika ya Umma kama inavyoonekana katika hotuba yangu ukurasa wa 23 mpaka 24. Aidha, hadi kufikia mwezi Machi 2020, Mfuko Mkuu wa Serikali umepokea jumla ya shilingi bilioni 612.87 kutoka kwenye Taasisi na Mashirika ya Umma kama gawio na michango ya Mashirika.

Mheshimiwa Spika, Wizara inasimamia Taasisi tano (5) za mafunzo ya elimu ya juu na Bodi mbili (2) za kitaaluma na kitaalamu ambazo ni Chuo cha Usimamizi wa Fedha *(IFM);* Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, Taasisi ya Uhasibu Tanzania, Chuo cha Uhasibu Arusha, Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika, Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu *(NBAA).*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hizo na mpango wa utekelezaji kwa mwaka 2020/2021 ni kama inavyoonekana katika kitabu cha hotuba yangu ukurasa wa 24 mpaka 27.

Mheshimiwa Spika, kati ya mwezi Julai, 2019 na Machi, 2020, Wizara imelipa mafao na pensheni kwa wastaafu wa Serikali 57,605, mirathi kwa warithi 1,006 na malipo ya kiinua mgongo kwa watumishi 457 wa Serikali walio kwenye mikataba.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara imeandaa vitambulisho vipya vya wastaafu vya kielektroniki katika mfumo wa *smart cards* na kuboresha mfumo unaotumika kutoa huduma kwa njia ya mtandao na kudhibiti fedha za

mirathi zinazotoka Hazina kwenda moja kwa moja kwenye akaunti za warithi *(Tanzania Pensioners Payment System).*

Mheshimiwa Spika, Tume ya Pamoja ya Fedha. Katika mwaka 2019/2020, Tume ya Pamoja ya Fedha imefanya stadi maalum kuhusu mfumo wa biashara kati ya Tanzania Bara na Zanzibar na Mwenendo wa Mapato ya Muungano. Aidha, Tume imefanya uchambuzi wa taarifa na takwimu halisi za mapato na matumizi ya Muungano kwa mwaka 2017/2018, mwaka 2018/2019 na mwaka 2019/2020. Taarifa ya uchambuzi wa takwimu hizo ilijadiliwa na Sekretarieti ya Tume mwezi Februari, 2020 na Serikali za pande zote zinaendelea kufanyia kazi mapendekezo yaliyomo katika taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Michezo ya kubahatisha. Hadi kufikia mwezi Machi 2020, Wizara imewezesha marekebisho ya Sheria ya Michezo ya Kubahatisha sura 41 ili kuipa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha mamlaka ya kuratibu, kusimamia na kudhibiti matangazo ya michezo ya kubahatisha. Aidha, Bodi inaendelea kuunda na kuunganisha mifumo ya TEHAMA ili kuimarisha udhibiti wa michezo ya kubahatisha.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Katika kuimarisha uwazi na uwajibikaji kwenye matumizi ya rasilimali za umma, hadi kufikia mwaka 2020, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imefanya ukaguzi kwa mafungu 66 ya Wizara na Idara mbalimbali za Serikali; Wakala 33; Taasisi 48; Balozi 42; Vyama vya Siasa 19; Bodi za Mabonde ya Maji 14; Hospital za Rufaa 27, Mashirika ya Umma 150; Mamlaka za Serikali za Mitaa 185; Mikoa 26; na Mifuko Maalumu 16. Aidha, ofisi imefanikiwa kufanya ukaguzi wa usimamizi wa mikataba ya ujenzi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 19. Lakini vile vile, ukaguzi umefanyika kwa miradi ya maendeleo 435 ikijumuisha miradi 65 ya Serikali Kuu na miradi 370 ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imepanga kuimarisha ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo hadi ngazi za Tarafa, Kata na Vijiji; kufanya ukaguzi wa miradi mikubwa ya maendeleo hususan Reli ya

Kisasa, Vivuko, Bomba la Gesi Mtwara na Ukarabati wa Reli ya Kati. Kupanua mawanda ya ukaguzi katika eneo la uchimbaji wa madini, mafuta na gesi ikiwemo kuimarisha ukaguzi wa kiuchunguzi na kiufundi na kuendelea kufanya ukaguzi wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma pamoja na kufanya ukaguzi na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Changamoto na Mikakati ya Kukabiliana Nazo. Utekelezaji wa majukumu ya Wizara unakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo tunaendelea kukabiliana nazo kwa kushirikiana na wadau wengine ili zisilete athari hasi katika malengo tuliyojiwekea. Baadhi ya changamoto hizo ni zifuatazo:-

i. Kasi ndogo ya ufuatiliaji na tathmini ya miradi na programu za maendeleo katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala, Taasisi za Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

ii. Mabadiliko ya mara kwa mara ya teknolojia ya mifumo ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato yanayoleta uhitaji wa upatikanaji wa teknolojia mpya na kuboresha na kuhuisha teknolojia ya mifumo iliyopo ili kuongeza ufanisi;

iii. Kuongezeka kwa gharama za mikopo kwenye masoko ya fedha duniani kutokana na mabadiliko ya sera za fedha katika nchi zilizoendelea;

iv. Uharibifu wa miundombinu ya barabara na madaraja kutokana na mafuriko; na

v. Mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona *(COVID-19).*

Mheshimiwa Spika, Mikakati ya Kukabiliana na Changamoto. Baadhi ya hatua zinazochukuliwa na Wizara katika kukabiliana na changamoto za utekelezaji wa majukumu yake ni pamoja na kuanza mchakato wa kutunga sera na mkakati wa ufuatiliaji na tathmini ya miradi na programu za maendeleo. Kujenga uwezo wa wataalam wa

ndani. Kuhamasisha wadau wa ndani kuendelea kushiriki katika minada ya dhamana za Serikali pamoja na kutafuta vyanzo vingine vya mikopo ya nje yenye riba nafuu.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia imekamilisha uchambuzi wa taarifa mbalimbali za kisekta ili kubaini kiwango cha athari zizazotokana na mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya Corlona *(Covid-19)* katika uchumi na kuainisha mikakati ya muda mfupi, wa kati na mrefu ya kukabiliana nazo. Taarifa jumuishi ya mikakati ya kupambana na Corona imewasilishwa kwenye ngazi za maamuzi Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2020/2021. Katika mwaka 2020/2021, Wizara inakadiria kukusanya maduhuli shilingi bilioni 973.02 kutoka vyanzo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na gawio, kodi za pango, marejesho ya mikopo na michango kutoka taasisi na mashirika, mauzo ya leseni za udalali na nyaraka za zabuni. Mchanganuo wa maduhuli ambayo yanakadiriwa kukusanywa tumeonesha kwenye kitabu cha hotuba ukurasa wa 34 Jedwali Na. 4.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Matumizi. Katika mwaka 2020/2021, Wizara ya Fedha na Mipango inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 12.39 kwa mafungu yote saba (7) kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 11.79 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 659 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya matumizi ya kawaida, shilingi trilioni 10.48 kwa ajili ya deni la Serikali, shilingi bilioni 750.29 matumizi mengineyo na shilingi bilioni 510 kwa ajili ya mishahara na marekebisho ya mishahara. Aidha, matumizi ya maendeleo yanajumuisha shilingi bilioni 624.7 fedha za ndani na shilingi bilioni 34.61 fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha, Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 80.5 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 68.87 ni

matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 11.66 matumizi ya maendeleo. Matumizi ya kawaida yanajumuisha shilingi bilioni 14.88 kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 53.99 matumizi mengineyo. Matumizi ya maendeleo yanajumuisha shilingi bilioni 6.70 fedha za ndani na shilingi bilioni 4.96 fedha za nje. Mchanganuo wa kiasi kinachoombwa kwa kila fungu umeainishwa katika Jedwali Na. 5 kwenye hotuba yangu ukurasa wa 35.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho; kama nilivyotangulia kusema, Mkutano huu wa Bunge ni wa mwisho katika muhula huu wa kwanza wa Serikali ya Awamu ya Tano. Napenda kutumia fursa hii kukiri kuwa, katika kipindi chote cha muhula huu, Wizara imenufaika sana na maoni na ushauri kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao umesaidia kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi na kuimarisha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine, naomba nirudie kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufanya kazi yake hii ya Waziri wa Fedha na Mipango aliyonipa kupitia kwa uteuzi wa Mheshimiwa Rais. Aidha, namshukuru tena Mheshimiwa Rais, kwa kuendelea kuniamini katika nafasi hii ngumu kwa miaka mitano mfululizo. Vilevile napenda kuwashukuru wananchi wote wa Tanzania hususan kwa kufanya kazi na kulipa kodi ili kujenga uchumi wa nchi yetu. Nawaomba Watanzania tuendelee kuchapa kazi kama alivyotuasa Mheshimiwa Rais wetu na kuitekeleza kwa vitendo kaulimbiu ya *"HAPA KAZI TU".*

Mheshimiwa Spika, kutokana na janga la mlipuko wa *Corona*, napenda kuchukua nafasi hii kutoa pole kwa wananchi wote waliopatwa na madhara yatokanayo na janga hili na kuwaasa kuendelea kuchukua hatua za kujikinga na ugonjwa huu kama inavyoelekezwa na wataalamu wa afya. Napenda pia kuwapongeza kwa dhati madaktari na watumishi wote wa afya walio mstari wa mbele siku zote katika kutoa huduma kwa wananchi hasa wanyonge na hususan katika kipindi hiki cha mlipuko wa *Covid-19* hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda nikushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha hoja hii pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Aidha nawashukuru wote walioshiriki katika maandalizi ya hotuba hii na kuhakikisha inakamilika kwa wakati. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya *www.mof.go.tz.*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**MAELEZO YA MHESHIMIWA DKT. PHILIP I. MPANGO (MB.), WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO WAKATI AKIWASILISHA BUNGENI HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NAMIPANGO KWA MWAKA 2020/2021 – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, iliyochambua bajeti za mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2020/21, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2019/20 na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu saba (7) ya Wizara pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2020/21.

1. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia afya njema pamoja na kutuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu kwa Taifa na leo amenipa kibali kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Mpango na Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka ujao wa fedha.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa moyo wa dhati kabisa, napenda kutoa shukrani zangu kwa kiongozi wetu, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kusimamia Wizara ya Fedha na Mipango kwa kipindi chote cha muhula wa kwanza wa Serikali yake. Ni heshima kubwa kwangu kufanya kazi chini ya Kiongozi Mkuu wa nchi huyu ambaye ana upeo mkubwa sana, mchapa kazi, mwenye uzalendo wa kweli na ambaye ameistaajabisha dunia kwa kutekeleza mambo makubwa ya kimaendeleo kwa kipindi kifupi. Itoshe tu kusema namshukuru sana, naendelea kumuombea afya njema yeye na familia yake ili kazi kubwa aliyoianza ya kuwaletea maendeleo makubwa wananchi wa Tanzania iweze kukamilika. Ahadi yangu kwa Mheshimiwa Rais na Watanzania ni kuwa, nitaendelea kuchapa kazi katika kipindi chote cha utumishi wangu ili kuenzi nafasi hii adhimu niliyokabidhiwa ya kutoa mchango wangu kwa mama Tanzania.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, napenda nitumie jukwaa hili kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati kabisa, Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Kassim M. Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna walivyojitoa katika kuwahudumia Watanzania. Nimefurahi kufanya kazi chini yao na ninawasihi Watanzania kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia wasaidizi hawa waandamizi wa Mheshimiwa Rais ambao ni makini na wenye mapenzi ya dhati kwa nchi yao. Tuendelee kwa pamoja kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu ili waendelee kuwa na afya njema na pia hekima na busara katika kazi zao za kumsaidia Kiongozi Mkuu wa Nchi.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kukupongeza wewe binafsi, kwa kusimamia mhimili huu wa Bunge kwa umahiri mkubwa sana. Aidha, ninakupongeza pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuongoza vyema majadiliano ya Bajeti za Wizara mbalimbali. Naomba pia nitumie fursa hii kuishukuru kipekee Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Mashimba

Mashauri Ndaki (Mb.), kwa maoni, ushauri na mapendekezo mazuri waliyotupatia wakati wa kuchambua mapendekezo ya Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2020/21. Nakiri kwamba mimi binafsi, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb.), Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara yetu na taasisi zake tumejifunza mambo mengi mazuri kutokana na hoja na ushauri wa Kamati hii nyeti. Vile vile, napenda nitumie fursa hii, kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wote wa Serikali ya Awamu ya Tano kwa kusimamia majukumu ya Wizara zao vizuri na kupelekea kupatikana kwa mafanikio makubwa katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi 2015 - 2020.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie pia nafasi hii kumpongeza sana Comred Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Aidha, natoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kumpoteza Mhe. Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga aliyekuwa Mbunge wa Kuteuliwa - CCM na Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Rashid Ajali Akbar, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini-CCM, Mhe. Mchungaji Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare, aliyekuwa Mbunge Viti Maalum – CCM na Mhe. Richard Mganga Ndassa (Senator) aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Sumve-CCM. Tunawaombea ili wapate rehema kwa Mungu, wapumzike kwa amani. Amina.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, Mbunge makini wa Kondoa na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, kwa msaada mkubwa anaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Nampongeza sana kwa uchapakazi na kujitoa kwake na napenda niwaombe Wananchi wa Jimbo la Kondoa wamrejeshe kwa kishindo mama huyu Hodari katika Bunge lijalo. Aidha, nawashukuru sana watumishi wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu ambaye pia ni Mlipaji Mkuu wa Serikali, Bw. Doto M. James, Naibu Makatibu Wakuu Bi. Amina Kh. Shaaban, Bw. Adolf H. Ndunguru na Bi. Mary N. Maganga kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Vile vile, nawashukuru Wakuu wa Mashirika na Taasisi zilizo chini

ya Wizara ya Fedha na Mipango (CAG, BOT, TRA, NBS, TR, TRAT, TRAB, Benki za Serikali, Taasisi 5 za mafunzo ya Elimu ya Juu na Bodi za Kitaaluma na Kitaalam) pamoja na watumishi wote wa taasisi hizo kwa ushirikiano walionipatia katika kipindi chote cha utumishi wangu kama Waziri wa Fedha na Mipango.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba sasa nijielekeze kwenye hoja yangu. Nitaanza kwa kuelezea mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara kwa mwaka 2019/20, maeneo ya kipaumbele pamoja na mikakati mbalimbali ambayo itatekelezwa na Wizara kwa mwaka 2020/21. Aidha, nitawasilisha Mpango na Bajeti ya mwaka 2020/21 kwa mafungu saba (7) ya Wizara ambayo ni Fungu 7 – Ofisi ya Msajili wa Hazina, Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha, Fungu 13 – Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu, Fungu 21 – HAZINA, Fungu 22 – Deni la Taifa na Huduma Nyingine, Fungu 23 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali na Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

## 2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2019/20 NA MALENGO YA MWAKA 2020/21

### Mapitio ya Mapato na Matumizi

8. ***Mheshimiwa Spika,*** mapitio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/20 ni kama inavyooneshwa katika hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 5 hadi ukurasa wa 8.

### Utekelezaji wa Majukumu kwa mwaka 2019/20 na Mpango wa Mwaka 2020/21

9. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kulielekeza Bunge lako Tukufu kwa ufupi juu ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Machi 2020 pamoja na Mpango na Bajeti ya mwaka 2020/21. Maelezo ya kina yapo katika hotuba yangu ukurasa wa 8 hadi wa 33.

**(i) Kubuni na Kusimamia Utekelezaji wa Sera za Uchumi Jumla**

10. ***Mheshimiwa Spika,*** Pato la Taifa limekua kwa asilimia 7.0 mwaka 2019, kama ilivyokuwa mwaka 2018. Sekta zilizoongoza katika ukuaji ni pamoja na Uchimbaji wa Madini na Mawe asilimia 17.7, Ujenzi asilimia 14.1, Sanaa na Burudani asilimia 11.2 na Usafirishaji na Uhifadhi wa Mizigo asilimia 8.7. Sekta zilizokuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa kwa mwaka 2019 ni: Kilimo (asilimia 26.6); Ujenzi (asilimia 14.3); Biashara na Matengenezo (asilimia 8.8); Viwanda (asilimia 8.5) na Usafirishaji na Uhifadhi mizigo (asilimia 6.9). Aidha, mfumuko wa bei umeendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja ambapo kwa mwezi Machi 2020, ulikuwa asilimia 3.4.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na uchambuzi wa awali, shabaha za uchumi jumla katika mwaka 2020/21 ni kama ifuatavyo: Pato halisi la Taifa linatarajiwa kukua kwa asilimia 4.0 mwaka 2020; mfumuko wa bei kubaki katika wigo wa tarakimu moja; nakisi ya bajeti ya Serikali kufikia asilimia 2.8; mapato ya ndani asilimia 14.5 ya Pato la Taifa; na mapato ya kodi asilimia 12.5 ya Pato la Taifa. Matarajio haya yanatarajiwa kupungua kutegemea ukubwa wa athari za mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu (unaosababishwa na Virusi vya CORONA) kwenye sekta mbalimbali.

**(ii) Uandaaji, Utekelezaji na Usimamizi wa Mikakati, Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Bajeti ya Serikali**

12. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Machi 2020, Wizara ilifanikiwa kuandaa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/21; kuandaa taarifa ya Hiari ya Nchi Kuhusu Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 (*SDGs*); kuunda mfumo wa kitaasisi wa ufuatiliaji na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 pamoja na mfumo wa awali (*prototype*) wa Kanzidata ya Kuhifadhi na Kutoa Taarifa za Miradi ya Maendeleo.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imechukua hatua za kimkakati za kuimarisha ukusanyaji wa mapato kama zinavyoonekana katika hotuba yangu ukurasa wa 11 hadi wa 14. Hatua hizo zimeiwezesha Serikali kukusanya mapato ya ndani ya jumla ya shilingi trilioni 16.06 katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, sawa na asilimia 92.4 ya lengo. Mapato ya ndani yameongezeka kutoka shilingi trilioni 14.07 hadi shilingi trilioni 16.06, sawa na asilimia 14.2 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2018/19.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya Julai 2019 na Machi 2020, Wizara imefanikisha upatikanaji wa fedha za misaada na mikopo nafuu ya jumla ya **shilingi trilioni 2.04** sawa na asilimia 93 ya lengo la kipindi hicho la **shilingi trilioni 2.78**. Aidha, Wizara imefanikisha mkopo wa kiasi cha **shilingi trilioni 3.44** kutoka katika soko la ndani, sawa na asilimia 101.5 ya lengo la kukopa **shilingi trilioni 3.39** na mkopo wa **shilingi trilioni 1.82** kutoka soko la nje sawa na asilimia 78.66 ya lengo la kukopa **shilingi trilioni 2.32.**

15. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Machi 2020, jumla ya **shilingi trilioni 24.65** zilitolewa kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali. Kati ya kiasi hicho, **shilingi trilioni 1.16** zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kielelezo na **shilingi bilioni 597.54** kwa ajili ya kulipa madai yaliyohakikiwa. Aidha, jumla ya **shilingi bilioni 33.98** sawa na asilimia **84.95** ya bajeti iliyotengwa zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi 18 ya kimkakati inayotekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

### (iii) Kubuni, Kuunda na Kusimamia Mifumo ya Usimamizi wa Fedha na Mali za Umma

16. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeboresha Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali (*GePG*) kwa kuongeza huduma kwa njia ya simu za kiganjani (*GePG application mobile*) na kwa kuunganisha mfumo huo na mifumo ya Mamlaka ya Mapato Tanzania ya ukusanyaji wa mapato. Utekelezaji wa jukumu la kubuni, kuunda na kusimamia mifumo ya usimamizi wa fedha na mali za umma

umefafanuliwa kwa kina katika hotuba yangu ukurasa wa 14 hadi wa 15.

### (iv) Usimamizi wa Sekta ya Fedha

17. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Machi 2020, Wizara imefanikiwa kukamilisha uandaaji wa Kanuni za Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018 ambapo zilianza kutumika rasmi mwezi Novemba 2019. Aidha, Wizara imeanza kutekeleza Mpango Maalum wa Elimu kwa Umma kuhusu sekta hii ili kujenga uelewa kwa wananchi. Vile vile, Wizara imekamilisha kuandaa Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha pamoja na Kanuni za Kumlinda Mtumiaji wa Huduma za Fedha. Ukurasa wa 16 -17 wa hotuba yangu unaainisha kwa kina kazi nyingine zilizofanyika katika kutekeleza jukumu hili muhimu kwa uchumi wetu kati ya Julai 2019 na Machi 2020.

### (v) Usimamizi wa Deni la Serikali

18. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Machi 2020, Serikali ilifanikiwa kulipa deni lake lote lililoiva lenye thamani ya **shilingi trilioni 6.19**. Kati ya kiasi hicho, Deni la Ndani ni **shilingi trilioni 4.06** ikijumuisha riba **shilingi trilioni 1.09** na mtaji **shilingi trilioni 2.98**. Aidha, Deni la Nje ni **shilingi trilioni 2.13** ikijumuisha riba ya **shilingi bilioni 636.75** na mtaji **shilingi trilioni 1.49.**

### (vi) Ubia kati ya Sekta ya umma na sekta binafsi

19. ***Mheshimiwa Spika****,* hadi kufikia mwezi Machi 2020, Wizara imefanikisha kutungwa kwa Kanuni za Sheria ya Ubia za Mwaka 2020 na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na.37. Aidha, Wizara imeendelea kupokea, kuchambua na kutoa ushauri kwa Mamlaka za Serikali zinazotekeleza miradi ya PPP ipatayo 10 ambayo ipo katika hatua za awali za kutafuta wabia, washauri elekezi, kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Wizara inatarajia kukamilisha taratibu za kuanzisha kituo cha ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi - *PPP Center*.

**(vii) Usimamizi wa Taasisi na Mashirika ya Umma**

21. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Msajili wa Hazina imeendelea kutekeleza jukumu lake la Usimamizi wa Taasisi na Mashirika ya Umma kama inavyooneka katika hotuba yangu ukurasa wa 23 -24. Aidha, hadi kufikia mwezi Machi 2020, Mfuko Mkuu wa Serikali umepokea jumla ya **shilingi bilioni 612.87** kutoka kwenye Taasisi na Mashirika ya Umma kama gawio na michango ya Mashirika.

**(viii) Taasisi za Mafunzo ya Elimu ya Juu na Bodi za Kitaaluma na Kitaalamu**

22. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inasimamia Taasisi tano (5) za mafunzo ya elimu ya juu na Bodi mbili (2) za kitaaluma na kitaalamu ambazo ni: Chuo cha Usimamizi wa Fedha -IFM; Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini – IRDP; Taasisi ya Uhasibu Tanzania – TIA; Chuo cha Uhasibu Arusha –IAA; Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika – EASTC; Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi – PSPTB na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu – NBAA. Utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizo na mpango wa utekelezaji kwa mwaka 2020/21 ni kama inavyoonekana katika kitabu cha hotuba yangu ukurasa wa 24 -27.

**(ix) Mafao ya Wastaafu na Mirathi**

23. ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya mwezi Julai 2019 na Machi 2020, Wizara imelipa mafao na pensheni kwa wastaafu wa Serikali **57,605**, mirathi kwa warithi **1,006** na malipo ya kiinua mgongo kwa watumishi **457** wa Serikali walio kwenye mikataba. Aidha, Wizara imeandaa vitambulisho vipya vya wastaafu vya kielektroniki katika mfumo wa "*smart cards*" na kuboresha Mfumo wa unaotumika kutoa huduma kwa njia ya mtandao na kudhibiti fedha za mirathi zinazotoka HAZINA kwenda moja kwa moja kwenye akaunti za warithi (*Tanzania Pensioners Payment System – TPPS)*.

**(x) Tume ya Pamoja ya Fedha**

24. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/20, Tume ya Pamoja ya Fedha imefanya stadi maalum kuhusu Mfumo wa

Biashara kati ya Tanzania Bara na Zanzibar na Mwenendo wa Mapato ya Muungano. Aidha, Tume imefanya uchambuzi wa taarifa na takwimu halisi za Mapato na Matumizi ya Muungano kwa mwaka 2017/18, mwaka 2018/19 na 2019/20. Taarifa ya uchambuzi wa takwimu hizo ilijadiliwa na Sekretarieti ya Tume mwezi Februari, 2020 na Serikali za pande zote zinaendelea kufanyia kazi mapendekezo yaliyomo katika taarifa hiyo.

**(xi) Sekta ya Michezo ya kubahatisha**

25. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Machi 2020, Wizara imewezesha marekebisho ya Sheria ya Michezo ya Kubahatisha SURA 41 ili kuipa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha mamlaka ya kuratibu, kusimamia na kudhibiti matangazo ya michezo ya kubahatisha. Aidha, Bodi inaendelea kuunda na kuunganisha mifumo ya TEHAMA ili kuimarisha udhibiti wa michezo ya kubahatisha.

**(xii) Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

26. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha uwazi na uwajibikaji kwenye matumizi ya rasilimali za umma, hadi kufikia Machi 2020, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imefanya ukaguzi kwa mafungu **66** ya Wizara na Idara za Serikali; Wakala **33**; Taasisi **48**; Balozi **42**; Vyama vya Siasa **19**; Bodi za Mabonde ya Maji **14**; Hospital za Rufaa **27**, Mashirika ya Umma **150**; Mamlaka za Serikali za Mitaa **185**; Mikoa **26**; na Mifuko Maalumu **16**. Aidha, ofisi imefanikiwa kufanya ukaguzi wa usimamizi wa mikataba ya ujenzi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa **19**. Vile vile, ukaguzi umefanyika kwa miradi ya maendeleo **435** ikijumuisha miradi **65** ya Serikali Kuu na miradi **370** ya Serikali za Mitaa.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imepanga kuimarisha ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo hadi ngazi za Tarafa, Kata na Vijiji; kufanya ukaguzi wa miradi mikubwa ya maendeleo (Reli ya Kisasa, Vivuko, Bomba la Gesi Mtwara na Ukarabati wa Reli ya Kati); kupanua mawanda ya ukaguzi katika eneo la uchimbaji wa madini, mafuta na gesi ikiwemo kuimarisha ukaguzi wa

kiuchunguzi na kiufundi; na kuendelea kufanya ukaguzi wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma pamoja na kufanya ukaguzi wa ufanisi.

## Changamoto na Mikakati ya Kukabiliana nazo

### Changamoto

28. ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa majukumu ya Wizara unakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo tunaendelea kukabiliana nazo kwa kushirikiana na wadau wengine ili zisilete athari hasi katika malengo tuliyojiwekea. Baadhi ya changamoto hizo ni:

(i) Kasi ndogo ya ufuatiliaji na tathmini ya miradi na programu za maendeleo katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Taasisi za Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(ii) Mabadiliko ya mara kwa mara ya teknolojia ya mifumo ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato yanayoleta uhitaji wa upatikanaji wa teknolojia mpya na kuboresha na kuhuisha teknolojia ya mifumo iliyopo ili kuongeza ufanisi;

(iii) Kuongezeka kwa gharama za mikopo kwenye masoko ya fedha duniani kutokana na mabadiliko ya sera za fedha katika nchi zilizoendelea (hususan Marekani na Nchi za Ulaya);

(iv) Uharibifu wa miundombinu ya barabara na madaraja kutokana na mafuriko; na

(v) Mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona (COVID-19).

### Mikakati ya Kukabiliana na Changamoto

29. ***Mheshimiwa Spika***, Baadhi ya hatua zinazochukuliwa na Wizara katika kukabiliana na changamoto za utekelezaji wa majukumu yake ni pamoja na:

(i) Kuanza mchakato wa kutunga sera na mkakati wa ufuatiliaji na tathmini ya miradi na programu za maendeleo;

(ii) Kujenga uwezo wa wataalam wa ndani katika kubuni, kuunda na kuhuisha teknolojia ya mifumo ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato;

(iii) Kuhamasisha wadau wa ndani kuendelea kushiriki katika minada ya dhamana za Serikali pamoja na kutafuta vyanzo vingine vya mikopo ya nje vyenye riba nafuu; na

(iv) Wizara imekamilisha uchambuzi wa taarifa mbalimbali za kisekta ili kubaini kiwango cha athari zitokanazo na mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona (COVID-19) katika uchumi na kuainisha mikakati ya muda mfupi, wa kati na mrefu ya kukabiliana nazo. Taarifa jumuishi ya mikakati ya kupambana na CORONA imewasilishwa kwenye ngazi za maamuzi Serikalini.

## 3.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2020/21

### (i) Makadirio ya Mapato

30. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Wizara inakadiria kukusanya maduhuli ya kiasi cha **shilingi bilioni 973.02** kutoka katika vyanzo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na gawio, kodi za pango, marejesho ya mikopo, michango kutoka katika taasisi na mashirika ya umma, mauzo ya leseni za udalali na nyaraka za zabuni. Mchanganuo wa maduhuli yanayokadiriwa kukusanywa umeoneshwa katika kitabu cha hotuba ukurasa wa 34 katika Jedwali Na. 4.

### (ii) Makadirio ya Matumizi

31. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Wizara ya Fedha na Mipango inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi trilioni 12.39** kwa mafungu yote saba (7) kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, **shilingi trilioni 11.73** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi bilioni**

**659** kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya matumizi ya kawaida, **shilingi trilioni 10.48** kwa ajili ya deni la Serikali, **shilingi bilioni 750.29** matumizi mengineyo na **shilingi bilioni 510** kwa ajili ya mishahara na marekebisho ya mishahara. Aidha, matumizi ya maendeleo yanajumuisha **shilingi bilioni 624.7** fedha za ndani na **shilingi bilioni 34.61** fedha za nje.

32. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/21, Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **shilingi bilioni 80.5** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Kati ya kiasi hicho, **shilingi bilioni 68.87** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi bilioni 11.66** matumizi ya maendeleo. Matumizi ya kawaida yanajumuisha **shilingi bilioni 14.88** kwa ajili ya mishahara na **shilingi bilioni 53.99** matumizi mengineyo. Aidha, matumizi ya maendeleo yanajumuisha **shilingi bilioni 6.70** fedha za ndani na **shilingi bilioni 4.96** fedha za nje. Mchanganuo wa kiasi kinachoombwa kwa kila fungu umeainishwa katika Jedwali Na. 5 lililopo katika hotuba yangu ukurasa wa 35.

## 4.0 HITIMISHO

33. ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyotangulia kusema awali, Mkutano huu wa Bunge ni wa mwisho katika muhula huu wa kwanza wa Serikali ya Awamu ya Tano. Napenda kutumia fursa hii kukiri kuwa, katika kipindi chote cha muhula huu, Wizara imenufaika sana na maoni na ushauri kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao umesaidia kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi na kuimarisha uchumi wa nchi yetu.

34. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mara nyingine, naomba nirudie kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufanya kazi yake hii ya Waziri wa Fedha na Mipango aliyonipa kupitia Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, namshukuru tena Mheshimiwa Rais, kwa kuendelea kuniamini katika nafasi hii ngumu kwa miaka mitano mfululizo. Vilevile, napenda kuwashukuru wananchi wote wa Tanzania hususan kwa kufanya kazi na kulipa kodi ili kujenga uchumi wa nchi yetu.

Nawaomba Watanzania tuendelee kuchapa kazi kama anavyotuasa Mheshimiwa Rais wetu na kuitekeleza kwa vitendo kaulimbiu ya "HAPA KAZI TU".

35. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na janga la mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona (COVID-19), napenda kuchukua fursa hii kutoa pole kwa wananchi wote waliopatwa na madhara yanayotokana janga hili na kuwaasa kuendelea kuchukua hatua za kujikinga na ugonjwa huu kama inavyoelekezwa na wataalamu wa afya. Aidha, napenda kuwapongeza kwa dhati madaktari na watumishi wote wa Afya walio mstari wa mbele siku zote katika kutoa huduma kwa wananchi hasa wanyonge na hususan katika kipindi hiki cha mlipuko wa COVID-19 nchini.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** mwisho kabisa, napenda nikushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha hoja hii pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Aidha, nawashukuru wote walioshiriki katika maandalizi ya hotuba hii na kuhakikisha inakamilika kwa wakati. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya *www.mof.go.tz.*

37. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Asante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa kusoma hotuba ya Wizara yako vizuri kabisa na kwa ufasaha; tunakushukuru sana, tunakushukuru sana. Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe kwamba leo ni siku ya kupiga kura, kwa hiyo endeleeni kupiga kura na mimi nitakuwa naziona hapa kadri zinavyokuja.

Kabla sijamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na yeye kusoma nitangulize shukrani zetu nyingi sana kwa Serikali na kipekee kwa Mheshimiwa Rais kwa kufanikisha zoezi la kuwarudisha Watanzania wenzetu waliokuwa kule India,

walikuwa wagonjwa kule India. Tumeweza kama taifa kuwarudisha ndugu zetu; na tunataarifiwa kwamba saa sita na nusu leo mchana ndege imetua Dar es Salaam ikirudi na wagonjwa wetu. *(Makofi)*

Hili ni jambo la kujivunia sana, ni jambo muhimu, Bunge hili linaipongeza sana sana Serikali kwa hatua hiyo kubwa na muhimu ambayo mmeichukua, ni historia kwa kweli ambayo itaandikwa na kukumbukwa kwa muda mrefu; kwamba awamu ya tano imewahi kufanya jambo hili muhimu.

Ahsante sana, mtaona kwamba hotuba ya Upinzani hatujaikubali leo, na sababu zake zipo wazi tu. Kwamba mwandishi wa hotuba hiyo Mheshimiwa Halima Mdee ni katika waliojifukuza wenyewe hapa Bungeni bila kufukuzwa na mtu yeyote; kwamba wao roho zao ni za muhimu sana kuliko zetu sisi wengine wote; na asiye kuwepo basi na lake halipo. Na kwa kuwa sasa kuna masharti ambayo Spika alikwisha kuyatoa ili waweze kurudi na kuanza kushiriki Shughuli za Bunge, masharti hayo hayajatekelezwa kwa hiyo haiwezekani, *naturally* haiwezekani ukapitishia dirishani kazi zako zikafanyika wakati wewe mwenyewe hata uliko hakujulikani. *(Makofi)*

Kwa hiyo tunaendelea na shughuli, Mwenyekiti wa Kamati tafadhali. Kamati ya Bajeti.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupa nafasi ya uzima lakini pili nikushukuru sana wewe kwa kunipa nafasi ili niweze kuwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango

kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ambayo inajumuisha Mafungu Saba (7). Mafungu hayo ni; Fungu Na. 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina, Fungu Na. 10 - Tume ya Pamoja ya Fedha, Fungu Na. 13 - Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu, Fungu Na. 21- Hazina, Fungu Na. 22 - Deni la Taifa, Fungu Na. 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali na Fungu Na. 50 - Wizara ya Fedha na Mipango. Taarifa hii inajumuisha pia Fungu Na. 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, tupitie kidogo utekelezaji wa Bajeti na Majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali. Hapa nitakachokisoma ni kwa kifupi tu lakini naomba Taarifa yote kadri inavyoonekana kwenye *tablets* zetu basi ionekane pia kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara ya Fedha na Mipango iliidhinishiwa na Bunge kutumia jumla ya shilingi 11,881,609,700,717 kwa mafungu yote saba (7). Kati ya fedha hizo Shilingi 11,157,327,758,988 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo yanajumuisha malipo ya deni la taifa ambayo ni pamoja na riba, deni la ndani na kwa ajili ya deni la nje zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2020 jumla ya shilingi 7,648,561,448,989 zilikuwa zimetolewa kwa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na mafungu yake yote, hii ikiwa ni sawa na asilimia 64.37 ya Bajeti yote ya Wizara kwa kipindi husika. Kati ya fedha hizo Shilingi 7,639,714,371,066, sawa na asilimia 68.47 ya lengo zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi 8,847,077,923 zilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na asilimia 1.22 ya Bajeti ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, tuangalie Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Fungu Na. 45. Kamati ilipitia Bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu

za Serikali ambapo kiasi cha shilingi 62,142,554,000 zikihusisha fedha za maduhuli kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali kiliidhinishwa kwa matumizi ya Ofisi hii katika mwaka wa 2019/2020. Kati ya fedha hizo, Shilingi 55,076,878,000 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, shilingi bilioni 6,300,000,000 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo na shilingi 765,676,000 ni fedha za makusanyo ya maduhuli.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2020 lilikuwa limepokea kiasi cha shilingi 46,431,843,915 sawa na asilimia 75.65. Kati ya fedha hizo shilingi 44,054,870,238 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 2,376,973,677 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ambayo ni sawa na asilimia 38 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Aidha, jumla ya shilingi 768,941,292 sawa na asilimia 100.4 zilikuwa za maduhuli zikiwa zimekusanywa na Ofisi.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Jumla Kuhusiana na Utekelezaji wa Bajeti kwa Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Kamati ya Bajeti imefanya uchambuzi katika mafungu saba (7) yaliyo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Fungu Na. 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali. Kamati imebaini kuwa hadi kufikia mwezi Machi, 2020 mafungu matatu (Fungu Na. 10, Fungu Na. 22, Fungu Na. 50) yote kwa pamoja yalipokea zaidi ya asilimia 60 ya fedha za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Mafungu mawili (Fungu Na. 13 na Fungu Na. 23) yalipokea zaidi ya asilimia 50 ya bajeti nzima ya fedha za matumizi ya kawaida. Mafungu mawili (Fungu Na. 07 na Fungu Na. 21) yalipokea chini ya asilimia 30 ya fedha za matumizi ya kawaida. Fungu moja (Fungu Na. 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali) ilipokea zaidi ya asilimia 60 ya fedha za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa na Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, aidha kwa upande wa fedha za maendeleo, kati ya mafungu saba (7) ni mafungu mawili tu yamepokea zaidi ya asilimia 50; nayo ni Fungu Na 13 na Fungu

Na. 23. Lakini Fungu Na. 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ilipokea asilimia 70 ya fedha za maendeleo. mafungu mengine matano yaliyobakia yalipokea fedha chini ya asilimia 30.

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu hizi utaona kuwa kati ya jumla ya Shilingi 724,281,941,731 zilizoidhishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ni kiasi cha shilingi 8,847,077,923 (sawa na asilimia 1.22) ndizo zimetolewa. Mwenendo huu si wa kuridhisha ukizingatia kuwa miradi mingi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango inahusu Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma, uboreshaji wa mifumo ya kiuhasibu kwa njia za kimtandao, uboreshaji wa mifumo ya ununuzi, utawala bora, ukarabati na ujenzi wa makazi. Hivyo ni dhahiri miradi hii imeathirika kwa kiwango kikubwa hasa ukizingatia kuwa Serikali imekuwa haitoi mchango wake wa fedha hasa fedha zile za ndani.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti inapenda kutoa ushauri kwa Wizara ya Fedha na Mipango kuwa sasa Dunia nzima inajielekeza kwenye mapambano ya ugonjwa wa *Covid-19,* hivyo ni dhahiri misaada na mikopo ya masharti nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo itapungua.

Mheshimiwa Spika, Tuangalie Uchambuzi wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Fungu Na. 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/ 2020. Kamati ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kufanya mashauriano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu hili.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa Fedha 2019/2020, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ilidhiinishiwa jumla ya kiasi cha Sh.61,376,878,000 kutoka Mfuko Mkuu kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo mishahara ni Sh.14,84,139,000, matumizi mengineyo ni Sh.40,992,736,000 na Sh.6,300,000,000 zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo fedha za ndani zilikuwa Sh.5,000,000,000 na Sh.1,300,000,000 ni fedha za nje. Kwa

upande wa maduhuli ofisi ilikadiriwa kukusanya kiasi cha Sh.765, 676,000; maduhuli ya ofisi hii yanatokana na marejesho ya gharama za ukaguzi kwa mashirika ya umma, ukaguzi wa miradi ya maendeleo inasimamiwa na Wizara chini ya *division* ya Serikali Kuu pamoja na ile miradi chini ya *division* ya hesabu za Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza bajeti hiyo hadi kufikia mwezi Machi, 2020, Ofisi hii ilikuwa imepokea jumla ya kiasi cha Sh.46,431,843,915 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, kiasi hicho ni sawa na asilimia 75.65. Kati ya kiasi hicho Sh.9,249,695,571 ni kwa ajili ya mishahara; Sh.32,161,747,099 ni kwa matumizi mengineyo na Sh.2,060,123,677 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kiasi hicho cha bajeti kilichotolewa kimewezesha ofisi kutekeleza shughuli mbalimbali zilizokuwa zimepangwa kulingana na Fedha zilizopokelewa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na makusanyo ya ndani. Aidha, mwenendo wa utolewaji wa Fedha kutoka Mfuko Mkuu kwa ofisi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo umebaki kuwa na changamoto ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2019/2020 kiasi kilichokuwa kimepokelewa na asilimia 38 tu ya makadirio. Hivyo ni vyema Serikali ikaangalia namna ya kuongeza Bajeti ya maendeleo katika ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya tathmini ya mwenendo wa sura ya Bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali iliyokuwa inatengewa na Serikali kwa kiasi cha miaka minne kuanzia 2017/2018 hadi 2020/2021. Bajeti ya Fungu 45 ilianza kushuka katika mwaka 2017/2018 hadi 2019/2020 ikilinganishwa na Bajeti inayoombewa mwaka 2020/2021. Aidha, mwaka 2020/2021, bajeti ya *NAOT* imeongezeka kwa asilimia 31. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza Bajeti ya ofisi hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla bajeti ya mwaka 2020/ 2021 imeongezeka kwa jumla ya Sh.19,168,057,373 ukilinganisha na ile ya mwaka 2019/2020. Kati ya kiasi kilichoongezeka fedha za matumizi mengineyo zimeongezeka kwa Sh.13,001,373,000 na matumizi ya maendeleo yameongezeka kwa Sh.5,367,940,000. Aidha,

ongezeko hili linapelekea pia kuongezeka kwa mawanda ya ukaguzi ambayo awali yalikuwa hayafanyiki kutokana na ukosefu wa fedha pamoja na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, sasa tuangalie makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Katika mwaka wa fedha 2020/2021, imekadiriwa kutumia jumla ya shilingi 12,402,962,303,000 kwa Mafungu yote saba. Kati ya fedha hizo shilingi 11,228,099,030,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na kwa ajili ya kulipia deni la Serikali la ndani na nje kiasi cha shilingi 8,649,941,441,000. Kiasi cha shilingi 510,045,950,000 kwa ajili ya mishahara na shilingi 664,820,323,000 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo inayotarajiwa kutekelezwa na Wizara katika kipindi husika.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa hesabu; kwa mwaka wa Fedha 2020/2021, imelenga kuimarisha ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali kwa lengo la kuimarisha, uwajibikaji na uwazi kwenye matumizi ya rasilimali za umma ambapo imepanga kutumia Sh.80,544,935,000 kwa kuzingatia vipaumbele na kazi za ofisi zilizolengwa kutekelezwa. Kati ya fedha hizo Sh.14,883,256,000 ni kwa ajili ya matumizi ya mishahara, Sh.53,993,739,000 ni matumizi mengineyo na Sh.11,667,940,000 ni jumla ya fedha za maendeleo za ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye maoni na mapendekezo ya Kamati ya Bajeti. Baada ya Kamati kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa Fedha 2019/2020 pamoja na mapato na matumizi ya Mafungu husika kwa mwaka wa Fedha 2020/2021, Kamati inapenda kutoa maoni na mapendekezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na usimamizi wa sera za kiuchumi katika kipindi cha janga la *Covid*-19 moja ya

jukumu kubwa la Wizara hii ni kuimarisha ukuaji wa uchumi jumuishi na endelevu kupitia sera bora za uchumi kwa maendeleo ya watu pamoja na ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Kamati inatoa ushauri kwa Wizara ya Fedha na Mipango kuanza kufikiria namna ya kupanga sera zake za kiuchumi katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu ili kusaidia kutatua matatizo ya kiuchumi yatakayojitokeza na gonjwa la *Covid*-19.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa *Covid-19* itaathiri mtu mmoja mmoja, kaya na biashara zote kwa ujumla na hivyo hali hii inaleta usumbufu wa utekelezaji wa shughuli za uchumi na pia itaathiri msingi wa maoteo ya mapato yaani *revenue forecast,* ulipaji na usimamizi wa kodi na mwenendo wa uchumi, hivyo kuna umuhimu wa Wizara kulazimika kufanya maamuzi muhimu ya sera kulingana na mazingira ya sasa kwa maendeleo ya watu pamoja na ukusanyaji wa mapato yetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kupitia Benki Kuu, imeanza kuchukua hatua za udhibiti wa sekta ya fedha na upatikanaji wa huduma za fedha kwa shughuli za kiuchumi. Hatua za kushusha kiwango cha *Statutory Minimum Reserve* kutoka asilimia saba hadi asilimia sita; kushusha kiwango cha riba ya kukopeshana kati ya mabenki na mabenki kutoka asilimia saba hadi tano; pamoja na kuongeza unafuu kwenye dhamana na hati fungani za Serikali. Ni matumaini ya Kamati kuwa hatua hizi pia zitaenda kuwanufaisha na kuwasaidia wakopaji wa kawaida, taasisi na makampuni binafsi watakaokopa. Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Benki Kuu kusimamia zoezi hili kwa mabenki ili lilete tija katika ukuaji wa uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Mfuko wa Majanga wa *IMF* na *World Bank;* itakumbukwa hivi karibuni Shirika la Fedha Duniani pamoja na Benki ya Dunia zimetoa ahueni ya kulipa madeni pamoja na Msaada kupitia Mfuko wa *CCRT* wa kukabiliana na majanga. Tumeshuhudia nchi jirani za Afrika mashariki, Magharibi na Kusini mwa Afrika zikipokea

fedha kwa ajili ya kupambana na janga la *corona* pamoja na kusaidia sekta mbalimbali kupambana na mdororo wa uchumi. Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kupata fedha hizo ili ziweze kusaidia kukabiliana na athari zinazotokana na janga la *Covid*-19. Uwezekano huo uangaliwe kwa kuzingatia faida na hasara za ahueni hiyo pamoja na kuzingatia Sheria ya Mikopo na Dhamana ya Serikali, Sura ya 137.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na matumizi ya Mfumo wa *TSA* kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi na Zanzibar; Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar bado haijaanza kutumia mfumo wa Akaunti Jumuifu ya Fedha kutokana na kuwa wakati mfumo huu unaanzishwa; Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa haijakidhi vigezo muhimu ikiwa ni pamoja na mifumo ya malipo ya kielektroniki. Aina ya mifumo hii ya malipo na mingine ndio ambayo ipo kieletroniki itawezesha Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupata mapato sahihi. Hivyo ni wajibu wa Serikali kulichukua suala hili kwa uzito wake ili kuhakikisha kuwa pande zote mbili za Muungano zinatumia mifumo inayosomana ikizingatiwa masuala ya kifedha ni ya kimuungano, lakini pia ili Akaunti ya Pamoja ya Fedha iweze kufanya kazi kwa ufanisi pindi itakapofunguliwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na deni la Taifa na huduma za Mfuko Mkuu Fungu 22; pamoja na kuhudumia deni la Taifa Fungu hili pia linatoa huduma nyingine za Mfuko Mkuu wa Serikali ikiwa ni pamoja na malipo ya pensheni; michango ya mwajiri; bima ya afya na mishahara ya viongozi na maafisa wa umma; na kiinua mgongo kwa baadhi ya viongozi. Matumizi hayo yanaongeza fedha kwa Fungu hili kuonekana kubwa na kwa tafsiri ya deni kuonesha malipo ya deni yanakuwa kwa kasi wakati nyingine ni stahili za viongozi na watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali, Fungu hili liwe ni maalum kwa ajili ya masuala yote ya madeni tu na hayo matumizi mengine yanaweza kuhamishiwa katika Idara na Taasisi za Serikali kama Utumishi, Mfuko wa Mahakama na Mafungu mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Soko la Bidhaa Tanzania; Kamati inatambua umuhimu wa kuanza kutumika rasmi kwa soko la bidhaa, lakini bado soko hili halijaweza kuwa na mifumo madhubuti itakayowezesha kufanya kazi kwa ufanisi. Mfumo unaoongelewa hapa, ni mfumo wa stakabadhi ghalani ambao sio mazao yote yana mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mfumo huu unataka kuwepo kwa miundombinu wezeshi kama, mfumo wa ununuzi (vyama vya ushirika) na maghala ya kutosha nchini yatakayoweza kukidhi mahitaji ya soko na kuongeza ufanisi wa mfumo wa stakabadhi za ghala. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha uwepo wa miundombinu hiyo wezeshi, kuwa na mfumo wa utoaji taarifa sahii za bei na masoko na usimamizi wa Soko lenyewe.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Mfumo wa Utathimini na Ufuatiliaji; moja ya jukumu la Wizara ya Fedha na Mipango ni pamoja na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala, Taasisi za Umma, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekta Binafsi. Aidha, bado kuna changamoto katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotokana na kutokufanyika kwa tathmini na utekelezaji wa miradi hii kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, miradi mingi ya maendeleo imekuwa na upungufu mkubwa, mingine kutokukamilika kabisa na mingine kutekelezwa miradi hewa. Hii ni dhahiri kuwa suala la *M&E* limekuwa halitekelezeki na hivyo kuipelekea nchi hasara kubwa. Hivyo, ni vema Serikali ikalichukulia suala hili kwa uzito wake na kuleta uwajibikaji katika Serikali na kuzingatia utaalam katika kusimamia miradi. Aidha, hatua hii iendane sambamba na uanzishwaji wa Sera ya Taifa ya Ufuatiliaji na Tathmini pamoja na ukamilikaji wa mfumo wa kitaifa wa ufuatiliji na tathmini ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Mfumo wa Kodi za Kielektroniki; moja ya mabadiliko makubwa yaliyofanywa na

Serikali ni kuanzisha mfumo wa Stempu za Kodi za Kieletroniki. Mfumo huu unasaidia kutambua bidhaa halisi na bidhaa ambazo hazina ubora katika soko.

Aidha, mfumo huu unaisaidia Mamlaka ya Mapato kukadiria Kodi Stahiki na mlaji kutambua kama bidhaa anayotumia ni halisi au la. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa mfumo huu kutumika katika bidhaa nyingine za viwandani ambazo zina mfumo unaowezesha stempu hizo kuwekwa ili kupata mapato sahihi kutoka bidhaa hizo. Aidha, mfumo huu unaweza kutumika katika utambuzi wa pembejeo ili kuwasaidia wakulima wetu ambao wamekuwa wakiathirika na uzalishaji, uingizaji na usambazaji wa pembejeo zisizo na ubora.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na uhakiki na ulipaji wa madeni ya watumishi, wakandarasi na wazabuni; katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020 Serikali ilikuwa imekwishalipa jumla ya shilingi 327….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mwenyekiti muda hauko upande wako, malizia.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI - MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, basi nihitimishe tu kwa kukushukuru sana wewe mwenyewe na Mheshimiwa Naibu Spika kwa uongozi wenu mnaotupa sisi kama Kamati. Pia niwashukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu wake, Katibu Mkuu na Manaibu Makatibu Wakuu niwashukuru sana. Niwashukuru sana wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao wanaonipa, lakini niwashukuru pia Sekretarieti wakiongozwa na Katibu wa Bunge letu Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

# MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21 KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2019/20, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/21 ambayo inajumuisha Mafungu Saba (7) ambayo ni Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina, Fungu 10 - Tume ya Pamoja ya Fedha, Fungu 13 - Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu, Fungu 21- Hazina, Fungu 22 - Deni la Taifa, Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali na Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango. Taarifa hii inajumuisha pia Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** moja ya jukumu la Kamati ya Bunge ya Bajeti kama yalivyoainishwa kwenye Nyongeza ya Nane kifungu cha 9 cha Kanuni za kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 ni pamoja na kusimamia shughuli za Wizara ya Fedha na Mipango na taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo. Aidha, kifungu cha 9 (1) (c) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 pia kinaipa Kamati ya Bajeti jukumu la kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu – 45, Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali. Kwa muktadha huo, katika nyakati tofauti, Kamati ilikutana na kufanya mashauriano na Serikali na hatimaye kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango na Mafungu yake yote Saba (7) pamoja na Fungu 45 - Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Fedha na Mipango ina jukumu la Kupanga Mipango ya Taifa na kusimamia utekelezaji Bajeti,

sera za mapato na matumizi ya umma pamoja na sera za fedha na uchumi kwa ujumla. Majukumu hayo yanatekelezwa kupitia mafungu yaliyo chini yake kama ifuatavyo: -

i. Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina: Ofisi ya Msajili wa Hazina imepewa jukumu la kusimamia na kulinda rasilimali zilizowekezwa na Serikali katika Mashirika na Taasisi za Umma pamoja na Kampuni ambazo Serikali ina hisa. Majukumu ya Ofisi ya msajili ni kama yalivyobainishwa kwenye Sheria ya Msajili wa Hazina Sura Na. 370.

ii. Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha: Tume ya Pamoja ya Fedha ni Taasisi ya Muungano wa Tanzania iliyoanzishwa kwa mujibu wa Ibara 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na baadae kuanzishwa kwa Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha ya mwaka 1996, Sura 140. Jukumu kuu la Tume ni kuwa chombo cha ushauri kuhusiana na mambo yote ya Muungano yanayohusu fedha baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na majukumu mengine kama yalivyoainishwa kwenye Ibara ya 134(2) ya Katiba.

iii. Fungu 13 – Kitengo cha kudhibiti Fedha Haramu: Kitengo hiki ni chombo cha kiinteligensia kilichoanzishwa chini ya Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu ya Mwaka 2006, Sura Na. 463 mahsusi kwa ajili ya kupambana na utakatishaji wa fedha haramu pamoja na ufadhili wa vitendo vya ugaidi nchini.

iv. Fungu 21- Hazina: Ofisi hii ina majukumu makuu matatu. Jukumu la **kwanza** ni kusimamia ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha za Serikali, **Pili** ni kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali na **Tatu** ni kusimamia Utekelezaji wa Sheria ya Mikopo na Dhamana ya Serikali Sura ya 137 ili kuhakikisha katika kipindi chote Deni la Serikali linaendelea kuwa himilivu.

v. Fungu 22 – Deni la Taifa: Idara hii inajukumu kubwa la kulipa madeni ya ndani na nje ya nchi (Principal debt) pamoja na

riba (Interest). Aidha Idara hii pia inajishughulisha na mafao ya pensheni kwa wastaafu pamoja na michango ya mwajiri.

vi. Fungu 23- Mhasibu Mkuu wa Serikali: Idara hii ina jukumu la kusimamia matumizi ya fedha za Serikali na kutoa miongozo ya mifumo ya kifedha inayopaswa kutumiwa na taasisi zote za umma.

vii. Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango: Fungu hili linajukumu la msingi la kusimamia uchumi jumla kupitia sera za fedha (Fiscal Policy) na matumizi na mifumo ya kifedha kwa ajili ya kuimarisha ukuaji wa uchumi (Monetary Policy).

## MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MAJUKUMU YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO PAMOJA NA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20

### Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha 2019/20, Wizara ya Fedha na Mipango iliidhinishiwa na Bunge kutumia jumla ya **shilingi 11,881,609,700,717** kwa mafungu yote saba (7) . Kati ya fedha hizo **Shilingi 11,157,327,758,988** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo yanajumuisha malipo ya Deni la Taifa (pamoja na riba) **shilingi 4,899,168,000,000** Deni la Ndani, **Shilingi 2,963,410,000,000** kwa ajili ya Deni la Nje na **Shilingi 724,281,941,731** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi, 2020 jumla ya **shilingi 7,648,561,448,989** zilikuwa zimetolewa kwa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na mafungu yake yote hii ikiwa ni sawa na **asilimia 64.37** ya Bajeti yote ya Wizara kwa kipindi husika. Kati ya fedha hizo **Shilingi 7,639,714,371,066** sawa na **asilimia 68.47** ya lengo zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 8,847,077,923** zilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na **asilimia 1.22** tu ya Bajeti ya maendeleo.

## Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Fungu 45

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipitia Bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ambapo kiasi cha **shilingi 62,142,554,000** zikihusisha fedha za maduhuli kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali kiliidhinishwa kwa matumizi ya Ofisi hii katika mwaka 2019/20. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 55,076,878,000** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, **shilingi bilioni 6,300,000,000** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo na **shilingi 765,676,000** ni fedha za makusanyo ya maduhuli.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi, 2020 lilikuwa limepokea kiasi cha **shilingi 46,431,843,915** sawa na **asilimia 75.65** Kati ya fedha hizo **shilingi 44,054,870,238** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 2,376,973,677** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ambayo ni sawa na **asilimia 38** ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Aidha, jumla ya **shilingi 768,941,292** sawa na **asilimia 100.4** za maduhuli zilikuwa zimekusanywa na Ofisi.
Aidha, **Jedwali Na. 1** hapo chini linaonyesha mgawanyo wa bajeti kwa kila fungu pamoja na utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha robo tatu ya mwaka wa fedha 2019/20.

### Jedwali Namba 1. Utekelezaji wa Bajeti Kwa Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2019/20

| FUNGU | JINA LA FUNGU | BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2019/20 | | FEDHA ILIYOTOLEWA HADI MACHI, 2020 | | ASILMIA YA FEDHA ZILIZOTOLEWA HADI APRILI, 2020 | | ASILIMIA KIASI CHOTE KILICHOTOLEWA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Matumizi ya kawaida | Maendeleo | Matumizi ya Kawaida | Maendeleo | Matumizi ya Kawaida | Maendeleo | (%) |
| 07 | Msajili wa Hazina | 40,510,802,000 | 2,300,000,000 | 9,778,470,300.67 | 450,934,700 | 24.1 | 19.6 | 23.9 |
| 10 | Tume ya Pamoia va Fedha | 2,207,935,000 | - | 1,648,993,077 | - | 75 | 0 | 75 |
| 13 | Kitengo Udhibiti Haramu | 2,015,586,000 | 200,295,998 | 1,128,552,377 | 173,054,011.50 | 56 | 86 | 58 |
| 21 | Hazina | 1,272,801,249,988 | 683,717,888,733 | 353,304,655,576.43 | 3,211,169,240.44 | 27.76 | 0.47 | 18.22 |
| 22 | Deni la Taifa | 9,730,012,708,000 | - | 7,204,020,041,449.15 | - | 74.04 | 0 | 74.4 |
| 23 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 44,066,048,000 | 3,300,000,000 | 21,833,018,743 | 722,930,000 | 49.55 | 21.91 | 47.62 |
| 50 | Wizara ya Fedha na Mipango | 65,713,430,000 | 34,763,757,000 | 48,000,639,543 | 4,288,989,971 | 73 | 12 | 52 |
| **JUMLA** | | **11,157,327,758,988** | **724,281,941,731** | **7,639,714,371,066** | **8,847,077,923** | **68.47** | **1.22** | **64.37** |
| 45 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | 55,076,878,000 | 6,300,000,000 | 44,054,870,238 | 2,376,973,677 | 80 | 38 | 76 |

**Jedwali Namba 2. Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo Kwa Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2019/ 20**

| FUNGU | JINA LA FUNGU | BAJETI YA MAENDELEO ILIYOIDHINISHWA 2019/20 | | FEDHA ILIYOTOLEWA HADI MACHI, 2020 | | ASILIMIA YA FEDHA ZILIZOTOLEWA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ndani | Nje | Ndani | Nje | Ndani | Nje |
| 07 | Msajili wa Hazina | 1,000,000,000 | 1,300,000,000 | 90,851,700 | 360,083,000 | 9.1 | 27.7 |
| 10 | Tume ya Pamoja | - | - | - | - | - | |
| 13 | Kitengo cha Udhibiti Fedha Haramu | - | 200,295,998 | - | 173,054,011.50 | 0 | 86 |
| 21 | Hazina | 656,000,000,000 | 27,717,888,733 | 137,005,000 | 3,074,164,240.44 | 0.02 | 11.09 |
| 22 | Deni la Taifa | - | - | | | | |
| 23 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 2,000,000,000 | 1,300,000,000 | - | 722,930,000 | 0 | 55.6 |
| 50 | Wizara ya Fedha na Mipango | 13,000,000,0000 | 21,763,757,000 | 2,196,828,476 | 2,092,161,495 | 17 | 10 |
| JUMLA | | 789,000,000,000 | 52,281,941,731 | 2,424,685,176 | 6,422,392,747 | 0.31 | 12.28 |
| 45 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu ya Serikali | 5,000,000,000 | 1,300,000,000 | 1,471,148,677 | 905,825,000 | 29.4 | 70 |

**Uchambuzi wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2019/20.**

**A: Uchambuzi wa Jumla.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti imefanya uchambuzi katika mafungu saba (7) yaliyo chini ya Wizara ya fedha na Mipango pamoja na **Fungu 45**- Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali. Kamati imebaini kuwa hadi kufikia mwezi Machi, 2020 :-

i. Mafungu **matatu 3** (**Fungu 10**- Tume ya Pamoja ya Fedha, **Fungu 22**- Deni la Taifa na **Fungu 50**- Wizara ya Fedha na Mipango) yalipokea zaidi ya **asilimia 60** ya fedha za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa na Bunge;

ii. Mafungu **mawili 2** (**Fungu 13** – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu na **Fungu 23** – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali) yalipokea zaidi ya **asilimia 50** ya bajeti nzima ya fedha za matumizi ya kawaida;

iii. Mafungu **mawili 2** (**Fungu 07** - Msajili wa Hazina na **Fungu 21**- Hazina) yalipokea chini ya **asilimia 30** ya fedha za matumizi ya kawaida; na

iv. Fungu **moja 1** (**Fungu 45**- Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ilipokea zaidi ya **asilimia 60** ya fedha za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa na Bunge.

Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo**,** kati ya mafungu saba (7)**, ni mafungu mawili tu** yamepokea zaidi ya **asilimia 50** (**Fungu 13** – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu na **Fungu 23** – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali. Aidha, **Fungu 45** Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ilipokea **asilimia 70** ya fedha za maendeleo. Mafungu mengine Matano yaliyobakia yalipokea fedha chini ya **asilimia 30**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa takwimu hizi, utaona kuwa kati ya jumla ya **Shilingi 724,281,941,731** zilizoidhishwa na Bunge kwa Wizara kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ni kiasi cha Shilingi **8,847,077,923 (**sawa na **asilimia 1.22)** ndiyo zimetolewa**.** Mwenendo huu sio wa kuridhisha ukizingatia kuwa miradi mingi ya maendeleo iliyochini ya Wizara ya Fedha na Mipango inahusu Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma, uboreshaji wa mifumo ya kiuhasibu kwa njia za mtandao, uboreshaji wa mifumo ya ununuzi, utawala bora, ukarabati na ujenzi wa makazi. Hivyo, ni dhahiri miradi hii imeathirika kwa kiwango kikubwa hasa ukizingatia kuwa Serikali imekuwa haitoi mchango wake wa fedha za ndani (*local component*) kwenye miradi hii. Aidha, Washirika wa Maendeleo nao wamepunguza kasi ya kutoa fedha (*foreign component*) kwenye miradi hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti inapenda kutoa ushauri kwa Wizara ya Fedha na Mipango kuwa, kwa sasa Dunia

nzima inajielekeza katika mapambano ya ugonjwa wa Covid-19, hivyo ni dhahiri misaada na mikopo ya masharti nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo itapungua.

**B: Uchambuzi wa Mafungu Mbalimbali.**

**Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2019/20, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **shilingi 42,810,802,000** hata hivyo hadi kufika mwezi Machi, 2020 kiasi cha **shilingi 10,229,405,00.67** ndicho kilikuwa kimetolewa na Hazina ikiwa ni sawa na asilimia **23.89** ya lengo.

**Mheshimiwa Spika,** utolewaji wa fedha kwa fungu hili umekuwa ni chini ya **asilimia 50** katika kipindi husika kwa miaka mitatu mfululizo**.** Mwenendo huu si wa kuridhisha hata kidogo na unaathiri matumizi maalum (special funds) ya urekebishaji wa mashirika ambayo ndiyo yanayochukua kiasi kikubwa cha bajeti ya fungu hili. Hata hivyo kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida kwa ajili ya ofisi hii zimekuwa zikiongezeka na majukumu yamekuwa yakiongezeka na yanahitaji ongezeko zaidi la fedha za matumizi ya kawaida. Hivyo, Serikali lazima izingatie umuhimu wa majukumu ya Ofisi ya Msajili wa Hazina katika kusimamia rasilimali za Serikali.

**Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha**

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Machi, 2020, Tume hii ilikuwa imepokea kiasi cha **shilingi 1,648,993,077** kati ya **shilingi 2,207,935,000** zilizoidhinishwa ikiwa ni sawa na **asilimia 74.68** ya bajeti yote ukiwa ni mwenendo mzuri wa utolewaji fedha kwa fungu hili.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa suala hili ni la muda mrefu, Kamati bado inaendelea kusisitiza juu ya ukamilishaji wa haraka wa mchakato wa ufunguaji wa Akaunti ya Fedha ya Pamoja (AFP) hasa ikizingatiwa kuwa tayari Muundo mpya ambao unaendana sambamba na majukumu ya Tume

ulishapitishwa na mamlaka husika ya Serikali tangia mwezi Oktoba, 2018.

**Fungu 13 – Kitengo cha kudhibiti Fedha Haramu**

**Mheshimiwa Spika,** hadi mwezi Machi, 2020 Kitengo kilikuwa kimepokea kiasi cha **shilingi 1,128,552,377** fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwa ni sawa na **asilimia 56.** Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, Kitengo kiliidhinishiwa kutumia kiasi cha **shilingi 200,295,998 na** hadi kufikia mwezi Machi, 2020 kiasi cha **shilingi 173,054,011.50** kilikuwa kimepokelewa sawa na **asilimia 86** ya makadirio.

**Mheshimiwa Spika,** fedha hizi za maendeleo kwa fungu hili ni za nje, hivyo utekelezaji wake unategemea kwa kiasi kikubwa cha fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo. Kamati inaishauri Serikali, kuanza kufikiria kutenga fedha za ndani kwa ajili ya uendeshaji wa Kitengo cha kudhibiti Fedha Haramu ili kiweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo pasipo kutegemea fedha za wahisani hasa katika kipindi hiki cha janga la Corona.

**Fungu 21- Hazina**

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi, 2020 Idara hii ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi 356,515,824,816.87** sawa na **asilimia 18.22** ya bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge ya **shilingi 1,956,519,138,721**. Kwa upande wa fedha za maendeleo, Fungu hili limepokea kiasi cha **shilingi 3,211,169,240.44** kati ya **shilingi 683,717,888,733** sawa na **asilimia 0.47** ya fedha zote za maendeleo. Hali hii ni tofauti na ilivyokuwa kwa mwaka 2018/19 ambapo ilipokea kiasi cha **asilimia 85.2** ya fedha zote za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua kuwa mradi mkubwa wa maendeleo katika fungu hili ni ule unahusisha maboresho ya fedha za umma (PFMRP) ambao fedha zake nyingi zinatoka kwa wahisani. Hivyo imefikia wakati kwa Serikali kuanza kufikiri upatikanaji wa fedha za kutosha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu, ukizingatia kuwa Idara hii

ina umuhimu mkubwa katika kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali, sera, kanuni; kusimamia ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha za Serikali; kufuatilia utekelezaji wa mipango ya maendeleo na mikakati ya kupunguza umaskini; kusimamia na kudhibiti Deni la Taifa.

**Fungu 22 – Deni la Taifa na Huduma Nyingine**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2019/20 Fungu 22 liliidhinishiwa kutumia kiasi cha shilingi **9,730,012,708,000.** Hadi kufikia mwezi Aprili, 2020 Fungu hili lilikuwa limepokea jumla ya **shilingi 7,204,020,041,449.15** ikiwa ni sawa na **asilimia 74.04** ya lengo. Kati ya fedha hizo, kiasi kilichotolewa kwa ajili ya kugharamia deni la ndani ni kiasi cha **shilingi 4,065,575,125,236.03** na deni la nje **shilingi 2,133,409,895,072.93** zote zikiwa sawa na **asilimia 86.05** ya fedha zote zilizotolewa. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha hizi ambazo pia zinasaidia kulipa mafao na pensheni kwa wastaafu wa Serikali wanaolipiwa Hazina pamoja na kulipa mirathi kwa warithi na malipo ya kiinua mgongo kwa watumishi wa Serikali walio kwenye mikataba

**Fungu 23- Mhasibu Mkuu wa Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali katika mwaka wa fedha 2019/20 iliidhinishiwa kutumia kiasi cha **shilingi 47,366,048,000**. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 Idara ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi 22,555,948,743** ikiwa ni sawa na **asilimia 47.62**. Kati ya fedha hizo **shilingi 17,470,446,734** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **shilingi 4,362,572,009** kwa ajili ya mishahara na **shilingi 722,930,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa Idara. Kamati inasisitiza Idara hii kuendelea kusimamia ipasavyo majukumu yake hasa yale yanayohusu usimamizi wa Sera za Serikali zinazohusu ubora na usalama wa fedha na mali za serikali pamoja na usimamizi wa utekelzaji wa Sheria ya fedha ya Mwaka 2001 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2004).

**Fungu 50 -Wizara ya Fedha na Mipango**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20 Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango liliidhinishiwa jumla ya **shilingi 100.477,187,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na

miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 Wizara ilikua imepokea jumla ya **shilingi 52,289,629,514** sawa na **asilimia 52.04** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo **shilingi 21,775,523,600** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **shilingi 26,225,115,943.01** kwa ajili ya mishahara na **shilingi 4,288,989,971** kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa Idara na Taasisi zilizo chini ya fungu hili. Hatua hii imewezesha Kuratibu na kusimamia shughuli za Bunge, Mipango na Bajeti ya Wizara pamoja na Kusimamia na kuratibu shughuli za taasisi na mashirika yaliyo chini ya Wizara.

**Uchambuzi wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/20.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kufanya mashauriano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu hili.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ni taasisi yenye jukumu la kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali, kama yalivyoidhinishwa na Bunge. Kwa mujibu wa Hati ya Majukumu ya mwaka 2018, Ofisi imepewa majukumu yafuatayo:

(i) Kukagua hesabu za Wizara, Mikoa, Halmshauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji, Ofisi za Balozi za Tanzania zilizoko nje ya nchi, Wakala za Serikali, Mashirika ya Umma, pamoja na Miradi ya Maendeleo inayogharamiwa na wafadhili na kutoa taarifa ya ukaguzi huo Bungeni juu ya mapato na matumizi ya fedha za Umma;

(ii) Kujenga, kukuza na kuimarisha utamaduni wa uwajibikaji katika Wizara na Taasisi za Serikali, Mikoa na Halmshauri;

(iii) Kuhakikisha kwamba, inajiridhisha kuwa upo uwajibikaji wa kutosha katika kusimamia na kudhibiti ipasayo ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali; na

(iv) Kuhakikisha kuwa jamii ya Tanzania inapata faida au tija kutokana na matumizi bora ya fedha za Umma, na mali za Umma zinahifadhiwa, kutunzwa na kulindwa ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/20 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali iliidhinishiwa jumla ya kiasi cha **Shilingi 61,376,878,000** kutoka Mfuko Mkuu kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo mishahara ni **Shilingi 14,084,139,000** matumizi mengineyo (OC) **Shilingi 40,992,739,000** na **Shilingi 6,300,000,000** zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo fedha za ndani zilikuwa **shilingi 5,000,000,000** na **shilingi 1,300,000,000** ni fedha za nje. Kwa upande wa maduhuli, Ofisi ilikadiriwa kukusanya kiasi cha **shilingi 765,676,000.** Maduhuli ya Ofisi hii yanatokana na marejesho ya gharama za ukaguzi (reimbursable costs) wa Mashirika ya Umma, ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayosimamiwa na Wizara chini ya Divisheni ya Serikali Kuu pamoja na ile ya miradi chini ya Divisheni ya Hesabu za Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Bajeti hiyo hadi kufikia mwezi Machi, 2019 Ofisi ilikuwa imepokea jumla ya kiasi cha **shilingi 46,431,843,915** kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali. Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 75.65**. Kati ya kiasi hicho, **shilingi 9,024,969,571** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 32,161,747,099** ni kwa Matumizi ya mengineyo na shilingi **shilingi 2,060,123,677** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo**.**

**Mheshimiwa Spika,** kiasi hicho cha bajeti kilichotolewa kimeiwezesha Ofisi kutekeleza shughuli mbalimbali zilizokuwa zimepangwa kulingana na fedha zilizopokelewa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na makusanyo ya ndani. Aidha, mwenendo wa utolewaji wa fedha kutoka Mfuko Mkuu kwa Ofisi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo umebaki kuwa wa changamoto ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2019 kiasi kilichokuwa kimepokelewa ni **asilimia 38** tu ya makadirio. Hivyo ni vema Serikali ikaangalia namna ya kuongeza bajeti ya maendeleo katika Ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya tathmini ya mwenendo wa sura ya bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi za Hesabu za Serikali iliyokuwa inatengewa na Serikali kwa kipindi cha

miaka 4 kuanzia 2017/18 hadi 2020/21. Bajeti ya Fungu 45 ilianza kushuka katika mwaka 2017/18 hadi 2019/20 ikilinganishwa na bajeti inayoombewa mwaka 2020/21. Aidha, mwaka 2020/21 bajeti ya NAOT imeongezeka kwa **asilimia 31.** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza bajeti ya ofisi hii muhimu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla bajeti ya mwaka 2020/21 imeongezeka kwa jumla ya **shilingi 19,168,057,373** ukilinganisha na ile ya mwaka 2019/20. Kati ya kiasi kilichoongezeka fedha za matumizi mengineyo zimeongezeka kwa **shilingi 13,001,000,373** na matumizi ya maendeleo yameongezeka kwa **shilingi 5,367,940,000**. Aidha, ongezeko hili limepelekea pia kuongezeka kwa mawanda ya ukaguzi ambazo awali yalikuwa hayafanyiki kutokana na ukosefu wa fedha pamoja na mambo mengine.

**Mheshimiwa Spika**, ongezeko la bajeti ya NAOT ni kiashiria kizuri kwa upande wa uhuru wa Ofisi ya CAG kwa kuzingatia vigezo vya kimataifa. Aidha, bado Ofisi ya CAG ina changamoto ya kutokuwa na kibali cha kuajiri watumishi wake mwenyewe. Hali ilivyo watumishi wa Ofisi hii wanajiriwa kupitia Ofisi ya Utumishi ambavyo ni kinyume na vigezo vya uhuru wa CAG vilivyowekwa kimataifa. Hivyo, ni ushauri wa Kamati kuwa Serikali izingatie Sheria na majukumu ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, ungezeko la fedha hizi zitasaidia kutatua baadhi ya changamoto zifuatazo:-

i. Kuongeza mawanda ya ukaguzi na kufikia maeneo ambayo Ofisi inaona yana viashiria vya mwenendo wenye shaka katika mapato na matumizi ya fedha za Serikali;

ii. Kukagua miradi mikubwa ya Maendeleo ya Kimkakati inayotekelezwa na Serikali yenye mahitaji makubwa ya kibajeti ya ukaguzi wa maeneo hayo. Hii ni pamoja na hitaji l kufanya ukaguzi wa kiufundi na thamani ya fedha katika miradi hiyo ili kujiridhisha kuwa Serikali inapata matokeo tarajiwa;

iii. Kufanya ukaguzi unaohitajika kwa kiwango cha kimataifa kwenye mifumo ya TEHAMA ya Serikali inayohusika na ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali;

iv. Kuongeza ukaguzi kwenye mahitaji maalum ya ukaguzi katika ngazi ya Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma, Bunge na Mahakama; na

v. Kununua vitendea kazi muhimu pamoja na ukarabati wa majengo ya ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (NAOT).

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO PAMOJA NA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21.**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mafungu 7 ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2020/21.**

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2020/21 imekadiriwa kutumia jumla ya **Shilingi 12,402,962,303,000** kwa mafungu yote Saba (7). Kati ya fedha hizo, **Shilingi 11,228,096,030,000** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo (OC) na kwa ajili ya kulipia Deni la Serikali (ndani na nje) kiasi cha **shilingi 8,649,941,441,000, shilingi 510,045,950,000** ajili ya mishahara na **Shilingi 664,820,323,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo inayotarajiwa kutekelezwa na Wizara katika kipindi husika.

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali (NAOT) kwa Mwaka wa Fedha 2020/21.**

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi kwa mwaka wa fedha 2020/21 imelenga kuimarisha ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji na uwazi kwenye matumizi ya rasilimali za umma ambapo imepanga kutumia **shilingi 80,544,935,000** kwa kuzingatia vipaumbele na kazi za Ofisi zilizolengwa kutekelezwa. Kati ya fedha hizo, **shilingi**

**14,883,256,000** ni kwa ajili ya matumizi ya mishahara; **shilingi 53,993,739,000** matumizi mengineyo na **shilingi 11,667,940,000** ni jumla ya fedha za maendeleo za ndani na nje.

**Mheshimiwa Spika,** kama tulivyosema hapo awali kuwa bajeti hii imeongezeka kwa asilimia 31 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2019/20. Aidha, fedha hizo zinajumuisha nyongeza ya fedha ya **shilingi 14,800,00,000** kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kati ya **shilingi 20,000,000,000** zilizokuwa zimeombwa nje ya ukomo wa bajeti. Ni matumaini ya Kamati kuwa Fungu 45 litaendelea kupatitiwa fedha kulingana na mahitaji yake ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kikatiba.

**Jedwali Namba 4. Maombi ya Fedha Kwa Wizara ya Fedha na Mipango na Mafungu yaliyo Chini Wizara Pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka 2020/21.**

| FUNGU | MATUMIZI MENGINEYO (OC) | MISHAHARA | MIRADI YA MAENDELEO | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 07 | 22,229,786,000 | 3,375,080,000 | 2,300,000,000 | 27,904,866,000 |
| 10 | 2,048,142,000 | 802,823,000 | - | 2,850,965,000 |
| 13 | 2,915,586,000 | - | 500,000,000 | 3,415,586,000 |
| 21 | 637,275,862,000 | 450,901,950,000 | 641,000,892,000 | 1,729,178,704,000 |
| 22 | 10,477,797,406,000 | 9,989,416,000 | - | 10,487,786,822,000 |
| 23 | 58,036,734,000 | 5,738,683,000 | 3,500,000,000 | 67,275,417,000 |
| 50 | 27,792,514,000 | 39,237,998,000 | 12,016,431,000 | 79,046,943,000 |
| **JUMLA** | **11,228,096,030,000** | **510,045,950,000** | **664,820,323,000** | **12,402,962,303,000** |
| 45 | 53,993,739,000 | 14,883,256,000 | 11,667,940,000 | 80,544,935,000 |
| **JUMLA KUU** | **11,282,089,769,000** | **524,929,206,000** | **676,488,263,000** | **12,483,507,238,000** |

## MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya

Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/20 pamoja na mapato na matumizi ya mafungu husika kwa mwaka wa fedha 2020/21; Kamati inapenda kutoa **maoni na mapendekezo** yake kama ifuatavyo: -

**Usimamizi wa Sera za kiuchumi (Fiscal policy) na Fedha (Monetary policy) katika kipindi cha janga la COVID -19**

**Mheshimiwa Spika**, moja ya jukumu kubwa la Wizara ya Fedha na Mipango ni Kuimarisha ukuaji wa uchumi jumuishi na endelevu kupitia sera bora za uchumi kwa maendeleo ya watu pamoja na ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Kamati inatoa ushauri kwa Wizara ya Fedha na Mipango kuanza kufikiria namna ya kupanga sera zake za kiuchumi katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu ili kusaidia kutatua matatizo ya kiuchumi yatokanayo na COVID -19.

**Mheshimiwa Spika,** ni dhahiri kuwa COVID -19 imeathiri mtu mmoja mmoja, kaya na biashara zote kwa ujumla na hivyo hali hii inaleta usumbufu wa utekelezaji shughuli za uchumi na pia imeathiri msingi wa maoteo ya mapato (*revenue forecasting*), ulipaji na usimamizi wa kodi na mwenendo wa uchumi. Hivyo kuna umuhimu wa Wizara hii kulazimika kufanya maamuzi muhimu ya sera kulingana na mazingira ya sasa kwa maendeleo ya watu pamoja na ukusanyaji wa mapato.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, Kamati inaipongeza Serikali kupitia Benki Kuu, imeanza kuchukua hatua za udhibiti wa sekta ya fedha na upatikanaji wa huduma ya fedha katika shughuli za kiuchumi. Hatua za kushusha kiwango cha *Statutory Minimum Reserve* - SMR kutoka asilimia 7 hadi asilimia 6, kushusha kiwango cha riba ya kukopeshana kati ya mabenki na mabenki kutoka asilimia 7 hadi 5 pamoja nakuongeza unafuu kwenye dhamana na hati fungani za serikali. Ni matumaini ya Kamati kuwa hatua hizi pia zitaenda kuwanufaisha na kuwasiaidi wakopaji wa kawaida, taasisi na makampuni binafsi watakaokopa. Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Benki Kuu kusimamia zoezi hili kwa mabenki ili lilete tija katika ukuaji wa uchumi.

**Mfuko wa Majanga wa IMF na World Bank (*Catastrophic Containment Relief Fund*-CCRT)**

**Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa hivi karibuni Shirika la Fedha Duniani (IMF) pamoja na Benki ya Dunia zimetoa ahueni ya kulipa madeni pamoja na Msaada kupitia Mfuko wa CCRT wa kukabiliana na Majanga. Tumeshuhudia nchi jirani za Afrika mashariki, Magharibi na Kusini mwa Afrika zikipokea fedha kwa ajili ya kupambana na janga la corona pamoja na kusaidia sekta mbalimbali kupambana na mdororo wa uchumi. Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kupata fedha hizo ili ziweze kusaidia kukabiliana na athari zinazotokana na janga la COVID-19. Uwezekano huo uangaliwe kwa kuzingatia faida na hasara za ahueni hiyo pamoja na kuzingatia Sheria ya Mikopo na Dhamana ya Serikali Sura ya 137.

**Ofisi ya Msajili wa Hazina**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na bajeti ya Fungu 7 kushuka kwa **asilimia 34.8** kwa mwaka wa fedha 2020/21, fungu hilo limeongezewa majukumu ya kusimamia Viwanda na Mashamba yaliyobinafsishwa na yaliyorejeshwa Serikalini ambapo kimsingi imeiongezea Ofisi gharama kwa ajili ya kuvitunza viwanda na mashamba hayo. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kuwa Ofisi hii inapatiwa fedha za kutosha ili kukabiliana na majukumu iliyoongezewa. Vilevile, Kamati inashauri Serikali kuja na mkakati wa haraka wa kuendeleza mashamba, viwanda na mali zilizoreshejwa Serikalini ili kuipunguzia Serikali mzigo wa gharama wa kutunza rasilimali hizo.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hayo, Kamati inasisitiza kuwa Serikali itekeleze yafuatayo: **kwanza**, kuwekeza katika yale mashirika ambayo ina umiliki mdogo (*minority shareholding*); **pili**, inapata *return* ya uwekezaji uliofanywa kwenye Mashirika hayo; na **tatu**, Serikali iangalie njia mbadala ya upatikanaji wa mitaji kwa mashirika yenye uhitaji mathalani kupitia Soko la Hisa (DSE) na sio kutegemea fedha kutoka Serikali Kuu.

**Matumizi ya Mfumo wa TSA kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar – SMZ**

**Mheshimwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar bado haijaanza kutumia mfumo wa Akaunti Jumuifu ya Fedha (TSA) kutokana na kuwa pindi mfumo huu wakati unaanzishwa; SMZ ilikuwa haijakidhi vigenzo muhimu ikiwa pamoja na mifumo ya malipo ya kielektroniki. Aina ya mifumo hii ya malipo na mingine ndio ambayo ipo kieletroniki itawezesha SMZ kupata mapato sahihi. Hivyo ni wajibu wa Serikali kuchukua suala hili kwa uzito wake ili kuhakikisha kuwa pande zote mbili za Muungano zinatumia mifumo inayosomana ikizingatiwa masuala ya kifedha ni ya kimuungano lakini pia ili Akaunti ya Pamoja ya Fedha iweze kufanya kazi kwa ufanisi pindi itakapofunguliwa.

**Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu**

**Mheshimiwa Spika,** kuna haja ya kitengo kuangalia upya majukumu yake kwa sababu yanaonyesha jukumu lao kubwa ni kupoakea na kuchambua Taarifa kwa maana nyingine wanakuwa *reactive* kuliko *proactive*. Ina maana kunapotokea watoa Taarifa hawajaleta Taarifa kitengo kitakuwa na kazi chache za kufanya. Ni vyema Kitengo hiki ikawa na mifumo ya mawasiliano itakayohakikisha upatikananji wa taarifa na takwimu sahihi za miamala ya malipo ili kubaini maeneo yenye viashiria vya utakatishaji wa fedha.

**Deni la Taifa na Huduma za Mfuko Mkuu**

**Mheshimiwa Spika,** Fungu 22 pamoja na kuhudumia deni la Taifa pia linatoa huduma nyingine za Mfuko Mkuu wa Serikali ikiwa ni pamoja na malipo ya pensheni, michango ya mwajiri, bima ya afya na mishahara ya viongozi na maafisa wa umma na kiinua mgongo kwa baadhi ya viongozi. Matumizi hayo yanaongeza fedha kwa Fungu hili kuonekana kubwa na kwa Tafsiri ya Deni kuonesha malipo ya Deni yanakuwa kwa kasi wakati nyingine ni stahili za Viongozi na Watumishi wa Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Serikali, Fungu hili liwe ni maalumu kwa ajili ya masuala yote ya madeni tu na hayo matumizi mengine yanaweza kuhamishiwa katika Idara na Taasisi za Serikali kama Utumishi, Mfuko wa Mahakama na mafungu mengine. Hatua hii ni ya busara kwa kuwa itaipa uzito wa kipekee fedha zinazotengwa kwa ajili ya kugharamia Deni la Taifa.

**Soko la Bidhaa Tanzania – TMX**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua umuhimu wa kuanza kutumika rasmi kwa soko la bidhaa – TMX lakini bado soko hili halijaweza kuwa na mifumo madhubuti itakayowezesha TMX kufanya kazi kwa ufanisi. Mfumo unaongelewa hapa, ni mfumo wa stakabadhi ghalani ambao sio mazao yote yana mfumo huu. Hata hivyo, mfumo huu unataka kuwepo kwa miundombinu wezeshi kama, mfumo wa ununuzi (vyama vya ushirika) na maghala ya kutosha nchini yatakayoweza kukidhi mahitaji ya soko na kuongeza ufanisi wa Mfumo wa stakabadhi za ghala.

**Mheshimiiwa Spika,** Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha uwepo wa miundombinu hiyo wezeshi, kuwa na mfumo wa utoaji taarifa sahii za bei na masoko na usimamizi wa Soko lenyewe.

**Mfumo wa Tathmini na Ufuatiliaji (M&E)**

**Mheshimiwa Spika,** moja ya jukumu la Wizara ya Fedha na Mipango ni pamoja na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala, Taasisi za Umma, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekta Binafsi. Aidha, bado kuna changamoto katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotokana na kutokufanyika kwa tathmini na utekelezaji wa miradi hii kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, miradi mingi ya maendeleo imekuwa na mapungufu makubwa, mingine kutokukamilika kabisa na mengine kutekelezwa miradi hewa. Hii ni dhahiri kuwa suala

la M&E limekuwa halitekelezeki na hivyo kuipelekea nchi hasara kubwa. Hivyo, ni vema Serikali ikalichukulia suala hili kwa uzito wake na kuleta uwajibikaji katika Serikali na kuzingatia utaalamu katika kusimamia miradi. Aidha, hatua hii iendane sambamba na uanzishwaji wa Sera ya Taifa ya Ufuatiliaji na Tathmini pamoja na ukamilikaji wa mfumo wa kitaifa wa ufuatiliji na tathmini ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile maboresho haya yaende sambamba na uwepo wa uhuru wa wakaguzi wa ndani wa Serikali Kuu, Halmashauri na Mamlaka za Serikali za Mitaa tofauti na ilivyo hivi sasa.

**Mifumo ya TEHAMA**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na juhudi nzuri zinazofanywa na Wizara katika ubunifu wa mifumo mbali mbali ya TEHAMA, kumekuwa na uanzishwaji wa mifumo mingi nchini na hivyo kupelekea kuwepo na utitiri wa mifumo ambayo mingine inafanya kazi zinazoshabihiana. Ni ushauri wa Kamati kuwa, Serikali iwe na mfumo mmoja na kuanzisha *modules* badala ya mifumo mipya ili kushughulikia masuala mapya pamoja na kuihisha mifumo iliyopo ili isomane.

**Mfumo wa Kodi za Kieletroniki *(Electronic Tax Stamp)***

**Mheshimiwa Spika,** moja ya mabadiliko makubwa yaliyofanywa na Serikali ni kuanzisha mfumo wa Stempu za Kodi za Kieletroniki. Mfumo huu unasaidia kutambua bidhaa halisi (*Genuine*) na bidhaa ambazo hazina ubora katika soko. Aidha, mfumo huu unaisaidia mamlaka ya Mapato kukadiria Kodi Stahiki na mlaji kutambua kama bidhaa anayotumia ni halisi ama la. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa mfumo huo kutumika katika bidhaa nyingine za viwandani ambazo zinamfumo unaowezesha stempu hizo kuwekwa ili kupata mapato sahihi kutoka bidhaa hizo. Aidha, mfumo huo unaweza kutumika katika utambuzi wa pembejeo ili kuwasaidia wakulima wetu ambao wamekuwa wakiathirika na uzalishaji, uingizaji na usambazaji wa pembejeo zisizo na ubora.

**Uhakiki na Ulipaji wa Madeni ya Watumishi, Wakandarasi na Wazabuni.**

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020 Serikali ilikuwa imekwisha kulipa jumla ya **shilingi 327,804,805,268.56** kwa ajili ya madeni ya Wakandarasi, Wazabuni na Watoa Huduma yaliyohakikiwa. Kati ya fedha hizo Wakandarasi walilipwa **shilingi 14,667,577,422.21**, Watumishi **shilingi 60,717,890,332.16,** Wazabuni **shilingi 147,731,394,644.53**, Watoa Huduma **shilingi 15,813,720,395.85** na madeni mengineyo kama vile fidia na michango ya kimataifa **shilingi 88,874,222,203.81**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada za kuendelea kuhakiki na kulipa madeni hayo. Hata hivyo, kwa kuwa suala hili ni la muda mrefu na madeni mapya yanaendelea kuzalishwa, Kamati inaendelea kuisistizia Serikali inahakikisha inaendelea na ulipaji wa madeni yote yaliyohakikiwa ili kupunguza gharama kwa Serikali hasa kwa madeni yenye ongezeko la riba lakini pia gharama kwa watoa huduma waliokopa kwenye mabenki kupata mtaji ili waweze kutoa huduma kwa Serikali. Suala hili la ulipaji wa madeni ni muhimu hasa katika kipindi hiki cha ugonjwa wa Covid-19. Hatua hii itasaidia kuongeza ukwasi kwenye uchumi ili kusaidia biashara zisife na kupunguza mikopo chechefu katika mabenki ya ndani ambayo Wafanyabiashara wengi wa ndani walikopa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwepo na changamoto ya hati za madai za wakandarasi kutoka wizara na taasisi nyingine zinazowasilishwa Hazina kwa ajili ya malipo. Hati hizo zimeonekana kuwa na upungufu na suala hili limekuwa linajirudia mara kjwa mara na hivyo kupelekea kuchelewa kwa malipo hayo. Kamati inaitaka Serikali kurejea Waraka Na 1 kuhusu Utekelezaji wa Bajeti na Waraka namba 3 kuhusu uhakiki na ulipaji wa madeni wa mwaka 2019 ambao unatoa muongozo kwa Maafisa masuuli wa namna ya kufanya manunuzi na kuwasilisha nyaraka mbalimbali za madeni ili ziweze kuhakikiwa na kulipwa. Hali ilivyo hivi sasa Nyaraka

hizo zinajulikana na kutumika zaidi na Wizara ya Fedha peke yake kuliko maafisa masuuli wa wiazra na taasisi nyingine.

**HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mhe. Spika, Dkt. Tulia Akson, Mb - Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa miongozo yenu ambayo mmekuwa mkitupatia. Shukrani pia ziwaendee Mhe. Dkt Philip Mpango (Mb) Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt Ashatu K. Kijaji (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu pamoja na wataalamu wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao mkubwa waliotupa wakati wote wa kujadili utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha, Kamati inatoa shukrani kwa Wakuu wa Taasisi na Idara zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano na ufafanuzi walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kuchambua bajeti ya Wizara hii na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Aidha, naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati kwa majina yao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb – M/Mwenyekiti
2. Mhe. David Ernest Silinde, Mb
3. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
4. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
5. Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
6. Mhe. Dkt. Immaculate Swale Semesi, Mb
7. Mhe. Ali Hassan Omar, Mb
8. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
9. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
10. Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
11. Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mb
12. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb

13. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb
14. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb
15. Mhe. Hasna Sadi Katunda Mwilima, Mb
16. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb
17. Mhe. Abdallah Majurah Bulembo, Mb
18. Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb
19. Mhe. Stephen Julius Masele, Mb
20. Mhe. Marwa Ryoba Chacha, Mb
21. Mhe. Dkt. Balozi Diodorus Buberwa Kamala, Mb
22. Mhe. Joseph George Kakunda, Mb
23. Mhe. John Kibera Kishimba, Mb
24. Mhe. Andrew John Chenge, Mb
25. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb
26. Mhe. Suleiman Ahmed Saddiq, Mb
27. Mhe. Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mb

**Mheshimiwa Spika,** mwisho naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Mkururgenzi wa Bajeti Ndugu Michael Kadebe kwa kuratibu shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na mafungu manane (8) yaliyo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mashimba M. Ndaki, Mb
**M/MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**

15 Mei, 2020

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti, Mheshimiwa Mashimba tunakushukuru sana kwa maoni hayo ya kamati ya Bajeti na kwa kazi kubwa ambayo Kamati hii inafanya kwa niaba yetu Waheshimiwa Wabunge wote, ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaenda kwenye uchangiaji ataanza Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba na atafuatia na Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Wizara hii ya Fedha. Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kukupongeza wewe mwenyewe kwa kuliongoza Bunge hili kwa viwango vya juu kabisa. Mheshimiwa Naibu Spika ameendelea kutusaidia vizuri, mmefanya kazi nzuri sana. Sasa nina miaka 10 ndani ya Bunge hili nimeshuhudia viwango vikiongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, tangu tumempa nchi hii katika miaka mitano viwango vyake havilinganishwi na Rais yoyote, viwango vyake vimejipambanua vyenyewe akili na uwezo wa Baraza lake la Mawaziri wanashauriana vizuri. Kwa hiyo kwa kweli tukiwa na Mheshimiwa Waziri wetu Mkuu Majaliwa Majaliwa na Mama yetu wanafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana kaka yangu Mheshimiwa Mpango, kaka yangu amefanya kazi nzuri sana kwenye Wizara hii na mama yetu Mheshimiwa Kijazi amefanya kazi nzuri sana katika kuendesha uchumi wetu wa nchi. Nilikuwa najiuliza hii miradi yote ambayo Mheshimiwa Rais ameamua tuitekeleze fedha tutatoa wapi na nidhamu ya kutumia itakuwaje? Naomba niseme, uliniteua kuwa kwenye Kamati ya Bajeti na nimeshuhudia kwamba kwa kweli Wizara ya Fedha inafanya kazi kubwa sana, tuipigie makofi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wako wataalam wao Makatibu Wakuu, wanaye Gavana pale wa Benki Kuu, wanaye *CAG,*

ni vyombo vyake vinavyomsaidia kwa kweli naomba nimpongeze sana kwa kazi nzuri sana. Naomba niipongeze Wizara na Serikali kwa ujumla, mwaka 2015 Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli alikuja pale Buhigwe akahidi tukawa wote kwenye jukwaa, naomba popote alipo ajue kwamba ahadi zake zote katika Wilaya ya Buhigwe amemaliza. Aje tu apite anasalimia wananchi, anawapa *mwakeye, mwidiwe* tumpe kura aweze kuondoka. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, niipongeze Wizara, juzi tu wananchi wangu wa Manyovu walikuwa wanapewa fidia kwa kujenga barabara ile ya Manyovu kwenda Kasulu kwenda Nyakanazi. Kwa hiyo ni jambo ambalo wananchi wangu wamesema niishukuru Serikali kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya. Sasa wananchi wa Buhigwe wataanza kuona lami na wao kama watu wengine. Pia niendelee kuishukuru Wizara ya Fedha na Serikali yake kuendelea kutushika mkono kwenye ile soko letu la mkakati ambalo linaenda vizuri sana. Kwa hiyo nawapongeza sana, wanafanya kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo mambo ambayo nafikiri inabidi yasaidie, Mheshimiwa Waziri pale kwenye Wizara ya Fedha ana kitengo cha *PPP* na amesema vizuri, hiki kitengo hawajakiwezesha kiasi kwamba kiweze kusadia uchumi wa nchi hii. Hatuwezi kuendelea hivi kwamba miradi yote ifanywe na hela anazozikusanya Mheshimiwa Waziri, lazima kuna watu wana mitaji pembeni, kuna miradi hiyo, sasa ifike mahali kitumike. Wanakitumia lakini hawawezi kukipa uwezo na wakaamua tukaweka miradi, sasa ni muhimu miradi hii iweze kuonekana kabisa kwamba huu ni mradi wa *PPP* na ume-*save* hela za Serikali kiasi hiki. Kwa hiyo kitengo hiki nafikiri ni vizuri wakiimarishe hakijajitokeza rasmi ingawa anakitoa vizuri kwenye hotuba lakini hakijajitokeza kuleta mchango wowote katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, miradi ya maendeleo; nimekuwa Mjumbe kwenye Kamati ya Bajeti, Wizara hizi wanapanga miradi ya maendeleo, tukienda kuangalia tunakuta saa nyingine fedha hazijatoka kuna *knowledge gape* kati ya

Wizara ya Fedha na Taasisi au Wizara hizi nyingine. Wizara ya Fedha ikishakupa bajeti yako ya maendeleo inataka uanzishe mchakato wa manunuzi na kuanza huo mradi halafu ulete *certificate* kwenye Wizara ya Fedha iweze kulipwa. Sasa Wizara nyingi zimejikuta zinasubiri zipelekewe fedha kwenye kasma zao, ndiyo pale unakuwa ile miradi haitekelezwi. Sasa ni vizuri tumwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha atoe elimu kwenye Wizara zake**.** Tunapowaita Wizara nyingine tunaona wao walikuwa wanasubiri na wanasema Waziri wa Fedha hajatupa fedha na Waziri wa Fedha anasema hawajaleta *certificates* nilipe. Kwa hiyo, ningeshauri elimu hii ndani ya Serikali iweze kueleweka vizuri.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Msajili wa Hazina; walipoingia ni vijana wenye taaluma lakini wameweza kutoa mchango mkubwa kwenye Serikali hii. Kwa hiyo, ni jambo kubwa ambalo nafikiri kwamba ni vizuri tuwapongeze kama alivyosema bilioni 612 ambazo zimeletwa kama mchango ni jambo kubwa ambalo limesaidia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini niendelee kuipongeza tena Ofisi ya *CAG* kwa kazi nzuri wanayoifanya. Mwaka huu hautukupata nao shida kwasababu fedha walizoziomba kwenye Serikali hii wamepewa zote. Zaidi ya bilioni 19 imeongezeka kwenye Bajeti ya Mwaka jana kwahiyo tunategemea kwamba *output* ya *CAG* na Kiongozi huyu mahiri kabisa, Kichere wetu watafanya kazi nzuri. Nina imani kwasababu wako *serious* nina imani watafanyakaiz vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ambacho Mheshimiwa Waziri sijakipenda kwenye hotuba yako; jumla kwenye mafungu yako ulipanga jumla ya fedha za maendeleo bilioni 677 sasa katika bilioni 677 na umetumia tu bilioni saba sasa hapa Je, ni *poor planning* au ni *poor decision* au ilichukuaje? Tunaomba ukisimama utuambie kwanini ulipanga bilioni 677 halafu ukatumia bilioni saba katika mafungu yako yote.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuipongeza Benki Kuu; nimeona wametoa *initiatives* angalau za kupambana

ugonjwa huu kwenye *Bank borrowing rates* na *reserve* za Mabenki. Hiyo ni hatua nzuri tunampongeza *Governor* kwa kazi nzuri waliyoifanya lakini sasa waangalie; unaweza ukayapunguzia Mabenki yakawa yanapata fedha nyingi kwa faida ndogo lakini sisi tukaendelea kuumia. Ni vizuri sasa hii i-*transform* ije kwetu na sisi tuweze kufaidi mikopo yetu. Kama watu wanapata kwa asilimia sita kwanini Mabenki bado yanatoza Watanzania asilimia 17, 18, 20? Kwa hiyo, hilo ni jambo ambalo kwa kweli Waziri wa Fedha tunaomba ulisikie. Kama mnaweza mka-*intervene* sukari mnaweza kusema sukari bei iwe hii kwanini sisi kukopa ninyi hamtusaidii? Sukari ikipanda tu dakika mbili penyewe mmeshaingia kwa hiyo, ni vizuri sana na hapo muweze kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia nimpongeze Mheshimiwa Rais; Bajeti aliyoifanya na mambo yanavyokwenda vizuri sana na niwatoe wasiwasi; mifuko kwa mfano, ile ambayo tulipitisha bajeti kwamba ziweze kupata hizi ziwe *ring fenced* fedha zote Wizara ya Fedha wanapeleka. Nilikuwa nafikiri kwamba kuna mahali watafeli lakini utekelezaji umekuwa mzuri sana kwa hiyo ufanisi Kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango, Ndugu yangu, Kaka yangu tunaetoka Jimbo moja umefanyakazi nzuri, nakupongeza na Mungu ataendelea kukuona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho kwa wananchi wangu wa Buhigwe; kwa kazi nilizofanya bado tunajadili tuone Serikalini jinsi ambavyo naweza kupita bila kupingwa kwa sababu kazi niliyoifanya kule ni kubwa na wananchi wanaijua na Mheshimiwa Rais ametimiza ahadi zake zote, Rais akitimiza zote na Obama ametimiza zote kwahiyo, Mungu awabariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba. Nilishakutaja Mheshimiwa Peter Serukamba kwamba ndiye unayefuatia basi na kule Msekwa mjiandae kama yuko Mheshimiwa Elibariki Kingu atafuata kama hayupo Mhehsimiwa Mbaraka Kitwana Dau, Msekwa pia.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nianze kwa kumpongeza Waziri wa Fedha, Watendaji wote, Naibu Waziri kwa kazi kubwa waliyofanya kwenye Wizar ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, leo nataka niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge; kama mambo tunayoyaona Wizara ya Fedha yanafanyia vizuri sana yuko Mtu kwa bahati mbaya sana hatumsemi leo nimeamua nitumie nafasi hii nimpongeze kwa kazi kubwa sana anayofanya. Kama kuna watu wanafanya, wanatusaidia sana pamoja na Waziri na Watendaji wake basi naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Ndugu Dotto James. Dotto James amefanya mageuzi makubwa sana Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, usimamizi na udhibiti wa matumizi ya Serikali umefanyika kwa viwango vya hali ya juu sana na kwa namna yoyote ile ni kazi iliyofanywa na Dotto James.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kupunguza madeni hewa ya ndani yanayotokana na manunuzi ya ndani kutoka kwenye *tender* tumeshuhudia Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha anawaomba watu walete manunuzi waliyoyafanya ili aweze kulipa madeni, anakuta madeni hewa. Kazi hii imefanywa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumeshuhudia *financial discipline* hasa katika kusimamia *Cash budget* kulingana na Sheria ya Bajeti kazi hii imefanya na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha. Mimi nampongeza sana kwa kazi kubwa hii ya kizalendo ya kulitumia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mifumo ya kielektroniki *(GPeG)* ni amefanya kazi kubwa sana Ndugu Dotto James. Nampongeza sana. Leo unaweza ukaona maduhuli ya Serikali yamekuwa makubwa sana kwasababu ya ku-*embarrass technology* na niwaombe sana watu wa Serikali tuendelee. Tunaona leo *TRA* inafanya mageuzi makubwa, wanakusanya pesa nyingi sana, ni

kwasababu ya matumizi ya kiteknolojia na yote hii ameisimamia kazi hii kwa tija kubwa Ndugu Dotto James na wenzake wote pale Wizarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumeona udhibiti wa matumizi yasiyokuwa na tija kwa kupata *value for money*. Nakumbuka hata ukimuita kwenye Kamati ya Bajeti unaona anajua anachokifanya, ana uzalendo na ndiyo maana leo tumefika hapa Wizara ya Fedha inafanya kazi nzuri sana kwasababu pia mfumo wa manunuzi wa *TANEP* sasa hivi wameleta mfumo mpya wa manunuzi ambao unaleta uwazi, unaondoa upendeleo na yote hii ni kazi kubwa ameisimamia Katibu Mkuu wa Wizara ya fedha. Mimi nampongeza sana kwa kazi hii kubwa ya kizalendo anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumeona matumizi ya Serikali yanayosimamiwa kwa kutumia mfumo wa *TSA* na hili nataka niliseme; unaweza ukaona Wizara nyingi zinasema hazijapata fedha lakini kwasabbau hawajajua namna ya kusimamia hayo manunuzi waliyoyapanga *in a year*. Tulizoea zamani, tukimaliza kupanga Bajeti, Makatibu Wakuu wa Wizara zote wanapelekewa mapesa *whether* wametumia, hawajatumia, ikifika mwisho wa Mwaka hela zote kama hazijatumika zinarudi Hazina. Hili amelikataa Katibu Mkuu wa Wizara ya fedha. Anawataka tutoe fedha kulingana na *needs* zilizokuwepo. Hili ni jhambo kubwa na nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwa suala la *consolidating financial statement;* sasa hivi serikali inatoa kitabu kimoja na tumeona kitabu chao sasa *report* za uhasibu ni nzuri sana. Nampongeza sana, sana, sana kwa kazi nzuri hiyo anayofanya.

Mheshimiwa Spika, lakini pia niwapongeze watu wa Wizara ya Fedha kwa ujumla, Waziri Mpango, Katibu Mkuu na wote kwa kufanya maamuzi ya kuanza kutumia *force account* katika miradi ya maendeleo. Mnaweza mkaona leo Vijijini miradi ya maji, miradi ya barabara, miradi mingi sana inafanyika kwa fedha ndogo kwasababu ya kutumia *force*

*account.* Haya ni mageuzi makubwa na tunapata *value for money* lakini pesa zetu kidogo tunafanya miradi mingi sana. Mimi nawapongeza sana, sana kwa kazi kubwa hii mnayoifanya watu wa Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, pia nataka kuongelea Msajili wa Hazina; tunayo Makampuni 267, katika haya, Makampuni 37 tuna ubia na tunaweza tukaona tunatarajia kupata *dividend,* tunapata *15 percent* ya *gross turnover,* tunapata *70 percent* ya *redemption* ya *excess capital* na mikopo kwenye Taasisi ambazo wanalipa riba, matokeo yake ni nini? Waziri wa Fedha amesema tumeongeza fedha nyingi sana kutoka kwenye non-tax revenue kulingana na *dividend*. Lakini hii yote imefanikiwa kwasababu kuna usimamizi thabiti wa haya Mashirika ambayo yako chini ya treasury.

Mheshimiwa Spika, nataka kumuomba na najua kazi hii Dotto utaiweza; naombeni sasa tuanze kwenye Makampuni yote ambayo Mataasisi ya Serikali tu-*embarass technology,* wote waende kwenye teknolojia tutapata fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuanze ku-*harmonise tax;* Mataasisi haya unakuta kodi ni nyingi sana matokeo yake yanakuja tutakuja kwenye *dividend* itakuwa ni kidogo kwasababu tuki-*harmonize tax* ninayo hakika tutatoka kwenye hiyo bilioni 600 tutafika mpaka trilioni mbili kutoka kwenye *non-tax* ambapo tutakuwa na Makampuni yetu. Naomba kazi hii tuifanye vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, lakini pia *decision making process;* nawaomba sana watu wa Wizara ya Fedha kuna baadhi ya maeneo tunachelewa sana kufanya maamuzi na kwenye Mataasisi haya, kwenye Makampuni haya huko ni biashara. Ili biashara iweze kwenda haraka lazima tufanye maamuzi kulingana na muda. Kwa hiyo, nimuombe Mtu wa *treasury registrar* ahangaike kuhakikisha maamuzi ya haraka yanapatikana ili tuweze kupata fedha hizo. Lakini pia tusimamie uongozi kwenye haya Mataasisi, tuangalie bodi tunazoteua watusaidie kazi zetu vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho nataka kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Ndugu Dkt. John Pombe Magufuli; watu wa Kigoma wamenituma, sisi Kigoma tuna deni kwa Rais Dkt. Magufuli na wameniambia watalipa deni hili tarehe 25.10.2020. sisi kilio chetu kilikuwa ni barabara ya Nyakanazi-Kigoma tumeipata tayari, kilio chetu ilikuwa ni kutuunganisha na Tabora tumeanza kuunganishwa na Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia niwakumbushe kuna suala la soko muhimu sana lile soko la Kagunga. Najua Serikali ilitenga fedha kwasababu ya watu kufanya vibaya kwenye baadhi ya Halmashauri wakasimamisha zile fedha ninawaombeni Mtu wa JKT yuko pale, zile fedha zirudi ili tumalize soko lile la kimkakati.

Mheshimiwa Spika, pia tunajenga hospitali za Wilaya ya Kigoma, tuna fedha kwa ajili ya hospitali ya Mkoa, tuna fedha kwa ajili ya miradi ya maji mingi Mkoa mzima wa Kigoma lakini pia tuna fedha kwa ajili ya kutuunganisha na gridi ya Taifa kutokea Tabora, kutoikea Nyakanazi. Yote haya yamefanya ndani ya miaka mitano hii ya Rais Dkt. Magufuli na ndiyo maana watu wa Kigoma tunalo deni. Na niwahakikishieni deni hili tutalilipa tarehe 25.10.2020.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema huu ni Mwaka wangu wa tano watu wa Kigoma Kaskazini wanayohakika nitarudi hapa kuendelea kuwatumikia. Siyo kwasababu nyingine, ni kwasababu ya kazi kubwa aliyoifanya Rais Dkt. Magufuli maana kama rais ameleta maji, amejenga mashule, anajenga barabara, analeta umeme kila Kijiji sasa Mheshimiwa Serukamba unamuondoaje kwenye hiyo hesabu? Hiyo hesabu ni watu watatu; yupo Rais, yuko Mbunge na Madiwani wangu. Kwa kazi hii iliyofanyika, ninao uhakika tunarudi hapa Mwezi wa 11 ili twende kumalizia kazi hii kubwa ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kusema nakupongeza sana wewe unavyotusimamia kwenye Bunge lako tukufu, nikupongeze Naibu Spika, nimpongeze Katibu wa Bunge lakini pia niwapongeze Waheshimiwa Wabunge

kwa kazi kubwa tunayofanya ya kutekeleza na Wenyeviti wote wa Kamati wenzangu lakini pia nikipongeze Chama Cha Mapinduzi kwa kuhakikisha Ilani yake inafanyakazi. Serikali hii imetekeleza Ilani ya Chama chetu kama ilivyopewa baada ya kuanza kampeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema nampongeza sana Waziri Mpango kwa kai kubwa aliyofanya, nawapongeza sana watu wa Wizara, nampongeza sana *CAG* rafiki yangu Kichere, nina uhakika Ofisi ya *CAG* na Bunge lako litafanyakazi nzuri sana kwasababu namfahamu Kichere ni Mtu muungwana lakini ana heshima ataliheshimu Bunge lako na tutakwenda mbali zaidi.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema nawashukuru, naunga mkono hoja ya Bajeti hii ya Wizara ya fedha, ahsanteni sana, nendeni mkaendelee kutufanya tuwe na Shime ili tufanikiwe katika mambo yetu. Ahsanteni sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Peter Serukamba tunakushukuru sana kwa mchango wako. Nilisema tunakwenda Msekwa kama yupo Mheshimiwa Elibariki Kingu aanze na atafuatiwa na Mheshimiwa Mbunge wa Mafia.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa kabisa nitumie fursa hii kuendelea kukupongeza sana Spika wetu kwa ujasiri wako na uzalendo mkubwa kwa Taifa lako maana ungeyumba hili Bunge leo tusingekuwepo hapa, ungeyumba leo tusingekuwa tunawasema Watanzania katika kuwapitishia Bajeti yao. Tunaweza tusiseme lakini nakwambia wewe utaingia kwenye vitabu vya historia, umekubali *mockery*, matusi na kebehi lakini umeyatanguliza maslahi ya walipa kodi wa Taifa hili mbele. Historia ya Taifa letu itakukumbuka Mheshimiwa Ndugai wewe na Naibu Spika wetu pamoja na Katibu wetu wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika, wiki mbili zilizopita nilichangia katika Bunge lako Tukufu nikatoa ushauri

wangu kama Mbunge namna gani Serikali yetu na hasa *BOT* nilitoa ushauti kwa *BOT* nikasema *BOT* mnalo jukumu kubwa la kuangalia mwenendo mzima wa uchumi katika kipindi ambacho Dunia iko katika crises na pandemic kubwa ya virusi vya corona.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme wka unyenyekevu mkubwa, Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ni serikali sikivu na hii ndiyo sababu imefanya Serikali ya Chama hiki imeendelea kuaminiwa na Wananchi toka nchi imepata uhuru, Chama Cha Mapinduzi kinaendelea kushika hatamu.

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu maelekezo waliyoyatoa katika *financial institutions* yameleta faraja kubwa sana kwa Taasisi za kibiashara na kwa Watanzania kwa ujumla. Ninatoa pongezi zangu za dhati kwa viongozi wa Wizara ya Fedha ukiwemo Waziri Kaka yangu Dkt. Mpango, Katibu wako Mkuu kama alivyosema Kaka yangu Mheshimiwa Serukamba, Kaka James Dotto pamoja na *BOT* kwa ujumla; haya miliyoyafanya yanazidi kuleta *smooth environment* zitakazokwenda kuleta *land slide victory* kwa Chama Cha Mapinduzi uchaguzi unaokuja Mwezi wa 10.

Mheshimiwa Spika, ninawpaongeza sana Viongozi wetu kwa kuwa wasikivu maana Wabunge tulipiga kelel Bungeni lakini Serikali yetu haijapita muda imechukua hatua. *This is all about good governance,* tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, niende katika suala zima la *economic diplomacy;* ni wazi sisi Tanzania siyo kisiwa, pamoja na kazi nzuri sana inayofanywa na Serikali yetu ya Chama Cha Mapinduzi, pamoja na kazi kubwa inayofanywa na Rais wetu pamoja na Mawaziri wake wote lakini bado tuna jukumu la kwenda *extra miles* mbele.

Mheshimiwa Spika, *extra miles* tunazohitaji kwenda kwa kuwa Taasisi za Kimataifa zimetoa relief ya kulipa madeni ambayo tulikuwa tunadaiwa, ninamuomba Kaka yangu Kabudi, Wizara ya fedha, Kabudi ni Gwiji aliyebobea katika masuala ya Sheria lakini pia Gwiji ambaye ameonyesha

uwezo mkubwa katika Wizara hii ya Mambo ya Nje. Niombe aungane na kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango Mashirika haya ya Kimataifa kama yatakwenda kujengewa hoja kwa maslahi ya Taifa letu tukapeleka hoja kwa *IMF*, *Wolrd Bank* na *some other international institutions* ambazo zimejikita katika ku-*finance* tunaweza tukapata *grants* ambazo zinaweza zikaja zika-*cube gap* ambayo nchi inaweza ikaipata kutoka na *crises* ambayo tunaweza tukaipata kutokana na kwamba tukashindwa kufikia malengo ya kukusanya *revenue.*

Mheshimiwa Spika, ninatoa wito sasa kwa Wizara ya fedha na watu wetu wote ambao wanashughulika na mambo ya Kidiplomasia tuanze mazunguzo na Mashirika haya ya Kimataifa, tuanze mazungumzo na nchi zetu wahisani za nje ili tuhakikishe ya kwamba *relief* hii kama nchi tunaitumia kwa ajili ya kupata fedha ambazo ikitokea tumeshindwa ku-*meet expectations* kutokana na bajeti hasa kutokana na mdororo huu wa uchumi ambao kimsingi *it's a global crises* tunaweza tukapata fedha ambazo zinaweza zikaisaidia serikali yetu ikatimiza na kumaliza miradi yote ya kimkakati ambayo imeasisi na Jemedari wetu, Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Spika, wewe unajua tunajenga *Standard Gauge rail,* tuna mradi wa *Stiegler's,* tuna miradi mingine mikubwa ya Kitaifa, tunajenga mahospitali nchi nzima. Hii yote imetokana na *sacrifice* kubwa ambayo imefanywa kwa uadilifu mkubwa na Wizara ya Fedha hasa watu wa *TRA.*

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika Serikali yetu kwa kipindi hiki cha Awamu ya Tano, kitu ilichokifanya imefanikiwa sana ni kuweka watu wasiotanguliza maslahi ya matumbo yao na kitanguliza maslahi ya Taifa. Ukiangalia *revenue* sasa hivi tunavyozungumza *TRA* leo imeweka kijana pale, Mcha Mungu, kijana mu-*adventist,* Msabato, Mcha Mungu mapato yamekwenda mpaka sasa hivi wanakusanya karibia 1.6 triliion. Mimi ninatoa pongezi za dhati sana kwa Kamishina wa *TRA* yeye na timu yake wanafanyakazi kubwa ya kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nijielekeze katika suala zima la *M'n'E (monitoring and evaluation);* ninatoa wito kwa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi waanzishe kitengo cha *monitoring and evaluation* haraka iwezekanavyo kwasababu hapa tunapozungumza pamoja na kazi kubwa inayofanywa na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi bado kuna miradi ukienda kwenye maeneo inafanywa bado kwa watu wasiowaadilifu kuna miradi haitekelezwi kwa kiwango ambacho walipa kodi walitegemea.

Mheshimiwa Spika, nitoe wito Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Wizara nyingine, fanyeni haraka kitengo hiki kikamilike ili walipa kodi kule; maana hatujui baada ya Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli kuondoka, hatujui atakayekuja. Tungeweza kuitumia neema hii tukaacha *legacy* kwa nchi Watanzania wakamkumbuka Rais huyu mpaka pale Yesu atakaporudi.

Kwa hiyo, wito wangu, naomba sasa Wizara ya Fedha hasa katika Kitengo kizima cha usimamizi wa miradi. Kaka yangu Mheshimiwa Dotto nimekusumbua sana. Nawapongezeni, mmenipa Vituo vya Afya viwili. Hata hivyo Mheshimiwa Kaka Dotto pamoja na Wizara niwakumbushe, kuna watu wangu wako mbugani kule Iyumbu, iko kilomita karibia 180 kutoka Makao Makuu ya Wilaya, hawana Zahanati, hawana Kituo cha Afya, hawana umeme.

Naomba kwa heshima na taadhima, kwa sababu tulishapitishiwa kwenye bajeti Mheshimwia Kaka Dotto na Mheshimiwa Dkt. Mpango mkitoka hapa ninaomba mkaagize fedha zihamishwe kesho kituo kianze kujengwa.

Mheshimiwa Spika, nataka nikwambie, katika mapato ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi watu hawa wanachangia karibia asilimia 17 ya mapato ya Halmashauri yangu. Kwa hiyo, tuwatendee haki watu hawa ambao wanalima mpunga tunaouza Kenya, Burundi na Rwanda. Namwomba Mheshimiwa Kaka Dotto chonde chonde, Mheshimiwa Dkt. Mpango ninakuomba, wapelekeeni shilingi milioni 500 tukaanze kujenga hiki Kituo cha Afya.

Mheshimiwa Spika, najua mkienda kujibana, kesho hizi fedha zitapatikana na watu wangu watajengewa Kituo cha Afya. Kule sisi kujiuliza maswali ya kura za Mheshimiwa Rais Magufuli halipo. Kwa sababu mimi nimeingia madarakani nimekuta maji yapo Kata mbili tu, lakini tangu nimeingia madarakani leo ninavyozungumza tumechimba maji zaidi ya vijiji 36. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa ninapozungumza karibia Makao Makuu ya Kata yote tumepeleka miradi ya zaidi ya mamilioni ya shilingi, maji yamechimbwa. Sasa suala la kuuliza kura za Mheshimiwa Rais, *to me that is not a question. Definitely* Serikali ya CCM kura itakazozipata uchaguzi unaokuja *it is unimaginable*, ni za kiwango cha juu.

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kusema, tunapozungumza suala zima la kuhakikisha ya kwamba tunaongeza mapato, naiomba Wizara ya Fedha, kwa taasisi na baadhi ya maeneo ambayo tumeweka ukiritimba wa kuwa na kodi, kodi, kodi, ambazo zina-*discourage* hata *FDI,* naiomba Serikali yangu Tukufu ya Chama cha Mapinduzi, ni wakati muafaka Serikali yetu kukaa na kufanya *review*. Kodi, kodi nyingi zinazovunja moyo wa wawekezaji kuja kuingia kwenye nchi yetu, naomba zifutwe. Kodi hizi zikifutwa tutapata *FDI* nyingi as *much as* tunapata *FDI* nyingi itatuwezesha kuwa na *tax base* kubwa na Serikali itakusanya kodi mahali pengi na kodi itakuwa kubwa, tutaharakisha maendeleo ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema Bunge lako tukufu halitaondoka katika historia ya mafanikio yaliyopatikana chini ya Awamu ya Tano. Wewe Spika, wetu, ninarudia: usingekuwa kiongozi shupavu, ukayumbishwa na watu ambao wanatumwa; kwao hata Watanzania wakose maji siyo haja, lakini umesimama imara. Umesimama imara kaka yangu, nasema, narudia, utaingia katika historia ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza sana na ninampongeza sana kaka yangu Mheshimiwa Mpango na

Wizara yake na Mwalimu wangu Mheshimiwa Dkt. Ashatu aliyenifundisha Chuo Kikuu cha Mzumbe, naye anaona madini ninayoyatema hapa, hana mashaka kwamba alitoa kijana aliyewiva, kichwa cha Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana kwa mchango wako Mheshimiwa Elibariki Kingu na shukrani pia kwa kututakia kila la heri Waheshimiwa Wabunge wote.

Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, atafuatiwa na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu. Mheshimiwa Dau, kule Msekwa.

Ukimya huu unaniambia kwamba hayupo, naendelea kukuita Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu wa humu ndani.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye bajeti hii ya Wizara ya Fedha na Mipango. Nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kutujalia uzima na kuweza kukutana tena kwenye kazi hii kubwa ya kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kutuwasilishia bajeti yake ambayo inatupa mwelekeo wa uchumi wa nchi yetu. Kwa hakika, hii aliyotueleza leo ni mipango ambayo ilikuwa imepangwa kwa muda wa miaka mitano kwamba tutawapeleka wananchi kwenye maendeleo wanayoyataka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nichukue nafasi hii kwa kweli kwa kuanza kabisa kushukuru kwa namna ambavyo miradi mbalimbali ambayo imeletewa fedha, imeweza kutusaidia katika maeneo; na katika Wilaya yetu ya Ikungi pale tulipata miradi mbalimbali ambayo leo tunaweza kusema itaenda kutukomboa sana. Kwa hiyo, niseme

kwamba kazi kubwa inayofanyika pamoja na miradi ya Kitaifa inaonesha wazi wazi kwamba Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Jemeradi wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli imedhamiria kuwaletea wananchi maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nichukue nafasi hii kwa kweli kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa miongozo yake ambayo leo inatuonesha wazi kwamba tunakwenda kuleta maendeleo ya kweli. Hata mnavyoona, ni kwamba hata ukuaji wa uchumi umeendelea vizuri kwa asilimia saba lakini mfumuko wa bei umeendelea kudhibitiwa ambao ndiyo umekuwa kilio kikubwa sana kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwa eneo hili la ugonjwa wa *Corona* ambao kwa kweli tumesema kwa muda mrefu na nimeona hapa Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri namna ambavyo Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba inadhibiti yale ambayo ni athari kubwa ambayo itaweza kujitokeza pamoja na kwamba kuna baadhi ya maeneo ya biashara pamoja na maeneo ya utalii na mambo kama hayo yalikuwa ni athari kubwa ya uchumi wetu. Hata hivyo Wizara mmekuja, niwapongeze sana Mheshimiwa Dkt. Mpango, nikupongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa namna ambavyo mnafanya kazi nzuri ya kuweza kutuongoza katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumeambiwa, *WHO* wamesema wazi kwamba huenda ugonjwa huu utaendelea, utakuwepo miongoni mwetu. Kwa hiyo, naendelea kusema tu kwamba tuendelee kujipanga; na hii ndiyo maana Mheshimiwa Rais ameoneshwa maono na Mwenyezi Mungu kwamba hatuwezi kuwa na *lock down* ambayo baadaye hatuwezi kujua itaisha lini. Leo nchi zilizoweka *lock down* zinarudi kazini tena. Maana yake ni kwamba Mheshimiwa Rais wetu aliona hatuna sababu ya kuacha kufanya kazi kwa sababu tu kuna ugonjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye hili niendelee kusema kwamba sisi Chama cha Mapinduzi na Wabunge mliotuchagua Watanzania na Mheshimiwa Rais wetu

tutaendelea kusimama nanyi kwa sababu maisha lazima yaendelee na tunaendelea kutoa tu pole kwa wote waliopata athari ya ugonjwa huu, lakini hatuwezi kuacha kufanya kazi za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo mnaona wenyewe, leo wamemaliza *quarantine,* wengine wameanza kujitokeza humu, lakini ukiwauliza kwamba, je, sasa ule uwoga wenu wa *Corona* umeishia wapi? Hawawezi kukupa majibu ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawaomba Watanzania, tuendelee kuona aina ya watu ambao hawana dhamira ya kuleta maendeo na vyama vingine ni kama vile vikundi vya kuanza kutafuta maslahi yao binafsi. Chama cha Mapinduzi toka uhuru tumeendelea kuongoza nchi hii na kwa hakika mwaka huu tutaona vumbi litakalotimka kwenye uchaguzi. Tutashinda kwa kishindo kuhakikisha kwamba tunaendelea kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nieleze sasa kidogo na kuwapongeza *BoT* kwa kazi waliyofanya. Mheshimiwa Waziri mlisikia maoni ya Waheshimiwa Wabunge na kwa kweli mmefanya kazi nzuri, lakini mmeona mawazo ya Kamati ya Bajeti, nendeni mkasimamie sasa zile benki ili isije ikawa huku tumetoa maelekezo lakini kwenye utekelezaji ikawa ni bure. Mwisho wa siku haitakuwa na maana yoyote kumgusa yule mkopaji wa mwisho ambaye anafanya biashara zake za kawaida.

Mheshimiwa Spika, niendelee kusema tu jambo dogo, ni eneo hili la miradi ya kimkakati. Sisi kama uchumi ambavyo unaonekana unaendelea kuyumba na mapato yanaendelea kukusanywa kwenye vyanzo vingine, lakini tunapaswa kuwa na vyanzo vipya. Juzi tulikuwa na Wizara ya Kilimo hapa, tumeeleza kwamba Serikali iwekeze sana kwenye kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, nitaeleza kidogo; kwenye eneo langu pale kuna bwawa linaitwa Muyanji, liko kwenye Kata

ya Makiyungu na kuna mradi wa Skimu ya Umwagiliaji ya Mang'onyi. Ile Skimu ilitengewa fedha mwaka 2017/2018 shilingi milioni 100, lakini fedha zile hazikwenda. Leo hii lile bwawa kina chake kimepungua. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba hatuna uwezo wa kuwa na maji ya kutosha; na mwaka huu mvua zilivyokuwa nyingi lile bwawa lilitapika na lilitaka kuleta athari kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba fedha tunazoomba tuwe tunapewa ili tuweze kuboresha ile Skimu ambayo iko pale, itaenda kufaidisha wakulima wengi sana ambao walikuwa kwenye Kata ile ya Mang'onyi. Kwa hiyo, naomba sana kwa sababu fedha nyingi kwenye Halmashauri zetu kodi nyingi tunapata kwenye mazao, basi tuboreshe kilimo ili tuweze kupata mapato na itakuwa ni mapato mbadala ya haya ambayo yanayumba kwenye biashara mbalimbali. Kwa hiyo, nilitaka hilo nalo nilieleze.

Mheshimiwa Spika, wakati naenda kumalizia, nieleze jambo dogo kwenye eneo la wastaafu. Kuna baadhi ya wastaafu wetu wanastaafu lakini wanashindwa kulipwa kwa wakati na wengi wao wametumikia Taifa hili kwa uadilifu mkubwa. Kwa hiyo, nawaomba sana Wizara ya Fedha, tuwe tunawalipa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, hapa ninao mfano wa wastaafu wetu wachache wawili ambao wako kwenye Wilaya yangu ya Ikungi. Wazee hawa kwa kweli wanalalamika kwamba hawajatendewa haki na mpaka sasa hivi ni miezi saba. Pale kuna mzee mmoja anaitwa Mohammed Selemani Ntandu ambaye hajalipwa mafao yake mpaka leo na mwingine anaitwa Bwana Massawe ambaye alikuwa ni Afisa Mifugo. Yule naye hajalipwa miezi saba. Alilipwa kiasi, hajamaliziwa. Wakienda pale kwa wenzetu wa Shirika la *NSSF* hawapati huduma vizuri. Kwa hiyo, naomba sana *connection* kati ya Makao Makuu na kule kwenye Mikoa kuwe na majibu ya kuwasaidia na kuwapa faraja wale watumishi wetu ambao ni wastaafu. Nilitaka tu niombe hilo kwa sababu ni mambo ambayo yanapaswa yasaidiwe watu wetu ambao wameitumikia nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu jambo dogo, ni kwamba unapokuwa na aina ya vyama vya siasa, lazima vyama viwe na *focus* ya kuwatumikia wananchi. Mmeona wenyewe na Watanzania wameona wenyewe, kuna baadhi ya vyama tunaamini tukikutana Oktoba kitatoka kuwa chama cha siasa kitakuwa ni kikundi cha watu wawili watatu. Kwa hiyo, Watanzania watajua namna ambavyo vyama hivi havijajipambanua kwenye maendeleo. Kwa hiyo, nawaomba sana, unapofika wakati wa kwenda kufanya uchaguzi, wachague vyama ambavyo vinaenda kuleta maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho nimtie moyo sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya, kwa hikika Watanzania wamemwelewa. Watanzania hawatamwacha. Haya yote makubwa aliyofanya hayatafutika kwenye uso wa Watanzania. Nimtakie kila la heri, sisi wapiganaji tuko pamoja naye; na kwa Jimbo la Singida Mashariki naomba nimhakikishie kura nyingi atapata, Mbunge nipo na Madiwani wote watapatikana kwa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, nawatakia kila la heri Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, hata wale wakimbizi natumaini wamepata ujumbe. *(Kicheko)*

Sasa Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla King atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Mayenga.

**MHE. PROF. NORMAN A. SIGALLA KING:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kabisa nianze kukushukuru sana kwa kazi yako nzuri na kubwa ulioyoifanya ya kuliongoza Bunge lako Tukufu. Mungu akubariki sana. Wasaidizi wako wote Mungu awabariki sana kwa sababu umeliongoza Bunge lako Tukufu vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, nimpongeze Rais wangu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kuelekeza na kusimamia miradi mbalimbali ili ijengwe Tanzania kwa kutumia fedha zetu. Mungu ambariki sana. Sambamba na hilo nimpongeze Waziri, rafiki yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango na Naibu wake, wanafanya kazi nzuri sana. Kazi nzuri imefanywa kwa kuunda Kamati ya Kuangalia Fedha za Muungano ili suluhisho litolewe. Mungu akubariki sana.

Mheshimiwa Spika, pia kazi kubwa imefanywa katika ku-*maintain growth rate* ya uchumi wetu kwa nukta saba. Mungu akubariki sana. Kazi kubwa hiyo imefanywa hata kuwezesha barabara za lami kujengwa kutoka Njombe kwenda Makete na Makete kwenda Mbeya. Ni jambo nzuri sana umefanya Waziri wa Fedha na Waziri wa Miundombinu, nawapongezeni sana, sana, sana. Mmefanya jambo hilo kwa uangalifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, pia mmewezesha maji. Maji Makete sasa hivi kila sehemu ni mradi wa maji. Mheshimiwa Waziri wa Fedha nakupongeza sana kwa sababu ulifanya mradi wa Matamba - Kinyika ambao ulikuwa umepewa shilingi bilioni 4.9 bajeti ya kwanza, mkasema lazima tuweke kwenye *Force Account,* tukaishia kwenye *2.4 billion*; kutoka shilingi bilioni 4.9 mpaka shilingi bilioni 2.4. Sasa hivi ule mradi maji yanatoka Matamba, yanatoka Kinyika na mwezi huu tunategemea kuuzindua ule mradi. Mungu akubariki sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na mradi wa maji wa Kinyika na Matamba ambao ulinifanya nimwite Waziri Mkuu aje kule Makete, akafanya Mkutano pale Matamba, Kinyika, Kitulo, Ujuni na Makete Mjini ili kusitiza umuhimu wa maji kuwepo Makete. Nimemwita Waziri *Engineer,* amekuja akahutubia pale Matamba na Kinyika kusisitiza mradi wa maji na sasa hivi maji yale yanatoka, Mungu awabariki sana, sana, sana. Pamoja na mradi wa Kinyika na Matamba, mradi wa maji wa Tandala, Bulongwa, Lupalilo na Lugao ni miradi

ambayo muda wowote ule imeshaiva, maji yanatoka. Mungu awabariki sana, sana, sana.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Waziri wa Fedha amewezesha sana fedha kutengwa kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Ipelele. Kimefanyika kile kituo, sasa hivi kipo imara, kinatoa huduma zake vizuri. Mungu akubariki sana.

Mheshimiwa Spika, lingine ni umeme. Umeme Makete sasa hivi; vijiji vilivyokupangiwa mara kwanza vilikuwa 27, lakini kupitia mimi nikasema vijiji ambavyo havina umeme Makete ni 57 siyo 27 na sasa hivi vyote vinawekwa umeme kuanzia mwezi wa Saba mwaka huu 2020, vitawekwa umeme vijiji vya Tarafa ya Ukwama vyote. Mungu ambariki sana Rais wangu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kufanya kazi hiyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni wazi kabisa kusema kwamba uchumi wa Tanzania unategemea sana Wizara ya Fedha na Wizara ya Fedha imedhihirisha kwamba ina watu timamu, makini, wenye kutosha kuvaa viatu vya kuendeleza uchumi wa Tanzania. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kusema kwamba Rais wangu Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, itakapofika tarehe ya uchaguzi Makete apumzike kabisa, kwa sababu Wana-Makete wote tutakuwa na ari moja tu ya kumpa kura ya ndiyo Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kumpa kura ya ndiyo Prof. Norman Sigalla King. Kwa nini? Kwa sababu kazi walizofanya zinaonekana na zinapimika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni hitimishe hotuba yangu kwa kusema kwamba Wizara ya Fedha ikazane sana kwenye *Force Account,* kwani ndiyo mahali pekee ambapo unatumia wataalam wako mwenyewe. Tumedhihirisha Makete kwamba mradi wa maji wa Kinyika Matamba, ulipangiwa shilingi bilioni 4.9, lakini baada ya kuingia kwenye *Force Account* tumetumia shilingi bilioni 2.4, tumeokoa fedha, lakini wataalam wetu wa maji wa Serikali wamejiingiza kwenye kufanya kazi halisi, siyo za usimamiaji tu, lakini kujenga halisi halisi.

Mheshimiwa Spika, *Force Account* ndiyo faida yake kwamba unatumia wataalamu wako kufanya kazi halisi ili walete matunda yanayonufaisha. Wakati usipo tumia *Force Account* maana yake wataalam wako wanakuwa wasimamizi tu halafu hawajui kitu wanachokisimamia, lakini hii ya sasa ya *Force Account* ni biashara nzuri, mahali tunaweza, tufanye hivyo. Mungu awabariki sana, sana, sana na Mungu abariki kwa mchango wangu.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla King. Nimeshamtaja Mheshimiwa Lucy Mayenga na Mheshimiwa David Silinde ajiandae.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi nami walau kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Fedha na Mipango. Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, leo ikiwa ni mara yangu ya kwanza kusimama kama mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nimshukuru Mungu kwa sisi kama nchi kuendelea kuwa na Mheshimiwa Rais huyu; Rais bora kabisa, Rais ambaye anatutakia mema. Kwa kweli huwa nawashangaa sana hawa wenzangu upande wa pili ambao kila siku wanazungumza vitu vya ajabu kweli kweli. Kuna wakati roho inauma unatamani hawa watu pengine hata wasingekuwepo kabisa.

Mheshimiwa Spika, Rais bora kabisa, Rais ambaye anatutakia mema, Rais ambaye kwa kweli mimi huwa nawashangaa sana hao wenzangu upande wa pili ambao kila siku wanazungumza vitu vya ajabu kwelikweli. Kuna wakati roho inauma, yaani unatamani kwamba hawa watu pengine hata wasingekuwepo kabisa. Kwa sababu kama ukiwa mzazi halafu unakuwa una watoto wako, halafu unajitahidi kwa kila njia, kwa kila hali kwamba nijaribu kuweka mazingira mazuri na maisha bora kwa watoto wangu; halafu watoto hao ha oleo unasikia huyu kafanya hili kesho unasikia huyu kafanya hili, kesho kutwa unasikia huyu kafanya hili; kwa kweli bora tu tubakie hivi wasiendelee kubakia hata hapa Bungeni tubakie wenyewe.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu Mheshimiwa Rais wetu amejitahidi sana kwenye masuala ya kujenga nchi yetu katika sekta zote za kiuchumi wa nchi yetu, amejitahidi sana sana sana. Sasa hivi hata hatua hizi ambazo anaendelea kuzichukua kwenye suala hili la *Corona* ni hatua ambazo sasa hivi ndipo watu wanaanza kusema kwamba kumbe Rais alikuwa amefanya maamuzi ya busara. Kumbe vile alivyosema kwamba tusiwe na *lockdown* kumbe vile alivyosema tufanya vitu fulani fulani kumbe alikuwa sahihi. Ni kawaida sisi binadamu, tena mimi naona hasa ni waswahili, watanzania, kwamba mtu baadaye akishaondoka ndio maneno yanakuwa mengi alikuwa mwema na nini unafki mtupu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Waziri wangu wa Fedha pamoja na Naibu wake, wamefanya kazi kubwa sana; kwa kweli ndio timu pekee ambayo imeweza ku-*sustain* miaka mitano bila kuguswa guswa popote. Wakati wanaanza kazi hii ya kusimamia uchumi wetu watu walisema mengi sana, lakini hatimaye wanaanza tena kusema sasa tumekuelewa Mheshimiwa Waziri Mpango. Mheshimiwa Waziri Mpango na Naibu wako na Katibu Mkuu wako sasa timu hii tumeielewa; ndivyo binadamu ndio walivyo.

Mheshimiwa Spika, niliwahi kusema katika moja ya hotuba zangu kwamba kuna watu wanasimama wanaongea vitu vya ajabu sana kuhusu Rais wetu na kuhusu Serikali; nikasema ipo siku mtakuja kumeza matapishi yenu. Sasa hivi sitaki kusema lakini nadhani nyie wenyewe mnaona sijui kwa sababu muda wa miezi imekaribia ya uchaguzi au vipi. *(Makofi)*

Mhehsimiwa Spika, nipongeze sana kuhusu hatua ambazo zimechukuliwa na Serikali kwenye suala la *monitoring policy* kwa *BOT*, wamefanya hatua kubwa sana na hatua nzuri sana. Hata hivyo nilikuwa naiomba Wizara hii ya Fedha itusaidie kwenye *Fiscal policy,* kwa maana ya *tax return* walau muweze kubadilisha; yale mambo ya kufanya *monthly* basi iwe ni *monthly;* lakini *at least* iwe, kwa siku 60 badala ya siku 30, *tax return.* Kwa sababu tunajua kwamba kuna sekta nyingi

ambazo zimeathirika sana katika kipindi hiki cha matatizo haya na janga hili; na hasa tukizingatia kwamba ni janga ambalo hatukulitarajia; ni kitu ambacho kimetokea hatukuweza kukijua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo lazima wizara hii ijitahidi sana kuangalia kwenye *Fiscal Policy* mambo kule waweze kuyarekebisha. Huku kwenye *Monetary Policy* tumeshasikia na tumeshaona ambacho tu nakiomba ni kwamba wizara iweze kusimamia, kwa sababu wakati mwingine kinachosemwa ni kingine na kule *on the ground* ni kingine, watu wanaendelea kutozwa riba kubwa kama kawaida nakadhalika kwa hiyo kidogo inaweza ikatusumbua.

Mheshimiwa Spika, nipongeze kuhusu Ofisi ya *CAG.* Ofisi ya *CAG* imeweza kuokoa takribani bilioni 1.4, ni pesa nyingi sana za Watanzania. Mheshimiwa Rais mara nyingi sana amekuwa anasema kwamba nchi hii imekuwa ikiliwa kwa muda mrefu sana. Ofisi ya *CAG* kwa kufanya hivyo wameanza sasa hivi kukagua taasisi pamoja na mashirika ya humu ndani; wameenda kukagua *BOT. BOT* ilikuwa inakaguliwa mara ya mwisho na hizi taasisi ambazo ni *private sector;* walikuwa wanakagua kwa takribani shilingi bilioni moja na milioni themanini, lakini Ofisi ya *CAG* imeenda kukagua kwa shilingi milioni 492.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya *CAG* imekwenda kukagua *TANAPA;* mara ya mwisho walikaguliwa kwa shilingi bilioni moja na milioni thelathini, lakini sasa hivi Ofisi ya *CAG* imeenda kukagua kwa shilingi milioni mia sita na mbili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaweza kuona kwamba kulikuwa kuna pesa nyingi sana zinapotea, kuna pesa nyingi sana ambazo zilikuwa zinakwenda kwenye mikono ambayo kwa kweli ndio ile ambayo ilikuwa inaonesha kwamba nchi ina pesa nyingi sana lakini hazionekani kwenye uchumi wa wananchi moja kwa moja. Kwa hiyo ninampongeza sana sana Mheshimiwa Rais, ninapongeza sana hatua hii ambayo imechukuliwa.

Mheshimiwa Spika, lakini hatua hizi ambazo zimechukuliwa kwenye Ofisi ya *CAG* watu wanapiga vita na nitawaeleza kwa nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wanapiga vita kwa sababu zamani taasisi na ofisi hizi za *private sector* ambazo zilikuwa zinahusika na mambo ya ukaguzi wao ndio walikuwa wanafanya hizi kazi za ukaguzi kwenye mashirika na taasisi mbalimbali Serikalini, na hata huko kwenye kazi binafsi; lakini sasa hivi Ofisi ya *CAG* kuchukua kazi hii wanaona kwamba ulaji unapungua na sasa maneno yanaanza kuwa mengi. Mimi nilikuwa naomba Mheshimiwa Rais ninaomba Ofisi hii ya *CAG* iendelee hivyo hivyo, uamuzi huo wa kufanyika wa Ofisi ya *CAG* kuendelea kukagua haya mashirika ya ndani nakadhalika iendelee hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, na wanasema kwamba Ofisi ya *CAG* haina uwezo, lakini ofisi hii ndiyo ambayo kwa miaka sita mfululizo imekuwa ikigagua mashirika ambayo yako chini ya Umoja wa Mataifa. Wamekuwa wakikagua vizuri sana na hakukuwa na malalamiko wala nini. Lakini sasa hivi kwa sababu wanaonekana sasa wanaanza kuingia kule ambako kulikuwa kuna maslahi makubwa ya watu maneno yameenza kuwa mengi. Kwa hiyo mimi nilikuwa naomba, na nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuidhinisha watumishi 25 ambao watakuwa ni wakaguzi wataalamu katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, labda tu cha kuongezea, ni kwamba tujitahidi kupata wakaguzi ambao watakuwa ni wazuri na wamebobea katika zile sekta ambazo ni mpya kama *oil and gas* nakadhalika. Hiyo itasaidia sana, kwa sababu kama bajeti walau mmeongezewa, najua kwamba maslahi ya watumishi yatakaa vizuri na kila kitu kitakuwa sawasawa. Lakini tukiendelea kwenye hilo ofisi hii hii ya *CAG* lazima pia Serikali ijaribu kuangalia; hivi hawa ambao walikuwa wanafanya hizi kazi za ukaguzi yalikuwa ni mashirika ya nani, ni ofisi za nani, ni kampuni za nani? Kwa sababu haya maneno yanaweza yakawa yanasemwa kumbe ni watu ambao tuko nao humo humo, wako humo humo. Kwa hiyo wao inakuwa ni rahisi kuanza kupaza sauti kwa kutumia watu;

kwamba jamani hebu pigeni makelele huko kwamba Ofisi ya *CAG* haina uwezo; uwezo unajengwa.

Mheshimiwa Spika, hii nchi imefika hapa tulipo katika baadhi ya maeneo kwa sababu tu ile ya kusema kwamba hiki hatuwezi, au kwa sababu tu ya kusema kwamba tuna maslahi binafsi. Hicho ndicho kimekuwa kikisababisha hata ajira za watu; vijana wanalalamika wanataka ajira lakini mtu anasema uwezo, jamani jamani uwezo na nini! Kumbe hiyo inatumika kama kichaka watu kuweza kufanya mambo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa naomba sana msimamo huu uendelee na haya mambo ya sababu ambazo zinakuwa hazina kichwa wala miguu tusizisikilize kabisa.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa; nilikuwa naomba kukutakia kila kheri Mheshimiwa Spika wangu. Umekuwa Spika bora, umekuwa ni baba wa miongozo mingi sana kwenye maisha yetu. Mimi nakumbuka hata kwenye hili ambalo nimetoa shukrani umechangia kwa kiwango kikubwa sana.

Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Spika wetu, kwa kweli ni dada mwema, na mimi ninakutakia kila heri Mwenyezi Mungu akusaidie akusimamie kwenye kila kitu; yale yote ambayo unayataka yaweze kufanikiwa; na najua kwamba kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu mambo yatafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kwa sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge Mwenyezi Mungu atujalie tuweze kurudi huko kwenye majimbo tukiwa tuko sawasawa, tuwe na afya njema, twende tukagombee kwa wale ambao watapenda, na *Inshallah* tuweze kurudi mwaka huu 2020 mwishoni tuendelee kuja kuijenga nchi yetu na tuendelee kusukuma gurudumu la maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kwa vile tu kwamba hayupo hapa, lakini kama ni kuwataja mawaziri ningewataja wengi

sana lakini naomba Baraza zima la Mawaziri liweze kurudi na mambo yaweze kuendelea. Baada ya kusema hayo nashukuru sana asante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana na shukrani nyingi Mheshimiwa Lucy Mayenga kwa salamu za kheri kwa Waheshimiwa Wabunge wote. Mheshimiwa Davidi Silinde atafatiwa na Mheshimiwa Dokta Raphael Chegeni.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi kunipatia fursa hii kuchangia Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, wakati mchangiaji wa mwisho anazungumza alikuwa anasema kwamba upande wa pili hatumpendi Rais Magufuli; lakini niweke wazi, wako Wabunge wengi wa Upinzani ambao wanaamini katika utendaji wa Rais Magufuli. Tunachokifanya humu ndani tunapotoa maoni tofauti lengo letu ni kutaka kumfanya kuwa bora zaidi. Kwa hiyo michango yetu tunajikita kuonyesha pale ambapo Serikali tunafikiri kama mawazo tofauti ili kuona mnakuwa bora zaidi. Hata hivyo tunaamini aliyoyafanya na tunayaona tunaweza tusiseme lakini moyoni mwetu. Tunakiri kabisa kwamba Yule bwana ni mwamba na amefanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, sina wasiwasi na utendaji kazi wa Waziri Mpango na Naibu wake, sina wasiwasi na utendaji kazi wa Katibu Mkuu na timu yake nzima na wewe uendeshaji wako wa Bunge. Lakini pamoja na mambo mema yaliyofanyika bado kuna mambo ambayo tunataka Serikali iyaweke sawasawa ili pasiwe na hizo *contradiction* ambazo zimeendelea kujitokeza ama zitaendelea kujitokeza kutokana na watu ambavyo wamekuwa waki ama kupotosha ama Serikali kushindwa kutoa taarifa kwa wakati sahihi kwa sisi wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha na Mipango, Fungu ambalo tunalipitisha sasa linaomba kuidhinishiwa bajeti ya trilioni 12.39. Kati ya trilioni 12.39 trilioni 10.48 ni kwaajili ya kulipa deni la Serikali. Kwa hiyo unaweza kuangalia wana

mzigo wa kiasi gani; na ukipitia kwenye majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango moja ya jukumu lao kubwa ni kusimamia na kulipa deni la Serikali, lakini jukumu lao lingine ni kusimamia sera ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 12 Mei, siku tatu zilizopita Benki Kuu ya Tanzania ilikuwa imetoa *press statement* yake kuhusiana na *Monetary Policy;* ile *monetary policy* ilikaa ikajaribukuonyesha *measures,* hatua ambazo inachukua kutokana na athari za kiuchumi zilizotokanana ugonjwa wa *corona*. Sasa nimezungumzia hawa *BOT* wanaosimamia Sera ya Fedha lakini hapa nawaunganisha na Wizara ya Fedha na Uchumi ambao wao jukumu lao kubwa ni kusimamia Sera ya Uchumi, kwa maana ya *economic policy. Economic policy* ina-*involve* mambo makubwa mawili, sera ya kibajeti kwa maana ya *Financial Policy* na ina- *involve* vilevile Sera ya Fedha kwa maana ya *Monetary Policy* ambayo inasimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, utaona kwenye *BOT* kwenye ile *statement* yake wameonyesha hatua sita ambazo wanazichukua; na hatua hizo ni pamoja na kupunguza riba kwa benki zinazokopa kutoka *BOT;* utaona pale wameainisha wanatoka asilimia saba mpaka tano. Sasa jambo hili si baya, na mimi binafsi nimelifurahia baada ya kuliona vile, kwamba ndiyo sehemu ya michango ya sisi Wajumbe wa Kamati ya Bajeti tuliyokuwa tunaitaka Serikali ichukue hatua kuhakikisha tunapunguza ugumu wa maisha kwa wananchi wetu kwa kuongeza ukwasi kwenye benki ambayo itakwenda kwa watu wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, nimeona wamejaribu kupunguza *statutory minimum reserve* kutoka asilimia saba mpaka sita ambayo itakuwa *into effect* kuanzia tarehe 08 Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, bado mimi nina changamoto kidogo. *BOT* wamefanya jukumu lao vizuri, sasa nakuja kwa hawa watu wa Wizara ya Fedha ambao wao wana jukumu sasa la kusimamia sera ya kibajeti. Sasa ukwasi unakwenda kuongezeka kwenye benki sasa jukumu la pili Wizara ya Fedha

wao sasa wanaitafsiri vipi ile *Monetary Policy* ili iweze kutafsirika kwa wananchi wa kawaida kule chini.

Mheshimiwa Spika, sasa hii tumeiona ni kwa sababu; moja katika kipindi hichi cha miaka mitano *BOT* wameshusha riba za kukopa si mara moja, walishusha ikaja tisa, ikatoka tisa ikaenda saba, imetoka saba sasa hivi iko tano. Hata hivyo bado hawajajibu lile swali ambalo wananchi wanalihitaji, na hilo ndilo ambalo mimi nataka Wizara ya Fedha itueleze hapa. Kwa sababu matokeo yake ni nini; Benki Kuu imeruhusu kushusha riba na *reserve* za benki kuweka fedha zao ndani ya Benki Kuu, matokeo yake wananchi wa kawaida huku chini zile fedha zinabaki kwenye benki na ukienda kwa wananchi wa kawaida riba bado haijashuka. Hayo ndiyo maswali; jukumu hili liko kwa Wizara ya Fedha ambao wanasimamia sera ya kibajeti; ndiyo hayo tunataka; kwamba jamani mtueleze baada ya hatua za msingi zilizofanywa na *BOT* sasa ninyi Wizara ya Fedha mnafanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa maswali hayo nilikuwa naona ni vizuri Wizara ya Fedha na Uchumi ikaja ikatupatia majibu. Mimi nilikuwa na mapendekezo, kama Wizara ya Fedha itaona inafaa ili yaweze kutafsiri ile sera ya *BOT* sawasawa.

Mheshimiwa Spika, pendekezo langu la kwanza nilikuwa nataka Wizara ya Fedha sasa hivi iwaambie *TRA* pale kwamba wale wafanyabiashara wakubwa wanaoagiza bidhaa kutoka nje ya nchi wanapoleta bidhaa zao wale ambao hawana uwezo wa kulipa kwa wakati wanaweza wakalipa nusu na mizigo ikatoka wakaendelea kuendesha biashara. Wakati huo huo ile *half of the* gharama ya kikodi ambayo anapaswa kulipa pale mfanyabiashara mkubwa iendelee kulipwa pole pole kwa kipindi ambacho watakubaliana kati ya *TRA* na yule mfanyabiashara husika. Hii ni kwa nini nimeisema hivi, ni kwa sababu sasa hivi matatizo ya kifedha yameikabili dunia nzima na yamekwenda kwenye sekta za kibenki na kwa wananchi wa kawaida mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la pili, ambalolilitolewa na *BOT* miongoni mwa *measures* ni kuhakikisha kwamba benki zinafanya mapitio ya madeni kwa wateja wake wote. Sasa hili ni nini, ndilo lile tulikuwa tunasema kwamba jamani fanyeni *restructuring* ya mikopo watu; waliokuwa wamekopa kibiashara; tunaona biashara haiendi. Na hii nimesema kwa sababu gani, bado benki sasa hivi zinawachaji wananchi, kwa maana ya wafanyabiashara, riba zilezile ambazo walikuwa wanawachaji wakati uchumi wetu uko imara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni vizuri sasa Serikali kupitia Wizara ya Fedha ikahakikisha jambo hili linafanyika kwa wakati; kwa sababu kwa kuliacha hivi hivi benki zitakachokifanya, hapa faida inabaki kwa benki, haiendi kwa Mtanzania wa kawaida, yule wa chini, moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kuhakikisha na wao wanatoa sasa msamaha wa kikodi kwa wale wote ambao walikuwa na ile *tax amnest;* sasa muda uongezwe, usibaki ule ambao tulikuwa tumeupitisha kibajeti katika mwaka wa fedha uliopita.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kwa kifupi sana; ni kwamba tumeona kwamba, na hata Taarifa ya Kamati ya Bajeti imeeleza hapa, kwamba kuna dirisha la *IMF* na *World Bank* ambalo limetoa unafuu kwa nchi kukopa ili kukabiliana na hii *Covid 19.* Sasa kilichotokea tumeona pale, Kenya wenzetu walipata dola milioni 749, Uganda 491, Rwanda 109, *South Sudan* 7.6 *million Us Dollar,* Burundi dola milioni tano. Hizi fedha limetolewa dirisha dogo; sasa watu wengi wanasema *IMF* na *World Bank* wanatumia *Covid 19* kama sehemu ya kutaka kukopesha nchi maskini. Ni kweli, lakini bado haya madeni, kwanza taarifa ambazo watu wengi hawajui; hii mikopo ya kuruhusu hii *relief* ni zero *rated* yaani haina riba yoyote isipokuwa zile *charges* ndogo ndogo.

Sasa sio kosa kwenda kutumia fursa hii kukabiliana na janga la *corona* wakati huo huo wewe ukitumia fedha zako za ndani kuhakikisha kabisa kwamba uchumi wako unakuwa imara.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa sababu umeona kabisa kwamba hapa Wizara ya Fedha sehemu ya mchango wake mkubwa utaona deni la Taifa ni kubwa takriban trilioni 10.48 wangeenda kuomba kufanya *restructuring* ili walau kwa mwaka huu tulipe labda trilioni saba halafu trilioni tatu zinazobaki tuweze kujikita kuweza ku-*revamp* uchumi wetu uweze kurudi katika hali yake.

Mheshimiwa Spika, na hii naisema kwa sababu moja tu; ukiangalia *World Economic Analysis* ambayo inatolewa duniani nzima ni kwamba athari za ugonjwa wa *corona* zitakwenda mpaka mwaka 2023; na huu ugonjwa wameshaeleza hauwezi kuisha leo wala kesho, utakuwepo; yaani wanasema *is mind set disease.* Kwamba tukubaliane kuishi nao kama ambavyo yapo magonjwa mengine. Sasa kwa sababu tumeya-*accept* na tumeona athari yake tumeona athari kwenye utalii, biashara za utalii tumeona zilivyoshuka. Kwa mfano *TANAPA* peke yake wiki iliyopita kwa siku walikuwa wanakusanya zaidi ya milioni 500 mpaka 600 sasa hivi wanakusanya milioni 5 mpaka 10 kwa siku moja.

Mheshimiwa Spika, ukienda ukiangalia kwenye masuala ya ndege, kumeathirika, kwa hiyo hii yote ni athari kwa sababu watalii hawajafika nchini ambalo sio kosa la Serikali. Ukiangalia ndege zimezuiwa kwa sababu ni jukumu letu sote. Sasa sisi jukumu letu kama Bunge ni kuishauri Serikali kuhakikisha kabisa kwamba wanafanya mapitio yao upya kuhakikisha tuna *restructure* deni la Taifa, tusilipe, hiki kiwango ni kikubwa sana, *10.48 trillion* ni nyingi. Tuna uwezo wa kulipa lakini tujaribu kupunguza ili tuhakikishe tunasaidia hizi sekta nyingine za kiuchumi. Tusisahau kutumia hilo dirisha dogo tupambane na ugonjwa wa *corona* kulingana na muda ambavyo unakwenda ili kuhakikisha kwamba tunasaidia nchi yetu yote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo, nishukuru sana kwa kunisikiliza, lakini niwapongeze kwa majukumu makubwa ambayo mmeyafanya katika kipindi cha miaka mitano na Mwenyezi Mungu awabariki sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa David Silinde kwa uungwana wako na mchango wenye roho safi yenye nia njema, tunakushukuru sana.

Nilishakutaja Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni, utafuatiwa na Mheshimiwa Bobali.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda niunge mkono hotuba ya Bajeti hii ya Wizara ya Fedha. Kwa kweli imeandaliwa katika misingi ambayo kila mmoja anaona, kwamba nchi hii tuko kwenye changamoto za kidunia ambazo siyo tofauti na mataifa mengine yote.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwa vile sisi ni wanachama wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola *(CPA)* naomba ku-*register* kwanza *concerns* zangu kwamba kwa kipindi ambacho umekuwa Spika tumeona Bunge letu limepata mabadiliko makubwa sana; naomba nikupongeze kwa hilo. Nikupongeze sana kwa sababu Bunge sasa linakwenda katika mfumo ambao kweli wewe umetokana na *CPA* na umetumia vizuri fursa ya wewe kuwa mwakilishi wetu wa *CPA* miaka ya nyuma kutambua namna gani Bunge liweze kuendeshwa. Nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna watu walikuwa wanajaribu kutingisha kibiriti, kumbe hawakujua Mgogo kibiriti kimejaa, wamerudi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Bunge letu limekuwa ni mfano na *records* zitazidi kusema kwamba Bunge hili limeandika historia ambayo haitafutika. Mwenyezi Mungu akujalie afya njema na wananchi wa Kongwa, naomba mimi kama Msukuma, babu yao, mtani wao, niwaagize; kama kuna mtu anajaribu kuzunguka kule Kongwa ashindwe na alegee. Tunakuhitaji uje tena hapa kipindi kijacho uongoze Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada, umefanya kazi na wasaidizi wako, unaye Naibu Spika, Katibu wa Bunge na

timu yake; mmefanya kazi vizuri zaidi. Pamoja na haya, hivi leo hii kuna Mtanzania gani asitambue kazi nzuri ya Mheshimiwa Rais wetu? Kuna Mtanzania gani jamani?

Mheshimiwa Spika, leo hii, nchi hii yote maendeleo ambayo tulikuwa tunahitaji Watanzania kwa miaka mingi tunaanza kuyaona. Mimi katika Wilaya yangu ya Busega nina vijiji 59, kati ya 59, vijiji 56 vyote vimepata umeme safari hii, ni kazi nzuri ya Dkt. John Pombe Magufuli. Tulikuwa na matatizo ya miundombinu ya barabara, nazo zimetengenezwa; miradi ya maji, imejengwa na imekarabatiwa.

Mheshimiwa Spika, watoto leo hii katika shule zetu wanapata elimu vizuri tena bila malipo. Upande wa afya, akinamama wanajifungua, zahanati zimeboreshwa, vituo vya afya vimejengwa; haya yote ni kwa sababu ya maono makubwa ya Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. John Pombe Magufuli. Naamini kabisa Watanzania na Wabunge wenzangu mlioko humu ndani pasipo shaka Watanzania wote tutamuunga mkono na kumpa kura zote za ndiyo Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Spika, kwa vile ni Wizara ya Fedha, napenda niseme kidogo; Mheshimiwa Dkt. Mpango kuna wakati nilikuwa simuelewielewi, alikuwa haelewekieleweki, lakini sasa kadri tunavyokwenda na Naibu wake wameanza kuelewekaeleweka, wanaeleweka vizuri sasa hivi. Isitoshe Katibu Mkuu, kuna watu walipigapiga kelele hapa, Katibu Mkuu sijui kitu gani na gani. Jamani katika kusimamia masuala mazima ya makusanyo na matumizi ya fedha katika nchi hii, Katibu Mkuu wetu wa Wizara ya Fedha amefanya kazi nzuri sana; tumpe pongezi kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii nikupongeze tena, uliunda Kamati ya Uwekezaji Mitaji ya Umma; bila wewe hii Kamati isingekuwepo. Kamati hii imeweza kuchagiza kupatikana kwa fedha, *non-tax revenue* (mapato yasiyotokana na kodi) trilioni 1.05. Hii kwa sababu ulisimamia kuanzishwa kwa Kamati hii, lakini Mheshimiwa Rais akaweka msukumo mkubwa zaidi, Wizara ya Fedha na Katibu Mkuu na wale watendaji wote

wakiongozwa vilevile na Msajili wa Hazina, tumetekeleza jambo hili na sasa Watanzania wamepata fedha ambayo ilikuwa haipatikani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2014/2015, tulikuwa tunakusanya tu shilingi bilioni 161, umeona tofauti hiyo. Mwaka jana fedha ambayo tumekusanya moja kwa moja kupitia kwa Msajili wa Hazina ni bilioni 683.23, zilizokwenda moja kwa moja kwenye Mfumo Mkuu ni shilingi bilioni 370.59. Hiki ni kiwango kikubwa sana na ni mafanikio makubwa sana. Nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Timu yake, nampongeza Katibu Mkuu na nampongeza sana Msajili wa Hazina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Msajili wa Hazina naomba isaidiwe sana. Kwanza katika uteuzi wa bodi za mashirika yetu kwa sababu mashirika yasipokuwa na bodi ambazo ni *substantive,* zinafanya kazi, maamuzi yanakuwa ni tatizo. Leo hii katika mashirika yetu, kati ya 232, mashirika 176 ndiyo yenye bodi kamili ambazo zinafanya kazi vizuri, lakini 56 bodi bado baadhi ya wajumbe hawajateuliwa. Nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ahakikishe mchakato huu wa kuwapata wajumbe wa bodi kwenye taasisi hizi unakuwa ni wa wepesi.

Mheshimiwa Spika, pili, tuwe na utaratibu wa *graduation,* wasichague wajumbe wote kwa wakati mmoja ili muda unapokwisha kuwe na bodi inayoendelea. Kwa sababu bodi inapokuwa imekwisha taasisi inashindwa kufanya kazi vizuri kwa kufanya maamuzi ambayo ni sahihi. Kwa hiyo naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha mchakato wa kuteua wajumbe wa bodi kwenye tasisi hizi, naomba tujaribu kuuangalia na tuufanye kwa uharaka zaidi na wepesi.

Mheshimiwa Spika, linakuja suala hili a *Covid-19.* Sisi sio kisiwa, kuna watu Mheshimiwa Rais alipochukua hatua za mwanzo walianza kumbeza, ooh Tanzania Tanzania, leo hii ambayo Mheshimiwa Rais aliyakataa wameanza kurudi kule kwetu; leo hii ambao walikuwa wanajaribu kubeza wanaanza kuona Tanzania tumekuwa mashujaa. Leo Wamarekani

wanashuhudia kwamba kwa kweli Tanzania tulichukua msimamo sahihi katika kukabiliana na suala hili la ugonjwa wa *Covid-19. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wangu; tumejenga marafiki na tumejenga na maadui. Wapo ambao kwa makusudi wanatuonea wivu sisi kama nchi na naomba Watanzania tuungane, tuweke uzalendo hapa, uwe mbele zaidi. Wenzetu ambao siku zote wanakuwa na tabia za kubeza na kuandika kwenye mitandao kuichafua Tanzania kila kukicha, wanapata faida gani? *This is your country. Put your country at your heart.* Watanzania tukifikia hapo tutajenga nchi yetu. Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa sana tumtie moyo, tumtie shime, siyo Watanzania walewale wanaanza kubeza yanayofanyika. Leo hii kupitia na janga la *corona* Tanzania tumekuwa mfano na watafuata tu, wataiga tunavyofanya.

Mheshimiwa Spika, mimi niiombe Wizara ya Fedha kwamba kupitia bajeti hii lazima waendelee kulipa madeni, madeni ya ndani na hasa madeni ambayo Watanzania wanahitaji wapate fedha hizo waweze kuendelea kufanya shughuli zao vizuri. Suala la *VAT Refund* Mheshimiwa Waziri wa Fedha alisimamie vizuri. Naomba mchakato wa kusema kwamba tunafanya hivi, mchakato unaendelea, tunafanya tathmini na kadhalika, tuachane nayo. Watanzania wapate fedha hizi waweze kuendelea kufanya biashara zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la *specific sector targeting.* Katika mapambano haya lazima tu-*target* sekta zipi ambazo sasa tuweke nguvu zaidi, lazima tuwe na uwezo wa kuona kwamba sekta hizi zisaidiwe kuweza kusisimuka na ziweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, kingine katika suala zima la kiuchumi tunahitaji kupata *comprehensive recovery plan.* Katika uchumi kuna kipindi cha kufanya *recovery,* kuna *boom* na kuna *recession.* Sisi tunaingia kwenye suala ambalo sasa tusiingie kwenye *recession,* tukiingia kule tutapata shida sana kuja kutoka pale.

Mheshimiwa Spika, niombe suala la Benki Kuu. Ukiangalia juzi wametoa *statement* yao, *Monetary Policy Statement,* ni nzuri sana. Naomba kama Wizara waliangalie jambo hili kwamba sasa *the trickledown effect* inakuwaje kwa wananchi, kwa sababu bado ukiangalia Benki Kuu imeshusha sana riba mbalimbali na yamelegezwa masharti mengi, lakini tunataka tuone sasa *the effects* kwa wale watu ambao wana-*deal* na zile benki ili watu wa chini waweze kuona *impact* yake moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika hili sasa afanye *translation* hiyo ili wananchi sasa waweze kuona kwamba kuna unafuu unaotokana na hayo yanayosemwa na Benki Kuu. *Otherwise* inabaki ni suala la ku-*create liquidity* kwenye *market,* kwenye *banks,* lakini wananchi huku wanabaki kumangamanga na kuhangaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, muda huu Watanzania tumuunge mkono Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Wale wote ambao wana nia njema na nchi hii huyu ndiye kiongozi wetu pekee. Niombe hata wale wengine wenye nia ya kutaka kuweka wagombea kwa nafasi ya Urais wangemwacha tu, sioni sababu yoyote. Atimize majukumu kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema kwamba, naunga mkono hoja hii na nimtake Mheshimiwa Waziri wa Fedha; tunataka tuone the *ripple effect* ya Benki Kuu kushusha zile riba, kulegeza masharti katika mabenki, lakini wananchi waweze kufaidika namna gani na hicho kitendo cha kufanya namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni. Nilishakutaja Mheshimiwa Hamidu Bobali, atafuatiwa na Mheshimiwa Shally Joseph Raymond kule Msekwa.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutupa uhai na uzima na kuendelea na shughuli zetu za Kibunge.

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumze kwenye maeneo mawili ama matatu. Kwanza nimewasikia wenzangu wakisema juu ya umeme, Mheshimiwa Dkt. Chegeni ametaja mpaka vijiji. Nilisema siku ya Wizara ya Nishati kwamba vijiji 8,000 vilivyopelekwa katika kipindi hiki cha Awamu ya Tano ya Rais Dkt. Magufuli, sisi watu wa Mchinga hatujapata hata kijiji kimoja. Kwa hiyo naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha a-*take* na alipe kwenye *record;* vijiji kadhaa tulivyopata umeme pale Mchinga ni vilevile alivyoviacha Mheshimiwa Rais Kikwete. Mpaka sasa Awamu ya Tano leo huu mwaka wa tano, haijatuletea umeme kwenye kijiji chochote Jimbo la Mchinga.

Mheshimiwa Spika, nasema hapa kwa sababu huyu ndiye Waziri wa Fedha na ndiyo anaidhinisha fedha, ajaribu kumsukuma Waziri wa Nishati atupelekee umeme kwenye vijiji ambavyo mara zote vimekuwa vikiingia kwenye mpango; Vijiji vya Dimba, Ruvu, Namkongo, Matakwa na Mputwa.

Mheshimiwa Spika, pia nizungumzie juu ya suala la kuongeza *tax base;* sisi Ukanda wa Pwani tuna zao ambalo kwa sasa linakuja kwa kasi sana, zao la mwani na linalimwa karibu Ukanda wote wa Bahari kuanzia Tanga mpaka kufika Mtwara. Katika Jimbo la Mchinga wananchi wameitikia wito kwa kiwango kikubwa sana na kwa bahati nzuri zao hili wakulima wake wakubwa ni wanawake, ndio wakulima wakubwa wa zao la mwani. Sasa kwanza kumekuwa na *contradiction* ya kikodi kwa sababu *nature* ya zao lenyewe unaweza ukiliona linaweza likaingia kwenye kilimo kwa sababu ni kama majani, lakini pia lenyewe linalimwa baharini, maana yake liko kwenye Wizara ya Uvuvi, na anayeshughulikia ni Katibu Mkuu anayeshughulikia masuala ya uvuvi. Sasa naomba wasafirishaji wa mwani wanapotoka kwenye maeneo yale wanayonunua mwani wanakutana na kodi ambazo zingine walishazilipa, yaani watu wa Uvuvi

wanawatoza kodi zao wakamalizana nao, ukija tena huku watu wa Kilimo na wenyewe kwa kushirikiana na halmashauri wanatoza kodi tena kitu hikohiko kimoja kinatozwa kodi na Wizara mbili.

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu gani? Ni kwa sababu Wizara ya Fedha hawajaliweka kwenye sera na mipango kama ni zao ambalo linaweza likachochea uchumi kwenye nchi. Kwa hiyo ombi langu kwa Mheshimiwa Dkt. Mpango; waliweke zao la mwani kwenye orodha ya mazao ambayo yanaweza yakachochea uchumi wa nchi yetu kwa kiwango kikubwa sana. Halina gharama kubwa namna ya kulilima, lakini pia kwa Ukanda wetu wa Pwani ambao tunapata jua kwa muda mrefu, ni za ambalo linakwenda kupunguza umaskini kwa kiwango kikubwa sana. Kwa hiyo waliweke kwenye sera na kwenye mipango. Wakulima wale wa Mchinga II, Ruvu na natambua mchango wao mkubwa sana Maloo, Mvuleni, Kijiweni, Kilolambwani na Nang'ole kwenye Jimbo la Mchinga wamehamasika kwa kiwango kikubwa saa Mheshimiwa Dkt. Mpango.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa leseni za ununuzi umekuwa ni mgumu na jambo hili linasababisha wale matajiri kushusha bei. Hivi sasa bei yake ni Sh.1,000 mpaka Sh.1,500 kwa kilo moja, lakini upatikanaji wake ni mgumu sana. Kwa hiyo naomba wakiliweka kwenye mpango, sasa hivi namna lilivyo ni kama suala la halmashauri na Wizara ya Mifugo, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Fedha kwa maana ya Wizara ya Fedha sijaona *intervention* ya kutosha kuweza ku-*regulate* zile sera ambazo zingeweza zikapunguza hizo kodi ambazo zipo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu suala la athari za *corona* kwenye uchumi. Ni jambo la kawaida na kila mtu mwenye akili timamu anajua kwamba *corona* italeta madhara makubwa sana katika uchumi wetu. Niwapongeze sana Benki Kuu kwa hatua walizochukua. Napendekeza kwa Mheshimiwa Waziri; kwenye suala la ulipaji wa kodi pale *TRA* wafanyabiashara, isiwe lazima mtu alipe fedha ya miezi sita ama miezi mitatu, hasa vyombo vya usafirishaji. Nimeona pale

Lindi *TRA* imekamata magari mengi, malori mengi yanakamatwa kwamba hamjalipa kodi mnadaiwa na *TRA.* Napendekeza; kutokana na shida hii ya uchumi iliyopo ni kwamba hawa watu waruhusiwe hata kulipa kodi ya mwezi, mifumo ile ya ukusanyaji wa kodi waibadilishe, isiwe tu ina-*adapt* kwenye miezi mitatu, miezi sita na mwaka, hata mwezi mmoja, miezi miwili mtu akiweza kulipa aweze kulipa na aweze kufanya shughuli zake zingine.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu, wakisubiri mtu apate fedha ya miezi sita ama mwaka mmoja inatuletea shida fedha hiyo haipatikanaji, magari yanakamatwa. Bahati mbaya sana ukikamatwa unatozwa na faini, sasa kile kiwango chenyewe cha kulipa hana halafu mnamkamata anatozwa na faini, hiyo faini anaitoa wapi. Kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Waziri hili jambo waliangalie sana.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu na inawezekana likawa jambo la mwisho, Mkoa wa Lindi ni wakulima wakubwa sana wa kilimo cha ufuta na kwa Tanzania nafikiri ndiyo mkoa unaoongoza. Pia nchi yetu hili zao la ufuta ni nchi ya tatu duniani na ya pili katika Afrika kwa kulima ufuta. Ni zao ambalo linaingiza kipato kikubwa. Naweza nikasema Wilaya ya Kilwa peke yake mwaka jana iliingiza zaidi ya bilioni tano kutokana na ufuta. Halmashauri ilipata ushuru wa shilingi bilioni 1.4, zao la ufuta. Sasa hivi kule Ruvuma ufuta umeanza kununuliwa lakini bei imeshuka kwa kiwango kikubwa sana. Zinatolewa sababu kwamba ni athari za *corona*, mimi siamini sana.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, afanye tathmini; matumizi ya zao la ufuta sidhani kama yanaweza yakaathirika sana na uwepo wa *corona, l*akini pia ni kwa sababu zao lenyewe la ufuta wakati mwingine linasafirishwa kupelekwa nchi jirani hapa kama Kenya, wanunuzi wakubwa wanakuja wanasafirisha. Vile vile hata hao wa maeneo mengine ambao wanakuja kuchukua kama India, Vietnam na Morocco, ndio wanunuzi wetu, sidhani kama kuna shida ya usafirishaji wa meli…

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Spika, taarifa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Taarifa. Mheshimiwa Bobali, pokea taarifa tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na mchango mzuri wa Mheshimiwa Mbunge, nataka nimpe taarifa kwamba wanunuzi na walaji wakubwa wa bidhaa zinazotokana na ufuta ni Japan pamoja na China. China ndiyo nchi ambayo *corona* ilianzia na viwanda vingi vimesimama na watu wengi wamepunguzwa makazini. Kwa hiyo mahitaji ya ufuta yameshuka, kwa hiyo *corona* ina athari kubwa kwenye biashara ya ufuta.

**SPIKA:** Pokea hiyo taarifa Mheshimiwa Bobali umalizie.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na nimeipokea kwa mikono miwili. Sasa nilichokuwa nakisema ni nini…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Bahati mbaya ni kengele ya pili kwa hiyo…

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Ooh! Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Bobali, wakati unasema hamna hata kijiji kimoja kilichopata umeme, nilikuwa naona Mheshimiwa Salma anakuangalia, Mheshimiwa Salma Kikwete. Tunaendelea, nilishakutaja Mheshimiwa Shally Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Niko huku Msekwa, hali ya hewa ina afadhali kuliko baridi iliyo huko jengo kuu.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai kwetu sote na sasa tuko hapa tukichangia hoja huu ya Wizara ya Fedha kama wizara na mafungu yake. Namshukuru sana Rais ambaye ndiye Mwenyekiti wangu wa chama tawala, Chama Cha CCM kupitisha jina langu nami leo niko Mbunge katika mjengo huu.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru wewe binafsi kwa kuniteuwa kuwa kwenye Kamati hii ya Bajeti. Nimejifunza mambo mengi na niseme kwa kweli, Kamati ya Bajeti ni chuo kikuu cha aina yake.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru wanawake wa Kilimanjaro walionituma huku, nami sijawaangusha na nitaendelea kuwatumikia. Namshukuru Mungu kwa kuwagusa wao na wakaona kwamba, ninaweza kuwa mwakilishi wao.

Mheshimiwa Spika, nina wengi wa kuwashukuru pamoja na Wabunge wenzangu walionipa ushirikiano wa kutosha, lakini na viongozi wote wakiwemo Mawaziri, Naibu Spika na hata ulipomtuma Kilimanjaro kuja kukuwakilisha kwa wakati ule ulipopata dharura kwenye kongamano letu. Nikuhakikishie tu alituacha tukicheka kwamba, tuna amani na yote aliyotuambia tumetekeleza na hata zile ahadi tulizotoa siku ile ya kongamano, nikiwepo pia mimi, tayari tumeshagawanya yale shuka kwenye hospitali za mkoa.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafsi hii kuwapa pole wanafunzi watoka shule za awali mpaka vyuo vikuu kwa kuwa nyumbani saa hizi kwa ajili ya huu ugongwa wa *COVID-19*. Ni jambo ambalo linawasumbua, lakini niwaambie tu tuzidi kumuomba Mungu atalipitisha na ataliondoa tatizo hili na ndoto zao zitatekelezeka kwasababu, watarudi shuleni tena wasome na wapate walichokuwa wanakitaka.

Mheshimiwa Spika, ni jambo gumu sana unaporudi katoto kadogo kanasema kwa nini huendi shule, corona. Corona ni nini, ni ugonjwa unaoletwa na uchafu, wao wanajua ni uchafu kwasababu kunawa mikono kila wakati

ni kuondoa uchafu. Tuwaombee watoto wetu na wao niwaombe sana pia waendelee kujitunza, waendelee kujisomea nyumbani kwasababu, shule ipo na watasoma.

Mheshimiwa Spika, napongeza Waziri wa Fedha kwa hotuba yake nzuri na ninampongeza Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na timu nzima. Tumekuwanao mara kadhaa katika majadiliano kwenye kamati na tumewaelewa na wenyewe wametuelewa na ninasema kwa kweli, namuamini Mheshimiwa Dkt. Mpango siku zote sio mtu wa bla-bla kwa hiyo, mengi tuliyomueleza tumeyaona kwenye kamati na nina hakika anakwenda kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa na bahati kupokea maombi kutoka maeneo mbalimbali yanayohusu huu ugonjwa wa *COVID-19* katika tiba na mengi yanatoka katika zile hospitali teule. Kabla sijaendelea kuizungumzia hii bajeti ya Wizara ya Fedha naomba kupitia kwako, hizi hospitali teule zilizo mikoani zipatiwe *PPE – Personal Protection Equipment's,* maana mpaka wafike ile hospitali kuu kama vile Hospitali ya Mkoa Mawenzi kuna Hospitali kama *Kibosho Hospital* haina kabisa zile *PPE.* Hospitali kama ile hospitali iliyo kule Bombo, kule Same, haina vifaa hivi. Hospitali kama ile iliyo kule Rombo, *Huruma Hospital* haina vifaa hivi.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nipeleke ombi hili kwenye ile kamati ya maafa kwa sababu, huwezi kumpata mtu sasahivi kwenye *desk* lake. Naombea pia, hospitali zote za Tanzania nzima, hospitali teule zipatiwe vifaa hivyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba niende moja kwa moja kwenye hii bajeti, mengi yamezungumzwa na sitaki kurudia, lakini nitakuwa sijalitendea haki eneo langu la benki kama sitampongeza Gavana kwa hiyo hatua aliyochuku ya kuweza kupunguza hizo asilimia kwenye *interest* ya kukopa mabenki kwa mabenki na *statutory minimum reserve.* Hiyo yote italeta ukwasi katika mzunguko wa fedha nchini na hivyo basi, itasababisha benki kuweza kukopesha kwa wingi na benki zikikopesha zinahitaji wateja ambao wanaweza kufanya biashara. Na mteja

anayeweza kufanya biashara ni yule ambaye amefanya biashara akalipa.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna benki ambazo zimefanya biashara na Serikali au benki zimetoa, yaani kuna wafanyabiashara ambao wamefanya biashara na Serikali au wametoa huduma kwa Serikali wakiwemo wakandarasi, wazabuni na wengine, hata watumishi ambao hawajalipwa mafao yao. Hiyo inasababisha kuweza kuwafanya wasiweze kuendelea na biashara zao.

Mheshimiwa Spika, nimeona nijenge hoja kupitia hivyo ili nimuombe sasa Waziri wa Fedha atakapokuja kutupa majibu, pamoja na ufafanuzi wake aliotupa na hii naomba niisome kwamba yameshahakikiwa madeni yaliyofikia bilioni 327.8 na madeni haya ni ya wakandarasi, wazabuni. Wakandarasi walilipwa bilioni 14.6, watumishi wa Serikali bilioni 60.7, wazabuni bilioni 147.7, watoa huduma bilioni 15.8 na madeni mengine kama vile fidia na michango ya kimataifa wamelipwa bilioni 88.8, kweli napongeza hatua hiyo, lakini bado haijatosha, wako ambao madeni yao ni mengi na yameshahakikiwa, lakini hawajalipwa.

Mheshimiwa Spika, na hii hali ambayo imekuja kutokea sasa kutokana na huu ugonjwa hali inazidi kuwa duni kwa mzunguko, watu hawa ndio wanaofanya vijana wapate ajira mzunguko wa hela uwepo.

Namuomba sana Waziri wa Fedha atakapokuja kutoa majibu atuambie *cut off point* au muda maalum wa kumaliza kulipa madeni hayo ni lini, ili watu wawe njiani sasa kufanya tena biashara kwa mtizamo mpya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo naomba sana benki zitoe elimu kwa wateja wao kuhusu *LCs, LC* ni *Letters of Credit.* Tanzania watu walizoea kupanda ndege na kwenda kununua vitu vyao, wengi walipenda kwenda China, Guangzhou mnaita huku wenyewe Wachina wanasema Wanjuu, lakini sasa haiwezekani, lakini bahati nzuri ndege za *cargo* zinafanya kazi na hii ni pongezi kwa Rais wetu.

Mheshimiwa Spika, ningeomba sasa benki zitoe elimu kwa wafanyabiashara hawa, ili waweze kuagiza mizigo yao kupitia benki, walipie kupitia benki mizigo ije na Kariakoo iendelee kushamiri kama ilivyokuwa na vitu vingine viendelee kupatikana kwa urahisi. Baada ya kusema hilo nilikuwa naomba pia, nimuombe Waziri wa Fedha kwamba, ni wakati muafaka sasa wa kuwa na sera ya *monitoring and evaluation.*

Mheshimiwa Spika, ni ada kwako kwenye Bunge hili wiki mbili kabla ya vikao vya Bunge kuanza huwa unatoa ruhusa au huwa unatoa idhini na kugharamia Wabunge waende wakatembelee miradi, ili kuona ile hela iliyopitishwa kwenye bajeti, *voted funds* zimetumika kama inavyotakiwa. Na kweli mara nyingi tumekwenda na kufanikiwa na Mwenyezi Mungu akaturejesha salama, lakini mambo tuliyoyakuta huko taarifa unazo, kwingine inakutwa miradi hewa haikufanyika au hela hazikwenda zilivyotakiwa au miradi haikumalizika, lakini bado hakuna sera ambayo inaelekeza rasmi kwamba, jambo hili lisimamiwe na Wizara ya Fedha, ili na wao pia waweze kuona ile hela ambayo imetoka inatendewa haki. Kwamba, ile hela sasa inaweza ikafanya ile miradi mpaka ikakamilika tukaona na tukaonesha umma *value for money.*

Mheshimiwa Spika, jambo hili sio zuri sana, na ndio maana nimeona jioni hii ya leo kwa nafasi hii uliyonipa hapa niweze kusisitiza na ninaomba atakapokuja Waziri wa Fedha anipe jibu au atupe ufafanuzi je, iko kwenye mipango?

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi yako umeshatuitia semina mbalimbali na liliungwa mkono. Hili jambo ni jambo zuri sana kwamba, kwa kweli, ni muhimu kabisa watu hawa waweze kupatiwa sera iweze kutekelezwa, ili wote waweze kufanya kama ilivyo kwenye kanuni.

Mheshimiwa Spika, nimalizie sasa kwa kusema kwamba, hakika utendaji wako umesikia kila Mbunge akishukuru Mungu kwa wewe kuwepo, lakini zaidi wakikupongeza. Ungepewa na wewe nafasi kusimama

ungesema haya yote yasingewezekana kama sio kuwa na Wabunge kama sisi. Sasa naomba nikusemee, lakini pamoja na kukusemea hilo naomba nikusemee jambo moja katika jimbo lako; Wabunge hapa tungetamani kila mmoja ukatugawia kata kule kwako tukaenda kukufanyia kampeni, jambo ambalo hatuwezi, lakini tunakuombea kwa Mungu akupe afya na wale watu Wazidi kukuelewa urudi tena hapa bungeni ukiwa na afya tele. Mungu wetu ni msikivu na hilo atafanya.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Shally Raymond...

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, namuombea Rais wangu afya tele. Nakushukuru, asante sana, naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana tunakushukuru sana ahsante. Mungu akubariki pia, tunakuombea pia na wewe urudi Bungeni kwa kishindo.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, ili kwasababu, orodha yangu hapa bado ni ndefu na mimi ningependa kila mmoja wenu apate nafasi ya kusema angalau kwa kifupi, basi nawaomba turudi kwenye dakika tano-tano ili wote mpate nafasi ya kuzungumza. Tuanze na Mheshimiwa Lathifa Hassan Chande, atafuatiwa na Mheshimiwa Oscar Mukasa na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko atafuatia, kengele Italia mara moja tu baada ya dakika tano.

**MHE. LATHIFA H. CHANDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, japo kwa bahati mbaya sana imetokea hizi dakika tano zimetokea pale ambapo ninapoanza kuchangia na nilikuwa nimejipanga kutoa shukrani zangu so *I will try my best* kuongea kwa haraka haraka.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu kwa kuniwezesha kusimama tena kwa siku nyingine kuweza kuchangia, lakini pia nishukuru chama changu pamoja na changamoto zote zinazoendelea kwa kuniwezesha kuniteuwa na kipindi hiki chote nimeweza kushiriki nikiwa

kama Mbunge kwa muda wa miaka mitano. Vilevile napenda kukushukuru wewe pamoja na Naibu Spika na Wabunge wenzangu wote kwa kunipa ushirikiano katika kipindi hiki chote ambacho nimekuwa Mbunge bila kuwasahau watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuanza kuchangia katika Wizara hii ya Fedha; awali ya yote ningependa kuzungumzia juu ya suala la Wizara kutokuwa na *consistency* ya utengaji wake wa fedha kwenye mradi wa mpango kabambe wa ufuatiliaji wa kupunguza umasikini, yaani *poverty monitoring master plan.* Nimejaribu kupitia vitabu vya bajeti, *Volume IV,* ambako nimebaini ya kwamba, katika Idara ya Kuondoa Umasikini mwaka wa fedha 2021 kwenye kifungu kidogo cha 6508 cha Mpango Kabambe wa Ufuatiliaji wa Kupunguza Umasikini, yaani *Poverty Monitoring Master Plan,* hakuna pesa zozote zilizotengwa. Hali hii inasababisha nione kwamba, Serikali haioni umuhimu wa kuwa na ufuatiliaji wa tathmini ya hali ya umasikini hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha, mwaka 2018/2019 hakukuwa na fedha zozote zilizotengwa kwa ajili ya kufanya utuatiliaji wa tathmini ya umasikini. Mwaka 2019/2020 pesa ambazo zilitengwa ambazo zilikuwa ni fedha za nje ilikuwa ni milioni 288, lakini mbaya zaidi ni kwamba, mwaka 2020/2021 hakuna tena fedha zozote zilizotengwa kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, basi kwa ajili hiyo, nimuombe Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mpango, aje alieleze Bunge lako tukufu endapo hakuna *consistency* ya utengaji wa fedha hizi kwa ajili ya kufanya tathmini ya hali ya umasikini, hizo tathmini au takwimu za tathmini ya kwamba, umasikini unapungua anazifanya kwa mtindo upi? Na je, ni kweli umasikini unapungua kama hakuna fedha zozote zinazotengwa kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji na tathmini?

Naomba Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mpango, aweze kuja kutuambia ni kwa namna gani Taifa linaweza kupanga mpango wa maendeleo huku kukiwa

hamna *consistency* ya tafiti za ufuatiliaji wa kuongezeka ama kupungua kwa umasikini hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, dira ya maendeleo ya Taifa inataka hadi itakapofika mwaka 2020/2025 tuwe katika uchumi wa kati na maisha bora kwa kila Mtanzania, basi ningeishauri Serikali iweze kutenga fedha katika Fungu hili la 6508 kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wake wa mradi huu wa *Poverty Monitoring Master Plan.*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo napenda sasa kuzungumzia juu ya marekebisho ya sera za fedha za bajeti. Naipongeza Serikali na *BOT* kwa hatua hizi walizozifanya za marekebisho ya sera, yaani *monitory policy,* japo naona wamechelewa kidogo. Na ningeomba kutoa wito kwa Serikali kufuatilia hizi benki kama tayari zimeshaanza kutekeleza marekebisho haya na tayari majadiliano yameshaanza na wateja juu ya kufanya *restructuring* ya marejesho ya mikopo hiyo. Tunaomba Waziri Mpango atakapokuja kuhitimisha hapa aweze kutuelewesha kama hili suala limeshaanza kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na marekebisho haya kufanyika naona bado haitoshi. Tunahitaji Wizara nayo iangalie kufanya marekebisho katika sera yake ya fedha, yaani *Fiscal Policy,* li kuweza kunusuru Wananchi katika kupambana na ugonjwa huu wa *COVID-19,* Corona. Na katika hili napendekeza watakapoleta...

**SPIKA:** Asante sana ndio dakika tano hizo zimeisha.

**MHE. LATHIFA H. CHANDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lathifa Chande Hassan Kigwalilo. Mheshimiwa Oscra Rwegasira Mukasa atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, bahati mbaya nimeangukia kwenye dakika tano, lakini ndio maisha, ndio hali halisi.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa hiyo, maneno ya utangulizi yatakuwa mafupi sana. Naipongeza Serikali kwa kazi nzuri, kwa ujumla kazi ni nzuri. Nina maombi matatu kwa Biharamulo kwa Mheshimiwa Dkt. Mpango na Mheshimiwa shemeji yangu Naibu Waziri:-

Mheshimiwa Spika, moja, tulipata bilioni 2.8 ya mradi wa kimkakati wa ujenzi wa wa maegesho ya malori kwenye njia panda ya Nyakanazi kwenda Kigoma kutoka Kahama, Bukoba na kwenda Rwanda. Tukasaini mkataba na Hazina, lakini ikasitishwa na tumeshapata mkandarasi, hatujapata maelekezo, tunaomba kujua kwasababu ule mradi ni muhimu sana, hilo neno tu mkakati tulikuwa na *projections* zetu nyingi sana, tunaomba mtusaidie.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili naipongeza Serikali kwenye kutekeleza miradi ambayo wananchi walikuwa wanaanzisha kama maboma ya zahanati na maabara na vitu kama hivyo, lakini kwenye mpango huu baada ya kuondolewa *capital development grant* sasa hivi inakwenda zaidi kwenye elimu kwa sababu, ya *P for R,* lakini na kwenye afya kupitia TAMISEMI. Ile miradi ambayo wananchi walianzisha kwa mfano ofisi za vijiji imesahaulika na pale ndiko *a good governance* inakoanzia, tunaomba na yenyewe muitazamie dirisha la kupitia kama ambavyo *P for R* imepita kwenye elimu.

Mheshimiwa Spika, lakini la tatu tuna taarifa na tunajua jitihada zinaendelea za kutupatia na sisi fedha ya kuanza ujenzi wa hospitali ya wilaya, lakini tunaomba kasi iongezeke kidogo kwasababu, tunahitaji sana kwa sasa, hiyo ni Biharamulo. Na mfano wa kijiji ambacho kimejenga ofisi na haijamalizika ni Kijiji cha Bisibo, tunaomba mtusaidie kuwa na dirisha maalum.

Mheshimiwa Spika, pongezi kwa mara nyingine kwa Wizara, hii bahati mbaya ninyi mnatakiwa kupewa pongezi na pole; pongezi kwa kazi nzuri na pole kwa sababu mzigo mkubwa wote wa kupanga Kitaifa unaanzia kwenu kabla haujaenda kwenye Wizara *specific.* Mnafahamu nilidokeza

jana hapa, sasa hivi Dunia inaongelea *resilience* yaani uwezo wa kilichoanguka kurudi kwenye hali ya awali. Kwa hiyo, kama Taifa na Mataifa mengine tutatafuta ku-*resiliate* na sekta.

Mheshimwia Spika, moja ya njia sahihi; ziko nyingi, lakini moja ya muhimu sana ni *metric capacity* ya nchi. Unasikia Wabunge wengine wanasema *M&E,* mwingine sasa hivi anasema *consistency* na kwa kifupi wanasema *metric capacity* ya nchi, nami ndiyo maana nataka kusemea *census.*

Mheshimiwa Spika, sensa yetu iliyopita tulitumia takriban shilingi bilioni 156 lakini duniani sensa zinafahamika, zinatoa majibu ambayo kwa kweli hayapendezi sana, ni duniani kote, siyo Tanzania tu. Ndiyo maana nchi za dunia ya kwanza sasa zinaenda kwenye *vital statistics.* Sisi kwetu hapa *RITA,* vizazi wanasajili kwa asilimia 49 mpaka sasa na vifo ni chini ya asilimia 10. *NIDA* nao naona wanajitahidi sana lakini bado wana-*struggle.* Tutafute namna ya kuwekeza huko kama mbadala wa sense. Sensa ikija iwe inakamilisha tu baadhi ya vitu, lakini nguvu tuweke huku.

Mheshimiwa Spika, hiyo shilingi bilioni 156 ukiigawa kwa miaka 10, ukagawa kwa vijiji 12,000 na kitu, unakuta Mwenyekiti wa Kijiji au yeyote unayemweka kwenye kijiji pale unaweza kumlipa shilingi100,000/= kwa mwezi, *RITA* na *NIDA* wakamsimamia, ukapata *real time data,* ukawa na *metric capacity* na kuona kila siku *in real time* kuliko kusubiri hiyo miaka kumi halafu unaleta kitu ambacho bado hakikufai.

Mheshimiwa Spika, kwa wastani sasa hivi vizazi na vifo *RITA* wanakadiria japo hawajavikamata vyote, wanakadiria kama milioni saba na kitu. Ukivigawanya hivi, yule Mwenyekiti wa Kijiji au yeyote kwenye kijiji anaweza aka-*register demographic events,* wastani wa 55 mpaka 100. Kwa pesa ile anaweza aka-*register* vizuri, akasimamiwa na *RITA* na *NIDA* kwa ngazi ya chini wilayani kule ukapata matokeo mazuri sana kuliko kusubiri sensa ambayo inakuja baada ya miaka

kumi, lakini *output* yake inafahamika duniani, siyo Tanzania. Haijakaa vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Wizara ya Fedha na Mipango kwa sababu ndio magwiji wa mipango yetu, hebu tuchukue namna ya kuongeza *metric capacity* kwa kupunguza gharama ili tusiongeze mzigo, kwa sababu *Corona* imekuja na wataalam wanasema sasa hivi itakaa *flat,* haitaongezeka sana lakini itakaa *flat* kwa muda mrefu sana. Kwa hiyo ni jambo tunakwenda kuishi nalo. Kwa hiyo, *metric capacity* ni ya muhimu sana, ndiyo maana unasikia wenzangu waliotangulia wanasema *M&E.* Ili *metric capacity* iwepo ni lazima tutafute namna ya ku-*save cost* na kupata matokeo mazuri zaidi. *Resilience,* moja ya jicho lake kubwa ni *data* na *evidence.* Sasa *evidence* utaipata kwa kuwa na *real time data* kuanzia kwenye ngazi ya kijijini na kata na tutaifanya vizuri kama tutawekeza kule chini.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Maoni yangu kwa Wizara ya Fedha ni hayo. Nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru sana kwa kuzingatia muda. Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwanko, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Salum Khamis, endapo yupo kule Msekwa.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Moja kwa moja nianze kwa kukushukuru wewe Dkt. Mpango, Naibu wako na timu yako yote ya Hazina pale. Umefanya kazi nzuri, hongera sana. Nasi Wabunge wa Kigoma tunasema umetupa heshima kubwa kwa uadilifu wako wa kazi. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina mambo machache sana. Kwanza nataka niwashukuru sana *TRA.* Baada ya kukutana na watu wa Wizara ya Fedha tuseme kupitia *TRA,* baada ya Mheshimiwa Rais kukutana na wafanyabiashara wa aina mbalimbali wa madini, *retail trade* na wengine, kwa kweli *attitude* ya *TRA* imebadilika sana. Sasa wanawaona wafanyabiashara kama wabia wa biashara. *TRA* hongereni,

Hazina hongereni. Tunataka *spirit* hii ya mahusiano mazuri kati ya wafanyabiashara na *TRA* yaendelee vizuri na *of course* bila ku-*compromise* mapato ya Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda niliseme ni swali. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, yamekuwepo mazungumzo; nazungumzia juu ya hii *central corridor* kwa maana ya Dar es Salaam mpaka Kigoma. Barabara inayojengwa katika *central corridor* Chaya – Goweko inajengwa sasa hivi, hongera, lakini barabara hiyo hiyo maana yake ni pamoja na kipande cha kutoka Tabora kwenda Kigoma ili kukamilisha hiyo *central corridor.* Kipande cha kutoka Malagarasi Darajani mpaka Uvinza, kumekuwa na mazungumzo ya muda mrefu sana katia ya *OPEC Fund* na Abudhabi *Fund,* huu ni mwaka wa nne.

Napenda utakapokuja utueleze, hayo mazungumzo ya *OPEC Fund* na *Abu Dhabi Fund* kukamilisha kile kipande cha kilometa 51 ili *central corridor* iweze kuwa na maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aje atueleze, vinginevyo kile kipande kinasumbua sana na *central corridor* inakuwa haina maana. Maana tafsiri ya *Central Corridor* ni pamoja na kutoka Dar es Salaam kwenda mpaka kwenye nchi za jirani za Congo, Burundi na Rwanda. Kwa hiyo, naomba utakapokuja uweze kufafanua juu ya jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa niliseme, nchi hii ina mikoa miwili tu ambayo haijaunganishwa kwenye gridi ya Taifa. Mikoa hiyo ni Mkoa wa Katavi na Kigoma. Sasa nimeona kwenye hotuba ya Waziri wa Nishati, mikoa hii imetengewa fedha za kukamilisha kazi hiyo.

Naomba kupitia kwako, Waziri wa Fedha, ni wakati sasa mikoa hii miwili ya Kigoma na Katavi iunganishwe kwenye gridi ya Taifa. Najua kutakuwa na shida ya kibajeti kutokana na maradhi haya ya *Corona*, lakini katika uchache

huo, kipaumbele kikubwa kielekezwe kuunganisha mikoa hii miwili kwenye Gridi ya Taifa ili mikoa hii nayo ifanane na mikoa mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe unajua kwamba umeme ni kila kitu na mikoa ambayo hatuna umeme wa gridi bado tuna umeme wa *generator* ambao kwa kweli matumizi yake ni madogo na tija yake pia inakuwa ni ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo napenda nilizungumzie kwa kweli ni kuishukuru Serikali, wamesema wenzangu Wabunge wa Kigoma. Tunamshukuru sana Rais, Mheshimiwa Dkt. Magufuli na Serikali yake, sisi watu wa Kigoma mmetupa heshima kubwa. Ile barabara ya kihistoria ya Nyakanazi mpaka Manyovu sasa wakandarasi wanajenga makambi na fidia zinalipwa.

Mheshimiwa Spika, naomba jambo moja, jana tarehe 14 timu ya Hazina ya fidia ilikuwa Kasulu. Wametokea Buhigwe, sasa wako Kasulu. Wamefanya kazi nzuri, lakini yako malalamiko madogo madogo ya kifidia. Napenda kupitia kwako Mheshimiwa Waziri, timu hii wakati bado iko Kasulu; wasitoke Kasulu, wasitoke Kibondo wala Kigoma, wakamilishe shida ndogo ndogo ambazo zimejitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, malalamiko yako kama 80 hivi, yameshapelekwa kwenye Kamati za Kata na nimeambiwa wiki ijayo yatapelekwa kwenye Kamati za Wilaya. Naomba wataalam wako ambao tayari wako katika Mkoa wa Kigoma wakamilishe yote hayo ili barabara hii tuliyoisubiri kwa muda mrefu kwa kweli iweze kuanza bila matatizo yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, ni ujenzi wa Ofisi ya *TRA* Kasulu. Mwaka 2019 nilimwomba Waziri wa Fedha kwamaba katika mipango yenu Wilaya ya Kasulu, Kibondo na Kakonko, hakuna Ofisi ya *TRA.* Tujengeeni Ofisi ya *TRA* Kasulu. Sisi Halmashauri ya Mji tutakupa kiwanja bure bila kukinunua, wala kukilipia chochote, lakini kiwanja hicho bado hujakitendea haki. Nakuomba, siyo lazima unijibu sasa hivi, hebu kaa chini, tenga fedha, anzeni kujenga Ofisi ya *TRA.*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Daniel.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, barikiwa.

Nilishakutaja Mheshimiwa Ali Salim Khamis, endapo upo kule Msekwa. Kwa ukimya huu maana yake tuendelee na Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwa ufupi bajeti hii ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2020/2021. Nitangulie kumshukuru Mungu kwa kunipa afya nikawa na uwezo wa kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu leo hii.

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri, Mheshimiwa Dkt. Phillip Mpango kwa hotuba yake nzuri. Nampongeza sana. Vile vile nipe kibali nimpongeze Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Kijaji, Katibu Mkuu Dkt. Dotto na Naibu Makatibu Wakuu, Watendaji wote wa Wizara pamoja na Wakuu wa Taasisi zote ambazo ziko chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Wabunge wenzangu wameshayasema, sina haja ya kuyarudia, hata kule Arumeru Mashariki, neema hiyo tumeiona.

Mheshimiwa Spika, naomba ku-*comment* kidogo kwenye Sekta ya Benki. Nampongeza Waziri na watumishi wote wa Wizara yake kwa kazi nzuri ambayo wamefanya kusimamia Sekta ya Benki. Tumeona Benki zikikua, zikiimarika na hata mitaji ya msingi kukua kwa asilimia 16.8. Kwa kweli nawapongeza sana. Pamoja na mafanikio hayo, kwenye hotuba ya Waziri sijaona Benki za Wananchi *(Community Banks).* Maana yake ni kwamba *Community Banks* zote zimefutika kwenye soko kwa sababu ya hitaji la mitaji kisheria.

Mheshimiwa Spika, kule Meru tulikuwa na Benki ikiitwa Meru *Community Bank* nayo ilikuwa *victim,* iliondoka kwenye soko mwaka 2018 Januari kwa hitaji la mtaji wa shilingi bilioni mbili kama *minimum capital* na baada ya pale kilichofuata ni *DIB* kuingia katikati na kulipa wadau kwa kiwango cha juu kabisa shilingi milioni moja na nusu. Najua pia kuna mtu mmoja alikuwa ameuza shamba lake akapeleka fedha shilingi milioni 40 kwenye ile Benki, kesho yake Benki ikafungwa, alipata *pressure.* Mpaka leo hakuna mtu anayejua ni nini kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri angalau atuweke wazi kwamba ni kitu gani kinafuata kwa sababu kule wananchi wanaendelea kuulizia kwamba nini kinafuata sasa hivi?

Mheshimiwa Spika, naomba unipa kibali pia nitumie nafasi hii kuwashukuru wananchi wangu wa Arumeru Mashariki kwa kuniamini kipindi chote cha mwaka mmoja sasa hivi ambacho nimekuwa hapa. Napenda kuwaambia kwamba yale machache waliyoona, ile kazi ndogo waliyoiona kwa mwaka mmoja huu ni za rasharasha, bado za masika zinakuja. Naomba waendelee kuniamini na pia niwaambie kwamba hiyo neema siyo kwa sababu yangu mwenyewe, ni kwa sababu tunaye Rais makini, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ambaye kwa kweli amekuwa mahiri sana katika kufanya kazi zake za miradi ya kimkakati na utekelezaji wa ilani. Haya yote ndiyo yakanifanya nami nikawepo hapa na kuyafanya yale machache ambayo yameonekana kule.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii sasa kushauri Serikali iangalie namna ya kubadili sheria kidogo kwamba hizi Benki, kwa mfano Benki za wananchi kufutwa siyo jambo jema sana kwa sababu zilikuwa zinabeba watu wanyonge wa vijijini. Ingekuwa jambo jema kama ile *DIB* badala ya kulipa *stakeholders,* ichukue zile fedha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Shukrani, ahsante sana. Mheshimiwa Kadhija Nassir atafuatiwa na Mheshimiwa Japhary Michael.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nipo. Ali Salim Khamis.

**SPIKA:** Aah, upo! Basi haya endelea Mheshimiwa. Nilidhani haupo.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia siku hii ya leo kuwa wazima na niwatakie mfungo mwema Waislamu wote duniani. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, pia nitoe shukrani zangu za dhati kwako wewe kwa kipindi chote cha miaka mitano kunichagua kuwa kwenye Kamati ya *PAC.* Nimejifunza vitu vingi, nimeweza kuelewa namna gani Serikali inatenda kazi zake. Kwa hiyo, nakushukuru sana kwa miaka yote mitano hii kuweza kuendelea kubaki katika Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, la pili, leo nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji kwa kusikiliza kile kilio cha muda mrefu ambacho Wabunge wa Zanzibar tulikuwa tukikisema kwamba walau basi kuwe na miradi ya kielelezo katika bajeti ya Jamhuri ya Muungano, jambo ambalo wewe mwenyewe ni shahidi.

Mheshimiwa Spika, pale ambapo tulikuwa tukitoa hisia zetu ndani ya Bunge, ulikuwa ukikemea ukiona tunaonesha namna gani Zanzibar inatengwa, lakini hatimaye leo ukipitia Mpango wa Bajeti ya sasa Mheshimiwa Mpango ameweza kuweka ile miradi minne ambayo ni ya kielelezo kwa upande wa Zanzibar, ikiwemo Bandari ya Zanzibar, Bandari ya Mpigaduri, Uwanja wa Ndege, barabara ile ya

Pemba pamoja na Mkongo wa Taifa. Nawashukuru sana kwa kusikiliza yale maneno na nimeamini kwamba yale ambayo tukiyatoa hapa kwa hisia walikuwa wanayasikia na wameyafanyia kazi. Tunawashukuru kwa kuiweka miradi hii kwa ajili ya kuwasaidia Wazanzibari ili Zanzibar iweze kujinyanyua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninayo mawili ambayo ningependa nichangie. La kwanza tuna mashirika ya Jamhuri ya Muungano ambayo kutoka mwaka juzi yameweza kutoa gawio kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Ukiangalia katika kitabu hiki cha *TR* ameonesha hapa kwamba mpaka kufikia Juni, 2019 imeweza kupata shilingi bilioni 402.6 kama gawio kupitia mashirika haya kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kama unavyojua Zanzibar ni mdau wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakapokuja hapa, atuambie katika fedha hizi za gawio ambazo zimepatikana kutokana na faida ambayo mashirika jinsi yalivyoendeshwa, vipi mgao ule wa Zanzibar ni kiasi gani na ni kiasi gani ambacho kimeshapelekwa ama kuna taratibu gani ambazo zinafanyika na hasa ukizingatia kwamba Bunge lako Tukufu limeridhia hapa mwaka 2017/2018 katika bajeti iliyoishia 2017/2018 ya *ratio* ya Watumishi wa Taasisi za Jamhuri ya Muungano ile 21:79. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atupe ufafanuzi juu ya jambo hili limetengenezwa namna gani na Zanzibar imepata mgao wake kiasi gani mpaka sasa kupitia gawio hili la Serikali.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ni mfuko wa pamoja kati ya Zanzibar na Tanzania Bara ili kuweza kuweka matumizi mazuri na michango ile ya wadau hawa wa Muungano kati ya Tanzania Bara pamoja na Zanzibar. Mheshimiwa Waziri ameligusia hapa, lakini kiukweli jambo hili lina muda mrefu. Limepitishwa kwenye Katiba mwaka 1977, limetungiwa sheria mwaka 1984, imeundwa Tume mwaka 2006. Toka mwaka 2006 mpaka sasa Tume hii ipo, lakini huu mfuko umeshindwa kuanzishwa.

Mheshimiwa Spika, samahani kwa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, amesema kwamba jambo ambalo limecheleweshwa na mfumo wa kielektroniki. Siyo kweli kwamba ni mfumo wa kielektroniki, hili jambo ni la muda mrefu, aje Waziri wa Fedha atuambie sasa ni lini mfuko huu wa pamoja wa Muungano utakuwa umeanza rasmi ili Tanzania Bara iweze kujua ni kiasi gani inaweza kuchangia katika mambo ya Muungano na vile vile Zanzibar ijue ni kiasi gani inatakiwa kuchangia katika Muungano ili masuala haya yaweze kupatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, masuala haya yameshafanyiwa utafiti na Taasisi ya Kifedha ambayo inaitwa *PriceWaterHouseCoopers.* Imeonesha ni jinsi gani fedha za Muungano zinaweza kuendesha Serikali ya Tanzania Bara na zipi zinaweza kuendesha Serikali ya Zanzibar endapo huu mfuko utakuwepo. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atusaidie kwamba ni lini sasa Serikali itafikia tamati ya jambo hili kwamba miaka mitatu iliyopita mwaka 2017/2018 alituambia kwamba jambo hili liko kwenye mazungumzo na linakwenda kwenye ngazi ya Mawaziri na litakamilika. Kwa hiyo, atuambie sasa ni lini jambo hili litakuwa limekamilika ili kuondoa hizi sintofahamu za Muungano na kuisaidia hii nchi ili iweze kuendelea.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Ali Salim Halisi.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, samahani ni Ali Salim Khamis.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Khadija Nassir utafuatiwa na Mheshimiwa Jaffary Michael na Mheshimiwa

Ally Hassan King ajiandae atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajab.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Kwanza kabisa nipende kukupa pongezi pamoja na wasaidizi wako kwa uongozi imara, lakini pia nipende kuipongeza Serikali kupitia Wizara hii muhimu Wizara ya Fedha na Mipango kwa kazi nzuri ambayo inaendelea kufanywa.

Mheshimiwa Spika, nipende kuipongeza *BOT* kwa hatua ambazo imechukua kutokana na athari za kiuchumi zilizotokea kutokana na janga hili la corona. Nitakwenda harakaharaka, niipongeze Serikali pia kwa kueleza mchakato wa tathmini ya athari ya kiuchumi kutokana na janga hili ambavyo inakwenda. Na niwaambie tu; hii ndiyo Serikali imara kwa sababu huwezi kukurupuka kutoa *precautions* na hatua kabla ya tathmini, nawapongeza kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafahamu Serikali itakuja na tathmini pamoja na hatua za kuzichukua ila mimi leo pia nitapenda kutoa ushauri kulingana na hali jinsi ilivyo na vipi twende. Ushauri wangu wa kwanza kwenye hili; nipende kuishauri Serikali kulinda thamani ya sarafu yetu kwa nguvu zetu zote. Nimeona *BOT* katika *press* yao wamesisitiza manunuzi ya ndani yafanyike kwa shilingi, nawapongeza kwa hilo. Lakini tusiishie hapo tu, nipende kuishauri Serikali kupitia *BOT* ifuatilie kwa karibu mwenendo huo lakini pia itoe adhabu kali kwa watoa huduma ambao bado wanasisitiza gharama za huduma hizo zilipiwe kwa *foreign currency especially* dola.

Mheshimiwa Spika, hilo liende sambamba pia kuwasisitiza wageni ambao wapo nchini kuweza kufanya manunuzi yao kwa kutumia shilingi. Kwa kufanya hivyo tunakwenda kupunguza uhitaji wa dola nchini lakini pia tunaenda kuimarisha shilingi yetu.

Mheshimiwa Spika, la pili; napenda kuishuri Serikali kuwapa nguvu wafanyabiashara wadogowadogo hasahasa ambao wamejikita katika Sekta ya Kilimo. Tunafahamu kuwa

sasa hivi tupo katika kipindi cha janga, na hali ipo shwari Tanzania kwa sababu tunaupatikanaji wa chakula wa kutosha, lakini hatujui janga hili litaondoka lini na litaweza kuingia na kutuathiri kiasi gani.

Kwa hiyo, ili tuweze kuendelea kuwa katika hali hii nzuri ni muhimu sasa *BOT* na *TBA* kuona namna gani ambavyo wanaweza kuwasaidia wafanyabiashara wadogowadogo ambao wapo kwenye Sekta ya Kilimo ili sasa tuweze kukaa kwenye hali nzuri na mambo yaendelee kuwa mazuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa harakaharaka suala la tatu ningependa kuishauri Serikali iangalie namna gani ambavyo itakwenda kuwasaidia wafanyakazi katika kipindi hiki kigumu. Ushauri wangu katika haya ilikuwa mambo matatu; tuweze kuangalia uwezekano wa kuwapunguzia *PAYEE.* Sasa hivi kila familia katika jamii zetu imekuwa ikiingia katika gharama ya matumizi ambayo tulikuwa hatujayazoea.

Mheshimiwa Spika, ili sasa hivi familia ziwe salama lazima uwe na *saniters* za kutosha nyumbani, barakoa lakini lazima uweze kuweka *stock* ya chakula kwa kuhofia kwamba kunawezekana kukatokea mfumuko wa bei. Sasa kwa kuwapunguzia *PAYEE* wafanyakazi tunakwenda kuwapa uwezo wa kuweza kufanya *stock* ya kutosha katika mahitaji haya muhimu lakini pia kuweza kuwapunguzia *stress* ya kuona kwamba hili janga linaweza kuleta athari kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, tumeona *BOT* kupitia Wizara hii imeweza kupunguza riba lakini hili haliwezi kwenda kusaidia kama litakuwa halina usimamizi mzuri. Wenzangu wengi wameongea hapa, *BOT* imeshafanya hivyo na imekuwa ikifanya kazi nzuri sana kuona wanapunguza mzigo kwa hawa wakopaji wadogowadogo. Tunapokuja katika hizi benki za biashara wanakuwa wazito sana kutimiza wajibu wao na kwa wakati ule ambao unapangwa.

Mheshimiwa Spika, sasa nitumie tu fursa hii kumuomba Waziri aweze kulisimamia hili kwa umakini mkubwa sana, siyo

kwamba tamko hili liende kufaidisha benki, tamko na hatua hizi zilizochukuliwa Serikali imemaanisha kuwasaidia wakopaji wadogowadogo katika hali *especially* katika kipindi hiki kigumu. Kwa hiyo usimamizi uendelee lakini pia *monitoring* iwe inaendelea ili kuona sasa hili tamko na hizi hatua zinafuatwa kama jinsi ilivyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, umenipa dakika tano na nimezitumia vizuri, naunga mkono hoja, asante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Khadija Nassir. Tunaenda Msekwa Mheshimiwa Jaffary atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan King.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwa dakika hizi tano.

Mheshimiwa Spika, pamojana jitihada kubwa ambazo Wizara ya Fedha imekuwa ikifanya kuhakikisha kwamba matumizi ya Serikali yanadhibitiwa na jitihada zote ambazo zimefanyika kwa upande wa *TRA* kuhakikisha kwamba angalau kumefanyika mabadiliko makubwa kwenye taasisi hii ya *TRA.* Mimi naamini kwamba ili Serikali Kuu ipunguze mzigo mkubwa wa kuhudumia miradi mikubwa na iache miradi mingine ihudumiwe na ngazi za chini, bado naendelea kupiga kelele kwamba tuna wajibu mkubwa sana wa kuziimarisha Halmashauri na kuzifanya ziwe imara zaidi katika suala la fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilikuwa nataka kushauri Serikali kwamba ni vizuri, kwasababu katika mafanikio haya lakini eneo la Halmashauri bado kuna mkwamo mkubwa katika masuala ya fedha na hasa vyanzo vya fedha; kwa hiyo ni vizuri Serikali (Wizara ya Fedha) ione ni namna gani katika Sera zake za Fedha itaweza kuzisaidia Halmashauri kuhakikisha kwamba zinakuwa na vyanzo vipya vya fedha ili ziweze kujiendesha kwa kujitegemea zaidi ili zipunguze mzigo wa Serikali Kuu kuzihudumia Halmashauri na Serikali Kuu ijihusishe zaidi na miradi mikubwa ya kimkakati ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Fedha ya Halmashauri inaruhusu Halmashauri kukopa, lakini bahati mbaya kipindi hiki Halmashauri zimeonekana kama hazipewi hiyo fursa ya kukopa. Katika miradi hii ya kimkakati ambayo Serikali imekuwa ikisaidia miradi ya kimikakati ya Halmashauri, miradi mingine imekuwa na ugumu wa kutekelezwa kwa sababu fedha zinazotoka Serikali Kuu wakati mwingine haziji kwa wakati, wakandarasi wakati mwingine hawalipwi kwa wakati lakini miradi mingine pia inahitaji fedha nyingi zaidi kwa muda mfupi; sasa fedha zinazokuja ni chache sana.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Moshi Mjini tuna mradi wa ujenzi wa stendi ya kisasa, stendi kubwa ya magari ya mikoani na ni kituo cha mabasi ambacho labda kituo kinachozidi kituo kile ni kituo cha Dodoma kwa uzuri na ukubwa; na inawezekana sisi tulianza hata kabla ya Dodoma. Mradi ule ni wa shilingi bilioni 28.2, lakini Serikali imetoa fedha takribani bilioni tano kwa miaka miwili. Sasa najiuliza huo mradi utaisha lini, matokeo yake maana yake huo mradi utakuwa mwisho wa siku ni *white elephant.* Sasa ni vizuri Wizara ya Fedha ione ni namna gani inaendelea kuruhusu Halmashauri kukopa kadri inavyofanya tathmini kwamba Halmashauri ina uwezo wa kulipa ili hii isaidie kama chachu ya kufanya Halmashauri ziweze kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninataka kuzungumzia suala la fedha haramu, kwa sababu moja wapo ya majukumu ya Wizara hii ni kudhibiti utakatishaji wa fedha haramu. Ni vizuri elimu itolewe fedha haramu ni zipi kwa sababu watu hawajui fedha haramu ni zipi. Watu walikuwa wanadhani fedha haramu ni mpaka uzi-*import* kutoka nje lakini unasikia sasa hivi mtu kwenye akaunti ya benki ana milioni 9 amefunguliwa kesi ya *money laundering.* Sasa ni vizuri wizara isukume hiyo elimu, watu wajue fedha haramu ni zipi ili watu wasionekane kama vile wanaviziwa, wajue kwamba hili ni kosa, hata kabla hajalifanya ajue kwamba ni kosa likiwa katika sura ya namna gani.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu *Force Account.* Suala la *force account* ni zuri sana na kimsingi ndiyo njia bora kubwa

ya kupunguza matumizi ya fedha za Serikali na kuhakikisha zinatumika katika *value for money.* Muhimu sana Wizara ione kwa namna gani itatoa sasa elimu kwa wataalam ambao wanakwenda kusimamia zile fedha na kwa kiasi ambacho huo mfumo wa *force account* hautatumika kama kichochoro cha watu kuendelea tena kuiibia Serikali kwa sababu watu ni walewale, wanaweza wakawa ni wezi kuliko hata hilo ambalo tunataka kuliepusha.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, Mungu akubariki sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jaffary Michael kwa mchango wako. Nimeshakutaja Mheshimiwa Ali Hassan King kule Msekwa utafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Adadi.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, asante, nashukuru sana kupata hii nafasi. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka hai na kutupa uwezo wa kuweza kusimama hapa tukiwa wazima.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo moja la muhimu sana kulisema ambalo wengi wamelisema; ni maono ya Mheshimiwa Rais; nianze nayo. Maono yake mimi nayaita ni sawasawa na jahazi la Nabii Nuhu. Nabii Nuhu alipokuwa akitengeneza jahazi ili kuwavusha watu na gharika basi watu walikuwa wakimcheka, lakini maji yalivyojaa kila mmoja alikimbikia na akapanda lile jahazi na wale ambao waliona kwamba anazidiwa waking'ang'ania kwamba ni lazima Nuhu utufungulie safina na sisi tuondoke nayo. Kwa hiyo haya ni maono ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, lingine niende katika Fungu Namba Saba ambalo ni Msajili wa Hazina ambaye anashughulikia mapato yasiyo ya kodi. Niashuri Serikali kupitia Msajili wa Hazina kufanya uchambuzi na ufuatiliaji katika taasisi na mashirika ili kujiridhisha kuwa yanaendeshwa kwa tija na kuweza kupata mchango unaostahili kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali na mashirika hayo hasa yale ambayo yaliyofanyiwa *new capital injection.* Kwa mfano, bandari na

mashirika ya meli sasa hivi siyo yale tunayoijua; sasa hivi kuna *new injection of capital,* ni lazima tija inaweza ikazidi na tusikae na historia ileile kama ilivyokuwa mwanzo.

Mheshimiwa Spika, ushauri mwingine, nije katika miradi mikubwa ambayo ipo chini ya *NDC,* kama huu wa *Arusha General Tyres,* Liganga, Mchuchuma na Engaruka (wa magadi soda). Hapa niombe Serikali ifanye maamuzi, bila kufanya maamuzi kuna fedha nyingi sana inawezekana tukawa tunazikosa. Naweza nikasema kwamba tunachelewa wakati mwingine watu wanasema kwamba chelewachelewa utamkuta mtoto si wako.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie *flexibility on 15 percent on gross revenue.* Kuna *gross revenue* katika mashirika 21 ambayo yanapatikana. Hapa nizungimzie kuna baadhi ya mashirika ambayo tunayaona kabisa kwamba haya ni *cash cows,* yanazalisha vizuri na kama yatakuwa yana *gross opportunities* na pia kama yatakuwa mashirika hayo yapo katika hali ya *survival* na yana uwezo wa kutengeneza, wanahofia *survival* yao na yana uwezo wa kutengeneza *cash cows* tuweze kubadilisha sheria na tuwe *flexible* katika hii 15 *percent.* Kwa sababu wapo kama wakina *TANAPA* tayari kule sasa hivi tunaona kwamba kutokana na janga hili, vipi wanaweza kwenda. Kwa hiyo iletwe ile sheria tujaribu kuweka hiyo *flexibility,* tunaweza tuka-*relax* katika baadhi ya mambo ili mashirika haya nayo yakaenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, tulifanya ziara kwa Msajili wa Hazina, Msajili wa Hazina akaeleza changamoto yake sasa hivi ana mashirika mengi lakini hayana mitaji. Tukafanya ziara *DSE (Dar es salaam Stock Exchange)* wao wakasema hawafiki watu kupeleka makampuni yao kwenda kuji-*register* wakapewa *shares.* Kwa hiyo niishauri Serikali, kupitia taasisi hizi zote mbili ambazo zipo chini ya Wizara ya Fedha ile *deficit spending units na* hii *surplus spending units* zote zipo hapo. Kwa hiyo tulikuwa tunaomba kupitia Msajili wa Hazina mashirika yale ambayo labda kwamba wanahisi yatakuwa hayana uwezo mzuri wa kupata fedha yapelekwe pale. Na

Msajili wa Hazina amerejeshewa sasa hivi mambo mengi sana, kuna hoteli pale, viwanja na vitu vingine vimerudishwa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru sana Mheshimiwa Ali Hassan King. Mheshimiwa Balozi Adadi atafuatiwa na Mheshimiwa Timotheo Paul Mzava kama mchangiaji wetu wa mwisho halafu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Spika, na mimi nashukuru sana kupata nafasi hii ya kuchangia hoja hii ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa maono yake hasa namna alivyoshughulikia tatizo la corona kwa sababu suala hili sasa hivi limeanza kupewa sifa kila mahali kwa kukataa kuweka *lockdown* hapa nchini. Sasa hizi ni pongezi maalum kabisa na leo mmeona Marekani pia wakipongeza suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake yote; Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa sababu kazi ambayo wameifanya pamoja na kuwa na miradi mikubwa hapa nchini, ni mikubwa kabisa na miradi mingine kwenye majimbo yetu lakini wameweza ku-*balance* utoaji wa hela bila ya kuwa na matatizo yoyote. Pongezi hizi wapokee wote, kwa kweli wamefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, kama walivyosema wenzangu *statement* aliyoitoa Gavana kwa ajili ya punguzo la riba kwenye benki zetu ni suala la kupongeza sana, na tunaamini kabisa kwamba punguzo hilo basi litakwenda mpaka litawafikia wananchi wa kawaida. Kwa hiyo ni suala la msingi ambalo Mheshimiwa Waziri tunaomba ulisimamie kuhakikisha kwamba punguzo hili basi wakopaji wote ambao wanatumia benki wanaweza kufaidika nalo.

Mheshimiwa Spika, suala la kuomba mkopo kwenye Mfuko wa Majanga *(CCRT);* suala hili ni muhimu sana na tumelijadili kwa kina kwenye Kamati na tunaona kwamba ni vizuri Serikali ikaangalia, ikafikiria tukipata fedha hizo naamini kabisa linaweza kuweka *sustainability* ya kuona kwamba fedha nyingine zinashughulikia mambo ya corona na nyingine mambo ya miradi. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri ni vizuri suala hili mkaliangalia kwa kina ili fedha hizi ambazo wenzetu wameanza kupata basi na sisi tuweze kuzipata.

Mheshimiwa Spika, vinginevyo ningependa pia kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri. Wakati Waziri alivyoleta hapa huu mfumo wa *Treasury Single Account* watu wengi tulikuwa na mashaka nao. Na alipoleta pia mfumo wa *Electronic Tax Stamp (ETS)* pia wengi tulikuwa na mashaka nao lakini sasa hivi mifumo yote hii miwili imeweza kuwa na manufaa makubwa sana hasa huu *Electronic Tax Stamp* ambao wafanyabiashara wenyewe wameanza kuusifu. Ni muhimu tu sasa hivi mfumo huu ukaendelezwa kwenye bidhaa nyingine za viwanda ambazo zinazalishwa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la fedha ambazo zinatolewa na Wizara hii; kwa kweli wamejitahidi sana kutoa fedha za miradi mingi. Miradi kwa mfano ya kwenye Jimbo langu ambayo fedha zimetoka kwenye Wizara hii, mambo ya miradi ya maji ambapo kuna mradi ambao unakaribia kumalizika wa maji pale Pongwe. Mradi huu tatizo lake lilikuwa pampu na Mheshimiwa Waziri Mkuu anajua lakini nafurahi kusema kwamba Tanga *UWASA* wametuthibitishia kwamba wale mafundi wataalam wa pampu kutoka *South Africa* watafika wiki ijayo Muheza na kuweza kukamilisha hilo suala la maji.

Mheshimiwa Spika, pia tumeweza kupata Barabara ya Amani kutokana na fedha za Wizara hii, tumepata pia Hospitali za Wilaya, vituo vya afya, mambo ya umeme Mheshimiwa Waziri Kalemani alikuwepo Muheza juzi tu hapa na alikuwa kwenye Vijiji vya Kwa Kopwe, Simkano na Kwemhanya ambapo sasa hivi mafundi wanaweka umeme.

Kwa hiyo mpaka mwezi ujao tutakuwa tumebakiza vijiji vichache sana ambavyo haviwezi kuzidi hata kumi. Kwa hiyo sina budi kupongeza na nashukuru sana kwa Wizara hii kuweza kutoa fedha ambazo zimeweza kusaidia miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, soko la hisa la *DSE (Dar es salaam Stock Exchange)* linaenda vizuri lakini tatizo ambalo lipo pale ambalo tuliliona tulipokuwa pale ni mifuko ya hifadhi ambayo ilikuwa inachangia sana. Sasa ile mifuko ya hifadhi sasa hivi *NSSF* pamoja na *PSPF* hawapeleki tena. Sasa tulikuwa tunaomba Serikali iangalie ili kuangalia uwezekano wa ku-*boost* ili soko lile liweze kuwa hai.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni *TMX,* soko letu la bidhaa ambalo ni muhimu sana. Soko lile halipo *very active* kwa sababu halitumiwi vizuri; sasa ni vizuri sasa hivi tukaangalia uwezekano wa kuanza kutumia soko lile la *TMX* vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja na nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Balozi Adadi, Mheshimiwa Timotheo Paul Mzava atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha jiandae.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametupa uzima. Nitumie nafasi hii kwa dhati kabisa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu wake lakini pia na Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya; mnafanya kazi nzuri sana na sisi tunabarikiwa na kazi yenu njema mnayoifanya.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine pia nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais. Nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya lakini pia kwa uongozi wake madhubuti na bora alioutoa hasa katika wakati huu wa janga hili la *corona*. Mambo mengi na mwelekeo

mkubwa ambao Mheshimiwa Rais aliutoa kuanzia mwanzoni kabisa, watu wengi walikuwa hawamwelewi, lakini sisi watumishi wa Mungu kazi yetu ilikuwa ni kumwomba Mwenyezi Mungu ili anayoyafanya Mheshimiwa Rais yaingie kwenye akili za watu na huko tunakokwenda kila mmoja anaona kwamba yale yote ambayo yalikuwa yanaonekana hayaeleweki sasa ndiyo yanaanza kuungwa mkono.

Mheshimiwa Spika, nichangie kidogo kwenye Wizara hii; tuipongeze sana Wizara kupitia Benki Kuu kwa marekebisho ya sera ambayo wameyatoa. Ni jambo kubwa sana na ni jambo la msingi, lakini msisitizo wangu ni kama walivyosema wengine, tunaomba tu marekebisho haya yakaonekane kwenye maisha halisi ya watu wetu. Pamoja na marekebisho yaliyofanyika pia tuombe Serikali iendelee kuangalia maeneo mengine kama *tax relief* kwa *materials* ambazo zinaingia kwa ajili ya kuzalisha bidhaa muhimu kwa wakati huu ambao tunao wa kipindi hiki cha janga la *Corona*.

Mheshimiwa Spika, nichangie kuhusu *DIB* inaitwa Bodi ya Bima za Amana *(Deposit Insurance Board).* Kati ya mwaka 2017/2018 Benki Kuu ilifuta leseni ya benki hizi ndogo karibu benki saba na baada ya kufuta leseni kwa utaratibu wa kisheria *DIB* inaingia sasa kwa ajili ya kumalizia zoezi la kuzifunga hizo benki, lakini pia na kuwalipa. Mtu ambaye ana *maximum amount* wanalipwa bilioni moja na laki tano. Naomba niishauri tu Wizara huko mbeleni tunakokwenda, tujaribu kuliangalia jambo hili.

Mheshimiwa Spika, benki hizi zinazofungwa zina watu wanafanya kazi kwenye zile benki, kuna watu wana kampuni za ulinzi wameajiri watu wanalinda kwenye zile benki, kuna watu wana kampuni za usafi wameajiri watu wanafanya usafi kwenye zile benki. Kwa hiyo benki mmoja inapofungwa madhara yake yanakuwa ni makubwa sana kiuchumi kwa watu wengi ambao kwa namna moja ama nyingine wanahusika na benki hiyo. Ningeomba huko mbele ya safari tuangalie namna ya kurekebisha sheria hii kwa upande wa *DIB,* ikiwezekana *DIB* asibaki na kazi ya kwenda kufunga na

kwenda kuhakikisha kwamba anakwenda kulipa bima kwa wale ambao ni wanufaika waliokuwa ni wateja wa zile benki.

Mheshimiwa Spika, turekebishe sheria ikiwezekana tuwe na utaratibu kama ukiangalia hii bilioni 1,500,000 inayolipwa na *administrative cost* za kuifunga hii benki mpaka na kumaliza na kulipa na kile ambacho ulichokuwa nacho unaweza kukuta inakaribiana kabisa na ule mtaji ambao benki hii imeukosa. Tuweke utaratibu wa kisheria angalau tuwe na uwezo wa kutafuta fedha *DIB* itoe fedha, benki kuu kwa sababu ina jukumu la kuzisimamia izisimamie hizi benki, waziwekee utaratibu mzuri zipite kwenye hiki kipindi kigumu ili tuweze kuwasaidia wananchi wanaonufaika na hizi benki, lakini pia kusiwe na taharuki kwa watu ambao wamewekeza kwenye hizi benki.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, juzi kwenye Wizara ya Kilimo wamesema kuhusu miradi ya kilimo cha umwagiliaji na tumesema kwamba kama nchi, tunataka miradi ya umwagiliaji iwe ni miradi ya kibiashara itakayoweza kujiendesha na kama nchi lazima twende huko ndiyo dunia inakokwenda, hatuwezi kuwa na kila kitu kinachotolewa bure. Niiombe Wizara ya Fedha, ukisoma ule Mwongozo wa Miradi ya Kimkakati tumejikita kwenye baadhi ya aina fulani ya miradi, miradi ya ujenzi ya vituo vya mabasi, miradi ya masoko, miradi ya machinjio na miradi ya namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, tuwe *flexible,* kwa wakati huu ambao tunataka kwenda kwenye kilimo cha umwagiliaji kwenda kwenye kile cha kibiashara tunao uwezo pia wa kuwa na miradi ya kimkakati kwenye halmashauri zetu kwa ajili ya skimu za umwagiliaji. Kikubwa ni kuweka utaratibu mzuri wa namna gani fedha hizi zitapatikana, namna gani skimu zitaendeshwa na namna gani fedha hizi zitaweza kurudishwa ili kwa muda ule ambao umetakiwa kurudisha zile fedha ziweze kuwa zimerudi.

Mheshimiwa Spika, sisi Korogwe tuna skimu pale katika eneo linaloitwa Bonde la Mkomazi. Tunahitaji bilioni sita tu kwa ajili ya kutengeneza ile skimu, lakini kuna kituo cha

mabasi kinajengwa kwa bilioni nne, tofauti hapa ni bilioni mbili vingine mpaka bilioni tano mpaka bilioni nane. Tungeweza kupata hizi bilioni sita kwenye mradi wa kimkakati tukaenda kuweka tukawasaidia wananchi wakaweza kulima, halmashauri zetu zikapata mapato na fedha ile ikarudi. Kinachohitajika hapa ni kuwa *flexible* kwenye ule Mwongozo wa ile Miradi ya Kimkakati.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, nishauri kwa upande wa Ofisi ya Msajili wa Hazina; ofisi hii inafanya kazi nzuri nami naipongeza sana kwa kazi kubwa wanayoifanya, bado tu tuna changamoto kidogo kwenye baadhi ya maeneo. Tusaidieni...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Waziri, Naibu Waziri na viongozi wote wa Wizara ya Fedha na Mipango, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali

ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge hasa katika kipindi hiki tunapopambana na janga la *Covid-19*.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka minne, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango imeshiriki katika utekelezaji kwa ufanisi miradi mingi ya kimkakati na pia kuboresha sera na kanuni za uchumi na fedha. Kutokana na usimamizi mzuri wa sera, imewezesha ukuaji mzuri wa uchumi ulioenda sambamba na utulivu wa shilingi dhidi ya dola ya Kimarekani na sarafu zingine za mataifa makubwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto za *Covid-19*, kuna viashiria vya uchumi wa dunia na hata hapa kwetu Tanzania kuathirika kwa kiasi kikubwa. Pamoja na ukuaji wa uchumi kudorola, bado kuna fursa kubwa hasa kwenye sekta ya kilimo na kuna mwelekeo wa bei nzuri hasa kwenye mazao ya chakula.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali isaidie mabenki kwa kuwapa *stimulus package* ili kuwepo na msukumo wa kuhamasisha mikopo ya kilimo kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo. Pia *stimulus package* ilenge kusaidia marejesho ya mikopo katika kipindi hiki na kutawezesha motisha kwenye kilimo na kuongeza mapato ya fedha za kigeni ili kupunguza pengo linalotokana na kukosa mapato kutokana na sekta zilizoathirika sana hasa sekta ya utalii.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali iweke mkakati wa kuimarisha soko la bidhaa *(TMX)* ambalo linahitajika sana katika kipindi hiki cha changamoto za *Covid-19*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nashukuru kupata nafasi muhimu ya kuchangia hoja hii ya Wizara ya Fedha. Kwa namna ya pekee nampongeza sana Jemedari wetu Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutokana na juhudi zake

kubwa za kuleta maendeleo ya Watanzania. Pia leo nimpongeze zaidi ya sana ambapo tukio kama la leo la kuwarudisha Watanzania waliokuwa wamekwama nchini India kutokana na *lockdown* ambao walikwenda kwa kupatiwa matibabu na wengine waliohitimu masomo yao kukwama huko kutokana kutokuwepo safari za nje kwa kipibdi kirefu sasa, halijawahi kutokea kwa Tanzania, hongera sana Dkt. John P. Magufuli kwa juhudi zako, tunamuomba Mwenyezi Mungu akulinde na kukupa umri mrefu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali na watumishi waliokuwa mstari wa mbele kusimamia na wanaoendelea kusimamia ipasavyo miradi yote iliyopangwa kutekelezwa katika kipindi chote cha miaka mitano. Utendaji wao umeleta sifa kubwa katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, wakati walipokuwa wanahimizwa na wengine waliokuwa wanafanya kazi kwa uzembe katika ufanisi wa kazi zao waliona na kuhisi kwamba wanaonewa, lakini nithubutu kusema kwamba faida yake tumeiona wote. Wafanyakazi wote niwapongeze kwa utendaji wao lakini pongezi zaidi ziende kwa Mheshimiwa Rais aliowateua na kuwapa majukumu yao kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi hizo bado wapo watumishi wanaoendelea kutokujielewa katika utendaji wao na kusababisha baadhi ya miradi kukwama na kusuasua na pia kuwepo upotevu mkubwa wa fedha. Naiomba sana Serikali kuendelea kusimamia vyema watumishi hawa ambao wanakwamisha miradi ya maendeleo nchini ambapo Taasisi ya Kupambana na Rushwa inaendelea na utaratibu wake.

Mheshimiwa Spika, watumishi wengi wanakiuka sheria na taratibu za manunuzi ambapo wanaendelea kudhoofisha juhudi za Serikali na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nampongeza tena Mheshimiwa Rais kwa kutuweka wazi kuhusu ugonjwa hatari wa *Covid-19*.

Mheshimiwa Spika, baada kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kukupongeza wewe kwa namna unavyoliendesha Bunge letu Tukufu kwa weledi wa hali ya juu. Mheshimiwa Spika wewe umekuwa si kiongozi tu wa Bunge letu bali ni mlezi mzuri sana wa sisi Wabunge. Sisi Wabunge ambao hatuna uzoefu wa Bunge tumefarijiki sana kwa namna unavyotukosoa na hatimaye kutuelekeza namna bora ya kutekeleza majukumu yetu. Mungu akupe afya njema pamoja na sisi ili tuweze kumudu kazi zetu.

Mheshimiwa spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii, Naibu Waziri, pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha na hatimaye kuiwakilisha hotuba hii kwa ufasaha mkubwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia kwenye maeneo yafuatayo; ukusanyaji wa mapato ya ndani.Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali yetu kwa namna inavyochukua juhudi kubwa za kuongeza mapato katika nchi yetu. Ongezeko la 14% ya mapato ya ndani ni ongezeko zuri kidogo, lakini juhudi zaidi zinatakiwa ili kuongeza ongezeko. Uwezekano wa kuongeza mapato ya ndani upo mkubwa.

Mheshimiwa Spika, bado kuna vyanzo vingi vya ndani ambavyo kama Serikali ikiviboresha uwezekano wa kuongeza mapato ni mkubwa. Kwa mfano, maeneo ya bandari bubu. Bandari bubu bado hazija boreshwa, sehemu hizi zina makusanyo makubwa sana kama yakiboreshwa. Lakini mpaka leo unaweza kutembelea katika bandari hizi bubu usimkute mfanyakazi wa aina yeyote wa kukusanya mapato.

Mheshimiwa Spika, hizi bandari zinaitwa bubu kwa sababu ya kutokuwepo huduma za aina hii ukusanyaji wa mapato. Ushauri wangu katika bandari bubu ni Serikali

kuweka wafanyakazi wa kukusanya mapato ili tuongeze ukusanyaji wa mapato ya ndani ambayo yatawezesha Serikali kuendesha shughuli za kutoa huduma kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja. Nampongeza sana Waziri na viongozi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nina ushauri wa mambo mawili, moja, kodi ya majengo ikusanywe na Halmashauri za Wilaya, Miji na Mijini na kuingiza akaunti ya *TRA* kwa 80% na 20% ibakie kwa wakusanyaji. Pili, Serikali ilipe madeni yote ya wazabuni na wakandarasi na hasa wa ndani iliyohakikiwa na madeni mengi yana zaidi ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa baadhi ya miradi imeamua kutumia mfumo wa *Force Account* badala ya mfumo wa *competitive bidding* kwa kutumia wakandarasi. Sina pingamizi na hilo ila ufanyike uchambuzi wa kitaalam, sahihi namna ya kutumia mfumo huu wa *force account.* Tulitoka huko ndiyo maana tulitunga Sheria ya Usajili wa Makandarasi na Sheria ya Manunuzi. Nimeona yapo maeneo wanachukuliwa mafundi mbalimbali wamepewa kandarasi kwa *quotation* na hiyo kuiita *force account.* Vilevile huu mfumo uangalie hawa wanaopewa kazi kwa mfumo wa *force account* wanalipa kodi ipi?

**MHE. ZAINAB M. AMIRI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu kwa kunipa afya njema na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo katika kila Wizara zote, naishauri Serikali Wizara hii ya fedha kupitia Hazina izipeleke fedha hizo kwa wakati ili ziweze kwenda kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kwa wafanyabiashara wadogo maarufu wamachinga, wafanyiwe utaratibu ili nao waweze kulipa kodi ya mapato kwa kuwa wanafanya biashara, maana Serikali inapoteza mapato mengi kutoka kwa wafanyabiashara hao.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kupitia Hazina iwalipe wafanyabiashara wenye viwanda ambao wanatumia sukari ya viwandani *withholding tax* ya asilimia15 inayochukuliwa na Serikali mara waingizapo sukari hiyo kwa wakati, maana madai yao ni ya muda mrefu takriban miaka minne sasa wanaidai Serikali kiasi kwamba uzalishaji wao umepungua pia kusababisha kupunguza wafanyakazi kwa kuwa Serikali imeshikilia mitaji yao.

Mwisho naishauri Serikali kutokana na janga hili la Corona, imesababisha biashara kudorora, hakuna mzunguko wa fedha hususan Mkoa wa Dar Es Salaam na wafanyabiashara walishakadiriwa kulipa mapato ya mauzo yao ya mwaka huu, Serikali ione haja ya kuwasaidia wafanyabiashara hao ili wapunguziwe kodi maana kwa sasa wanakula mitaji yao, mwisho watashindwa kulipa kodi na kufunga biashara zao, Serikali iwasaidie waweze kupunguziwa.

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kukupongeza kwa weledi na umahiri mkubwa katika kuliendesha Bunge lako Tukufu. Aidha, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa ya kuliongoza Taifa letu. Kwa kipekee nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa umahiri na umakini wao mkubwa katika kuisuka upya Wizara hii na sasa matunda tunayaona. Pia nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara na timu yake kwa kazi kubwa ambayo wameifanya.

Mheshimiwa Spika, nina mambo mawili tu ya kuishauri Wizara; jambo la kwanza ni kwamba hadi sasa nchi yetu hatuna sera ya kudhibiti vitendo vya uhalifu wa utakatishaji fedha haramu pamoja na ufadhili wa ugaidi licha ya kwamba tunayo sheria ya kudhibiti aina hii ya uhalifu.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali ilifanyie kazi jambo hilo, ikumbukwe kwamba uhalifu juu ni tishio kubwa kwa usalama wa nchi yetu na uchumi wetu kwa ujumla. Jambo la pili ni kwamba Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu chini ya Wizara hakina meno kwani hakina nguvu ya kuchunguza au kushtaki watuhumiwa wa utakatishaji wa fedha haramu. Kazi kubwa ya kitengo hiki ni kupokea taarifa juu ya uhalifu kutoka kwa wazungu na kuzifanyia uchambuzi na hatimaye matokeo kuyapeleka Polisi, TAKUKURU au *TRA.* Kwa hiyo, kazi kubwa zaidi ni kama ya utawala tu ya kuratibu na kushauri. Naomba jambo hili litazamwe upya ili tuweze kuwa na uwezo mkubwa wa kupambana na aina hii ya uhalifu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango, Naibu Waziri Dkt. Kijaji, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri na uwasilishaji wa bajeti yao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na watendaji wa Wizara yapo mambo ambayo nilikuwa nataka kutoa mchango wangu kwa mambo yafuatayo; Kitengo cha *GPSA.*

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza Serikali yetu kwa kuweka mazingira rafiki kwa wafanyabiashara kwa kuondoa *uranium* na kuweka huduma zote pamoja *One Stop Centre* lakini Kitengo cha *GPSA* cha kuwataka wazabuni wanaotaka kutoa huduma kwa Serikali kutakiwa kuwa na leseni ya biashara na kuwapunguzia uwezo na uhuru na kujipanua katika nchi yao.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali isiruhusu kila Mtanzania mwenye leseni ya biashara kuruhusiwa kufanya biashara sehemu yoyote ya nchi badala ya kuongoza utitiri wa biashara kitu ambacho kitawafanya wazabuni kutoa katika huduma hiyo, ikitiliwa maanani kuwa muda uliotolewa

kujaza *tender* ya *GPSA* ni mdogo na wafanyabiashara hawakushirikishwa ili kujiandaa katika hili.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Gavana wa *BOT* kwa kuwapunguzia riba mabenki nchini katika kipindi hiki kigumu cha ugonjwa huu wa *Covid-19*; ni imani yetu hata mabenki ya biashara italeta nafuu kwa kuwapunguzia riba wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iweke utaratibu wa kuwalipa wastaafu wetu mapema mara tu wanapomaliza mkataba wa kazi zao, kwa sababu kila mfanyakazi anajulikana anastaafu lini. Ungewekwa utaratibu mzuri wa kuwaandalia malipo hata mwaka mmoja kabla ili wastaafu wakimaliza tu mkataba anakabidhiwa *cheque* yake kabisa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Ofisi ya *CAG* kwa kuwa kinara tuzo ya kimataifa kwa riport bora ya ukaguzi. Ni kweli wanastahili wakifanya kazi nzuri sana ya kuisimamia hii Serikali yetu hasa upande wa mahesabu kukaa sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Spika, awali nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na kwa uchapakazi. Nawapongeza pia Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa utekelezaji mzuri wa Ilani ya Chama.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Wizara kwa kuwezesha utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati ya kitaifa ikiwemo reli ya *SGR,* Mradi wa Umeme wa Mwalimu Nyerere na ununuzi wa ndege mpya kwa ajili ya *ATCL.* Miradi hii ni miradi ya ukombozi wa nchi yetu, ni kichocheo kikubwa cha kutuingiza katika hadhi ya nchi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kuteua miradi ya kimkakati ya Halmashauri za Wilaya. Miradi hii inategemewa kuboresha kwa kiasi kikubwa mapato ya ndani ya Halmashauri husika. Halmashauri ya Bagamoyo ni miongoni mwa Halmashauri zilizotengewa pesa kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa kimkakati wa soko la samaki. Wanabagamoyo wamefurahi sana na wanaishukuru Serikali kwa kuwajali. Kwa shauku Halmashauri imefanya maandalizi yote na kumpata mkandarasi na mtaalamu mshauri kwa wakati.

Sasa namuomba sana Mheshimiwa Waziri aturudishie pesa za ujenzi ambazo zimezuiliwa ili ujenzi uanze na hivyo hivyo zuio liondoshwe kwa Halmashauri zote ambazo taratibu zao ziko sawa. Wana-Bagamoyo wanahoji sana kuhusu kuchelewa kuanza mradi wao. Wana shauku sana na mradi huo. Nina imani kuwa Mheshimiwa Waziri atalifanikisha hili kwa maslahi ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kukupongeza wewe binafsi kwa kazi nzuri unayoifanya ya kuongoza Bunge letu tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, niruhusu nimpongeze Waziri wa Fedha Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Naibu Waziri Mheshimiwa Ashatu Kijaji, Katibu Mkuu na wataalam wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, Nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kusikiliza kilio chetu kuhusu mradi wetu wa *LNG* pale Likong'o Mkoani Lindi kwa kutoa pesa kwa ajili ya fidia. Wananchi wamefurahi sana, kura zote za ndio ni za kwako. Nilizugumza hili Bungeni, nakushukuru sana Mheshimiwa Rais wangu kwa kusikiliza hoja hiyo.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kukushukuru Mheshimiwa Waziri Mpango kwa kufanikisha jambo hili kwa wakati muafaka. Nikutakie heri na mafanikio makubwa ili urudi tena uongoze Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali bila ya kuathiri utendaji na sheria, iharakishe haraka utekelezaji wa mradi huu ili kufikia uchumi wa kati wa Tanzania ya viwanda ifikapo mwaka 2025. Sambamba na hilo kuleta chachu ya uchumi wa viwanda katika Mkoa wa Lindi, Mtwara, Tanzania, Afrika na duniani kwa ujumla.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana kwa kazi kubwa mnayofanya, lakini nina ushauri katika mambo mawili; kwanza malipo kwa *Songoro Marine*. Baada ya ajali ya kivuko cha *MV* Nyerere (2018) Serikali ilianzisha mradi wa kutengeneza kivuko kingine kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wa Ukerewe. Mradi huu unasuasua kwa sababu ya malipo kutotolewa, wananchi wa maeneo haya wanateseka sana na kuhatarisha maisha yao kwa kuwa na usafiri usio na uhakika. Ombi langu pesa zilipwe Songoro ili mradi ukamilike.

Mheshimiwa Spika, pili, mradi wa barabara wa Bunda - Nansio ukamilike ili kusaidia harakati za kiuchumi kwa wananchi wa Ukerewe.

**MHE. ABDALLAH HAJI ALI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyeizi Mungu muweza wa mambo yote. Aidha, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha na Mipango ndio Wizara mama kwa Wizara zote nchini. Aidha, Wizara hii ndio inayotegemewa kuziwezesha shughuli zote za kimaendeleo na ustawi wa nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, waswahili wanasema dharura haina bajeti, makusudio yangu ni kwamba tumevamiwa na

janga la ugonjwa wa *Covid-19* unaosababishwa na virusi vya *corona* ambao unaitingisha dunia.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na kwa kutumia taratibu, sera na haja au dharura hii iliopo ya *corona* iweze kutoa fedha za kutosha ili tuweze kupambana na janga hili.

Mheshimiwa Spika, tunahitji vifaa tiba kwa kupambana na janga hili, aidha, vifaa mahususi kwa ajili ya madaktari wetu wanaoshughulikia waathirika wa *corona* wapate vifaa vya uhakika vya kujikinga ili wawe na uhakika wa kulinda afya zao, waweze kutoa huduma stahiki kwa wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, elimu juu ya *corona* dhidi ya wananchi katika kujikinga na *corona* inahitajika ni imani yangu kwamba Serikali kupitia Wizara hii fedha itatolewa na kuweza kuwaelimisha wananchi njia mbalimbali za kujikinga.

Mheshimiwa Spika, *Covid-19* ni janga ambalo limeuporomosha uchumi wa dunia na hata Tanzania tumeyumba hivyo naishauri Serikali kuwa makini na anguko hili la uchumi duniani na kujipanga katika na hali hii kubuni njia mbadala zenye ufanisi na za haraka ili kuweza kurudisha hali na ustawi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko ya siku nyingi kuhusiana na Akaunti ya Fedha ya Mfuko wa Pamoja kati Serikali ya Muungano na Serikali ya Zanzibar. Jambo hili limekuwa la siku nyingi limeshindwa kukamilika ukizingatia ni jambo linaloihusu nchi yetu kwa maslahi na ustawi wa wananchi wa Tanzania Bara na Zanzibar. Ushauri wangu juu ya akaunti kwa Serikali kwamba basi inatosha, naomba ifunguliwe ili huo utata uliogubika uondoshwe, hili suala limalizike sote tunajenga Taifa moja.

Mheshimiwa Spika, aidha kuna malalamiko mahususi yanayoihusu Zanzibar kwamba kuna miradi ya maendeleo mikubwa ambayo inasemekana inakwamishwa kwa

makusudi miradi kama vile bandari ya Kwampigaduri, uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume na barabara ya Chakechake - Wete. Naomba jambo hili limalizike, hii miradi ijengwe kwani ni ya kimaendeleo ambayo Wazanzibari wanayahitaji sana. Naomba kila linalokwamisha utekelezaji wa miradi hii naomba sana iondolewe na miradi ijengwe sote ni Watanzania. Ahsante sana.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, tunamshukuru sana Mungu kwa majaliwa yake kwetu sote kwa muda wetu toka mwaka 2015 hadi 2020, hakika nchi yetu imestawi kijamii, kiuchumi, kisiasa, kiplomasia na huduma bora kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, nawaomba sana Watanzania kwa imani yetu mbalimbali kuiombea nchi yetu na dunia nzima kwa Mwenyezi Mungu kutokana na janga hili la *Corona* linalotikisa dunia nzima kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu ndugu zetu Watanzania wote waliofariki dunia kwa namna mbalimbali kipindi chote awapokee katika ufalme wake usio na mwisho. Tunawaombea mioyo ya faraja Watanzania wote waliopoteza wapendwa wao.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbulu Mjini nachukua nafasi hii kutoa salamu za shukrani, pongezi na kumwombea Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli na Serikali nzima ya awamu ya tano kwa kazi kubwa ya utekelezaji wa Ilani ya CCM 2015 hadi 2020 hakika tuko kidedea kuelekea Uchaguzi Mkuu Oktoba tukutane uwanjani.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nitoe mchango wangu kwa Serikali kupitia Wizara hii. Kwa kuwa hakuna mafanikio ya kiuchumi bila mikopo na kwa kuwa mikopo yote ni lazima iwe na riba, Serikali yetu kupitia Benki Kuu kufanya marekebisho ya sera ya fedha na mikopo, kuna namna ya kupunguza viwango vya riba kwa ngazi zote kwani kwa sasa

mikopo hailipiki na wakopaji wengi wamepoteza amana zao kulingana na mikopo wanayodaiwa na vyombo vya fedha. Hali hii inakwamisha ustawi wa biashara nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ifanye mapitio ya mchakato wa malipo kwa wastaafu wetu kutoa maelekezo ya muda wa Wizara na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, kwani kutokana na umri na utumishi wao malipo yao yanachelelewa hali inayowapa mawazo, usumbufu na kuichukia Serikali yao waliyoitumikia.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali itazame mfumo mzuri wa kufanya mizania ya hesabu za wafanyabiashara zinazofungwa kila mwaka zinazowasilishwa *TRA* kwani kwa sasa hesabu hizo huachwa mpaka miaka mitatu mpaka mitano na hatimaye maafisa wetu wa *TRA* kumwandikia barua mfanyabiashara madai yasiyolingana na biashara hali inayopelekea walipa kodi kuichukia Serikali na *TRA* na kutokuwa mahusiano mazuri kati ya *TRA* na wafanya biashara wetu nchini.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi Serikali iangalie mfumo mzuri wa kuendeleza vikao vya uelimishaji, uhamasishaji, majadiliano katika kuzipatia utatuzi wa changamoto mbalimbali zinawakabili wafanyabiashara katika ngazi za Mikoa na Wilaya kote nchini kama alivyofanya Mheshimiwa Rais kule Ikulu mwaka jana kwa kuwa bado kuna maafisa wachache wa Mamlaka ya Mapato kwenye ngazi za Wilaya na Mkoa wanatumia nguvu kubwa katika kukusanya mapato kwa wafanyabiashara nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mamlaka ya mapato nchini inakabiliwa na upungufu wa majengo ya ofisi, magari na rasilimali watumishi, Serikali itazame mpangilio mzuri wa rasilimali chache zilizopo na kuona vipaumbele kwa mpango wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa turudi Wizarani Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri muda wenyewe ndiyo huo, nitaomba basi Mheshimiwa Naibu Waziri utumie dakika 10, halafu Waziri dakika 20, tuwe tumemaliza. Ahsante sana karibu sana Mheshimiwa Dkt Kijaji.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa fursa hii muhimu ili niweze kuchangia hoja ambayo imewekwa mezani na Mheshimiwa Waziri wangu wa Fedha na Mipango na nianze kusema naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo imekuwa ni kawaida yangu naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kuwa pamoja kukamilisha leo kuwasilisha hotuba hii ya Wizara yetu ya fedha kwa mwaka wa tano. Hakika ni baraka kubwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu, hatuna budi kumshukuru yeye kwani yeye ni muweza wa yote.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru sana wazazi wangu; baba yangu na mama yangu ambao wamekuwa ni nguzo na kinga kwangu. Wamesimama nami katika kipindi chote cha miaka mitano ya utumishi katika Wizara hii ya Fedha, nawashukuru mno. Tatu naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuniamini kwa miaka mitano, alisema vizuri mwanangu Lucy Mayenga kwamba ni katika Wizara chache sana na nafikiri ni Wizara hii tu ya Fedha, sina kumbukumbu kama kuna Wizara nyingine ambayo wamedumu Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa miaka mitano. Hii ni neema kubwa sana kwetu namshukuru sana Mwenyezi Mungu na namshukuru sana Rais wetu kwa kutuamini.

Mheshimiwa Spika, hakika siyo jambo rahisi sana wamesema Waheshimiwa Wabunge na nakumbuka niliwahi kumwambia Mheshimiwa Waziri wangu kwamba endelea kusimama imara usitikisike, leo wamekiri na nampongeza sana Mheshimiwa Waziri. Kazi yake ni njema, amesimama imara, amefanya kazi, amepita kwenye magumu mengi, kwa

hakika nampongeza sana. Naomba niikumbuke siku alipoapishwa alipoingia pale Wizarani alinikuta, nilikuwepo, nakumbuka alichoniambia, naomba tuishi kama ndugu, mimi ni kaka yako, wewe ni mdogo wangu. Hakika nathibitisha kwa ulimi wangu tumeishi hivyo kwa miaka mitano, hakika yeye ni mlezi, amenilea, alibeba mengine hata ya Jimbo la Kondoa akayashughulikia, namshukuru sana kaka yangu, katika watu wanaoingia kwenye kitabu cha kumbukumbu ya historia ya maisha yangu ni yeye Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Rais wetu aliyemleta na akaweza kunipa malezi haya, naamini peke yangu nisingeweza. Kwa hiyo namshukuru sana Mheshimiwa Dkt John Pombe Magufuli kwa kuweza kutuvumilia, najua tu sisi ni binadamu tuna mapungufu lakini ameweza kutuvumilia na kwa pamoja tunaimaliza miaka mitano, Waheshimiwa Wabunge wakikiri kwamba wametuelewa sasa, ilikuwa ni ngumu kutuelewa lakini sasa tumeeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana wewe mwenyewe kama Spika kwa jinsi ulivyoendesha Bunge letu Tukufu, lakini kama kaka yangu, ndani ya Mkoa wa Dodoma hakika umenitendea makubwa na wana Kondoa watakukumbuka daima, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru sana Makamu wa Rais mama Samia Suluhu Hassan, yeye ni mama, yeye ni mlezi na amenilea pia alinifuta machozi nilipolia, nikasimama imara nikaendelea kufanya kazi. Nasema ahsante sana mama kwa malezi yako mema kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, nasema ahsante sana, amekuwa mwalimu mwema pale tulipokosea aliniita akanionya, alinielekeza na kwa pamoja tumeweza kuyatenda haya siku hii ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru sana familia ya Wizara ya Fedha na Mipango, hakika ni familia ninapotoka nyumbani nikiingia pale Wizarani niko na familia nyingine, nawashukuru sana tukiongozwa na Dotto James, naamini atakuwa Daktari siku siyo nyingi, hakika ameimarisha familia ya watendaji wamefanya kazi nzuri, sisi ni wamoja, nawashukuruni sana na endeleeni kumsaidia Rais wetu aweze kutekeleza maono yake kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru sana wapigakura wangu wa Jimbo la Kondoa, tumeyatenda mengi kwa pamoja kwa miaka yetu mitano, tumeiandika historia kwa pamoja, tumejenga madaraja kwa pamoja, tumejenga vituo vya afya kwa pamoja, tumejenga barabara kwa pamoja, yote haya katuwezesha Dkt John Pombe Magufuli na Serikali yake, kwa niaba ya Wanakondoa nasema ahsante sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kuyatenda makubwa kwa wapigakura wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa viongozi wangu wa Chama cha Mapinduzi kuanzia Tawi, Kata, Wilaya, Mkoa tukimalizia na Taifa nasema ahsanteni sana, nilikuwa mgeni sana kwenye siasa, wamenilea na sasa niko vizuri kisiasa, nawaambia Wanakondoa wasibabaishwe na yeyote, tuko imara tuliyoyaanza mwezi wa 10 tutarejea kwa kishindo ili tuendelee kuyatenda yote kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru sana mume wangu mpenzi Dkt Muhajir Kachwamba na watoto wangu wawili hakika wamenisaidia sana, niliporudi niko *stressed* waliweza kunielewa na tumeishi kwa amani na upendo. Hakika nasema ahsanteni sana tuendelee kuvumiliana ili tuwahudumie Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa dakika tano naamini ni muda mchache sana na leo yamesemwa mengi mazuri juu ya Wizara yetu ya Fedha. Nianze kwa Mheshimiwa Rais wetu na msimamo wake thabiti wa kimaendeleo hasa tulipopita katika msukomsuko huu wa janga la *corona,* amesimama imara sana Waheshimiwa Wabunge wamesema vizuri juu ya

sera za kibajeti, sera za kiuchumi ameongelea Mheshimiwa Silinde, ameieleza vizuri sana. kwa kweli nimpongeze sana Dkt John Pombe Magufuli. Moja ya *assumption* muhimu sana kwenye uchumi wa Taifa lolote ni *confidence,* kutokuwa na hofu na Mheshimiwa Rais wetu kwenye hotuba yake ya tarehe 22 Aprili, aliweza kuihakikishia dunia yeye ni Daktari wa *Chemistry,* lakini kwa hotuba yake ya tarehe 22 Aprili alithibitishia dunia yeye ni daktari wa uchumi pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jamii yoyote ambayo ina hofu wote walaji pamoja na wazalishaji hakuna chochote ambacho mnaweza kufanya na hatimaye ni kuporomoka kwa uchumi, lakini Watanzania bado tuko imara. Tupo imara kwa sababu tuna kiongozi makini, aliyeelewa athari nzima ya janga hili na ambaye anaelewa mfumo mzuri wa uchumi na sasa Taifa letu limesimama imara na naamini tutavuta salama kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, nimwambie Rais wangu mpendwa, nilimwambia katika bajeti ya 2018 nilimtajia aya moja kwenye kitabu kitukufu cha Mwenyezi Mungu naomba niirudie leo; katika Sura ya 68, *Suratul qalam,* Mwenyezi Mungu anasema: *"Falatutwiy-l-mukadhibina";* wala usiwatii wanaokukadhibisha, liko jambo wanalolitafuta kwako, watajifanya wema leo, ili uweze kuwafuata. Mwenyezi Mungu akamalizia aya ya tisa (9) akasema: *"Waddu lautudihinu fayudihinuna"* kwamba wanataka ulegeze masharti, ulegeze msimamo wako ili wakufurahie kwa muda mfupi, halafu baada ya hapo utakapokwama, watakuwa wao wa kwanza kushangilia kushindwa kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwambia Mheshimiwa Rais wangu hongera sana, ana imani na Mungu, amesimama na Mungu, aendelee kusimama na Mungu, tutavuka salama kwenye janga hili na uchumi wetu hautatetereka kwa kiwango ambacho wengi wanatufikiria kwamba tutafika huko. Hiyo yote ni kwa sababu amewaambia Watanzania waiondoe hofu, wachape kazi, huo ndiyo msingi imara wa uchumi wowote ule duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaombe sana na niwashukuru Watanzania, leo kupongezwa kwa Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa kuweza kukusanya makusanyo mazuri ni kwa sababu Watanzania walimwelewa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli.

Niwaombe waendelee kumwelewa na tunapopita kwenye janga hili tuchukue tahadhari, lakini tuchape kazi, kila mmoja kwenye eneo lake la kazi. Kwa kufanya hivyo, tutaimarisha uchumi wa mtu mmoja, tutaimarisha uchumi wa Taifa letu kwa pamoja na tutawashinda na kuishangaza dunia kwa sababu tuna hofu ya Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme pia katika sera hizi za kibajeti sisi kama Wizara ya Fedha tulianza kuitekeleza na tunaendelea kutekeleza, wamesema Wajumbe wetu wa Kamati ya Bajeti na niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Bajeti wakiongozwa na ndugu yangu, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki ahsanteni sana. Tumefanya kazi kwa pamoja kwa ajili ya Taifa letu, tumesimama kwa pamoja wamesema vizuri wakati tunakuja kwenye Kamati kwenye madeni tulishalipa shilingi bilioni 327 tu. Leo hii kwa sababu tunafahamu msingi imara wa uchumi ni wananchi kuwa na pesa mkononi kuendelea kufanya kazi, leo hii tayari tumeshalipa shilingi bilioni 597.54 kwa ajili ya wakandarasi wetu, wazabuni wetu, watumishi wetu na tukifahamu kabisa bajeti nzima kwa mwaka huu ilikuwa shilingi bilioni 600, tayari tumeshalipa bilioni 597...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na narejea kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana sana. Tunashukuru na kupokea dua ulizotutolea kwa niaba ya wote uliowataja.

Mheshimiwa Waziri sasa hitimisha hoja yako kwa dakika 20.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naendelea kumshukuru Mungu kwa nafasi hii, lakini na wewe nakushukuru sana kwa kunipa nafasi sasa ya kuhitimisha hoja. Pia Namshukuru sana Mheshimiwa Mashimba Ndaki, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa hotuba nzuri sana ambayo imejumuisha maoni ya Kamati. Kwa kweli nawashukuru sana na kwa niaba ya wenzangu katika Wizara ya Fedha, naendelea kuwashukuru sana kwa ushauri wao mzuri, tutaendelea kuuzingatia mpaka pale wengine watakapokuja nyuma tukawakabidhi vijiti.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote 35 ambao wamechangia katika mjadala wa bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango. Wabunge 23 wamechangia kwa kuzungumza na 12 wamechangia kwa maandishi. Nawashukuru kwa kuunga mkono hoja ambayo nimeiwasilisha. Vile vile nawashukuru sana kwa pongezi zenu kwa Mkuu wetu wa Nchi, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na sisi wasaidizi wake, kwa kweli mmetutia moyo sana. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia niseme nakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa meneno mazuri juu yangu kwa kweli nasema wazi kabisa sijapata tabu pale wizarani nimekuwa na msaidizi makini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja zilizotolewa ni nyingi ni ushauri nitajaribu kupita haraka kwa zile ambazo nitaweza kwa dakika nilizopewa lakini niwahakikishie Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge kwamba tutawasilisha majibu yetu ya ufasaha kwa maandishi kama ilivyo ada.

Mheshimiwa Spika, sasa ni kweli kabisa tumeshauliwa hapa kwamba kama Wizara ya kusimamia uchumi na husanani katika mazingira haya ya Homa Kali ya Mapafu inayosababishwa na virusi vya Corona, ni kweli tunahitaji sana kuifanyika kazi zaidi kadri unavyoenda kwasababu taarifa

zote haziji kwa pamoja. Kwa hiyo, tunaendelea kupokea taarifa hivi sasa, tuanzichambua kadri zinavyokuja, lakini niwahakikishie kwamba tumefika pazuri kama ambavyo mmpongeza hatua ambazo zimetangazwa na Benki Kuu ndani ya siku chache na hakika wakati wa Bajeti Kuu ya Serikali basi tutaongeza na hatua ambazo tume fikiria kama Serikali kwa upande kwa kibajeti na upande wa uhaueni wa kodi.

Mheshimiwa Spika, niwahakikishie pia kwamba ule mpango wa *the group of 20 the G 20* ambao pia na *World Bank* wameuafiki lakini pia na baadhi ya nchi wakopeshaji *bilateral creditors.* Tunafanya kama Serikali kila linalowezekana kuiweezesha Tanzania kunufaika na hizo program ambazo zitatuwezesha kuarisha malipo ya mikopo yaani *debt service payment* kwa utaratibu ambao wamepanga kwamba kwa sasa tutanufaika kuanzia tarehe 01 Mei mpaka tarehe 31 Disemba mwaka huu. Na hayo mengine yanayofuata basi wata-*adjust* kulingana na ambavyo tutazungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapokea ushauri kwamba pawepo fungu maalum la kulipa Deni la Taifa tutafakari tuone kama njia bora inaweza ikasaidia ikaelewaka zaidi. Tunapokea pia ushauri wa TMX kwamba inahitaji miundombinu wezeshi ni vema kabisa bahari nzuri soko la bidhaa tayari limeanza kufanya kazi na *prospects* ni zuri sana na kwa hiyo, tutaendelea kuimarisha miundo mbinu yake ili lengo letu litimie la kuhakikisha kwamba wakulima wetu kweli wanauliza mazao yao kwa bei ambayo inalipa jasho lao.

Mheshimiwa Spika, tumeambiwa tuchukue kwa uzito suala la *MNE* niseme tu tunakubali na tumeazimia kufanya hivyo, sababu hili lilisemwa sana kwenye Kamati ya Bajeti kwamba kwa kweli kama hatufuatili huko tutatoa fedha lakini hatuna uhakika zinafanya nini huko kwa hiyo ni jambo la msingi tutalitia mkazo.

Mheshimiwa Spika, labda niseme pia kuhusu kitengo cha *PPP* kipewe uwezo sawa tumesikia na ndiyo dhamira

ambayo tumefanya tumekuwa tunawaongeze watumishi, tunawaongea bajeti. Lakini pia tumekuwa tunawapeleka mafunzo ili kuhakiksha kwamba kitengo hiki kweli kinafanya kazi yake na hatimaye Taifa iweze kuona faida ya Serikali kupunguziwa mzigo kwa kuwa na miradi ya *PPP* ambayo inatekelezeka.

Mheshimiwa Spika, uliteolewa ushauri kwamba ni kweli kuna mchakato wa mnunuzi baada ya bajeti ya Serikali kupitishwa lakini inaonekana kuna *disconnect* baadhi ya Wizara wanasindwa nawasubiri tu wapekewe fedha.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kutoa elimu kama ilivyoshauriwa, lakini niwakumbushe tu kwamba kila Bunge hili linapopitishwa Bajeti kazi moja ya kwanza ambayo Mlipaji Mkuu wa Serikali anafanya ni kutoa waraka wa namba moja wa hazina wa kila mwaka, ambao unaeleza taratibu namna gani yakupata fedha ni kitu gani kinahitajika kutoka hazina. Kwa hiyo, tutalifualia kuendelea kutoa elimu kwa kushirikiana na Makatibu Wakuu kuhakikisha kwamba tunapunguza hili linaloonekana kwamba halijafanyika ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Benki Kuu imechukue hatua ambazo mmezipongeza, lakini niseme kwamba hata sasa baada ya hatua ambazo zimekuwa zinachuliwa mara kwa mara hata sisi ndani ya Serikali hatujaridhika na kiwango cha riba za benki kupungua. Kwa hiyo, ni kweli kabisa na niseme kwamba tunajipanga ndani ya Serikali kuongeza usimamizi wa hizi benki, kuangalia sana gharama zao ambazo zinasababisha hizi riba kuendelea kuwa juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, basi tunaendelea kupokea shukrani zilizotolewa kwangu na watendaji wenzangu ndani ya Wizara, na hususani kwa maboresho mengi amboyo tumefanya ya mifumo ya kieletroniki ya kusaidia kukusanya mapato lakini pia kudhibiti matumizi ya Serikali. Maana hizi ni fedha za wanyonge wa Tanzania ni wajibu wetu tuhakikishe kwamba zinasimamiwa vizuri, ahsanteni sana kwa kweli nimesema mmetutia moyo.

Mheshimiwa Spika, vile vile tumepokea ushauri juu ya kazi nzuri anayofanya Msajiri wa hazina lakini pia *CAG*, na Msajiri wa Hazina kwa upande wa kusimamia mashirika tutaendelea kufanya hivyo na nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Chegeni na kamati anayoingoza kwa kazi nzuri sana ambayo imewesha Serikali ikapata nyongeza kubwa katika mapato yasiyo ya kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande ushauri wa kufuata kodi za kero na kwamba zinaweza zikafutia *Foreign Directing Investment* zaidi nikumbushe tu kwamba Serikali ya Awamu ya Tano imefanya hivyo mnakumbuka bajeti ambayo tunayo sasa mwezi Juni mwaka, Serikali ilifuta kodi za kero na tozo 56 na tutaendelea kufanya hivyo kama ambavyo tuliahidi kwamba tunatekeleza ile "*Blue Print on regulatory reforms to improve the business involvement*" ni wahakikishiea kabisa Mheshimiwa Spika na Bunge lako Tukufu kwamba tutaendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali iendelee kupambana na Corona huyu mnyama tunaye tunashukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake lakini tunaendelea kupambana ndio maana wapo hapa pole zao hawa waliokimbia uwanja wa vita lakini niwahakikishe kabisa Serikali inafanya hivyo na siku chache tutaleta taarifa ya hatua gani nyingine ambazo tunaongeza kupamba na huyu manyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wastaafu nimpokea kile kilichosemwa na Mheshimiwa Miraji na bahati nzuri tayari umeaniwashilishia hapa zile *document* basi nitazifuatilia lakini ni *commitment* ya Serikali kwamba tutajitahidi kadri inavyoonekana wazee waliotumikia Taifa letu vyema kwa kweli wanastahili mafao yao tena kwa wakati. Kinachotusumbua mara nyingi ni udhaifu katika taarifa lakini Wizarani pale ni moja ya mambo ambayo tumeyawekea kipaumbele kwamba tuhakikishe wastaafu wetu basi wanaendelea kustaafu kwa amani kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipende kusema zimetolewa shukrani nyingi na mimi niwarudishie Mungu awabariki

Wabunge wote na hasa Wabunge wa Hapa Kazi Tu na kwa kweli tunawaombea kama Wizara machanguliwe mrudi kwenye Bunge la Novemba mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, suala la *Force Account* kweli tunalipokea kweli litetupa *mileage* kubwa limerahisisha utekelezaji wa miradi na imekwenda kwa kasi zaidi na faida ambazo zimeelezwa humu ndani tunazitambu ndani ya Serikali na niwadhibitishie kwamba kwa kweli tunataendelea nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani imesemwa vizuri sana kuhusu uwezo wa CAG hapo nyuma tulipata shida kidogo lazima yakague na makampuni mengine hapana uwezo na nini, lakini siyo kweli na *CAG* mpya nampongeza sana. Kwa mara ya kwamba Benki Kuu imekaguliwa vizuri kabisa na ofisi ya *CAG* bila tatizo lakini pia *TANAPA* na faida zake zimewekwa vizuri kabisa. *CAG* anao uwezo mzuri na *commitment* ya Serikali ni kuendelea kumuwezesha ili aendee kutufanyia kazi nzuri ya kuibua madudu ili tujisahihishe kuokoa fedha za wanyonge wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Silinde niseme kwamba kwa kweli hata kwenye kamati amekuwa ni mjumbe wa kamati ambaye amekuwa *very constructive* kwenye kamati, na haya mapendekezo ambayo anasema basi tutayatafakari ili kwenye hatua za kibajeti na kikodi nadhani la msingi asubiri tu wakati ukifika tutayaeleza hayo nasi tumefikiria ndani ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na Waheshimiwa Wabunge kwa kweli niseme kwamba tumeendelea kupokea pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais katika ngazi ya Serikali Kuu lakini pia mpaka huko vijiji naona Mheshimiwa Chegeni anasema yeye umeme amebakiza vijiji vitatu tu. Kwa kweli niseme kwa kifupi kwamba hata sisi ndani ya Wizara ya Fedha tunajivunia sana kuwa sehemu ya mafanikio ya kishindo yaliyoletwa na Serikali ya Awamu ya Tano. Nimekwisha kusema kwamba ninampongeza sana yeye na kamati yake wamekuwa chachu ya kuongeza mapato yasiyo ya kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimshukuru sana kwa kusisitiza hili la kuwa baadhi ya watanzania wanakejeli wanaungana na maadui zetu kupinga hatua za dhati kabisa ambazo Serikali imechukua niseme kwa kweli ni dhambi kuwa kutokuwa wazalendo. Si vyema tukawa sehemu yakubeza jitihada njema maana tunafahamu hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ulieleza vizuri sana kwa kweli kumtarajia mtu familia ambayo inategemea yule mama anatoka Gongolamboto anakwenda kununua samaki ili arudi Gongolamboto akakaange samaki ili familia yake ipate kipato watoto wake waende shule watoto wake wale halafu umwambie fungia ndani haiwezekani. Sasa hawa wanaobeza msimamo ambao ametuongoza Kiongozi wetu Mkuu kwa kweli tuwapuuze sisi tuendelee kufanya kazi kama alivyotuelekeza lakini tuchukue tahadhali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zile hatua ambazo zimengazwa na Benki Kuu ya Tanzania tumeshauriwa hapa kama wizara tusimamie kuhakikisha kwamba zinafikisha manufaa yake kweli yanaonekana kwa wananchi. Niwahakikishie kwamba wizara yangu itasisitiza hilo na kwa kweli tutalisimamia ndiyo maana tupo hapa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hoja ni nyingi lakini nisema walau nyingine chache mradi wa barabara ya Uvinza maragarasi, mradi huu utachegwa kwa mkopo kutoka mfuko wa *OPEC* na Abu Dhabi na wafadhili *OPEC* watafadhili dola za Malekani milioni 18 na Abu Dhabi milioni 15. Mshauri elekezi anakamilisha usanifu wa mradi yaani *design* na atawasilisha *TANROADS* na matarajio kuwa mwezi Julai mwaka huu zabuni ya mkandarasi itatangazwa, na mkopo kwa ajili ya mradi huu ilikwisha patikana na mikataba ilikuwisha kusainiwa. Kwa hiyo, ni taarifa njema kwa ndugu zangu kwa Kigoma wasubiri tu Serikali yao ya Awamu ya Tano haitawaangusha ahadi zake zipo pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ilisemwa pia kwamba tuanzishe kitengo cha *MNE* wizarani, nipende kuliambia Bunge lako tukufu tayari wizara imekwishaanzisha kitego cha

*MNE* na imekwisha kuteua kamishina msaidizi kwa ajili ya kusimamia hiki kitengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tumeanzisha mfumo *MNE* ambao kwa sasa upo kwenye majaribio ambao tunategemea utaanza kufanya kazi rasmi mwezi Julai, 2020. Nzuri zaidi ni kwamba umeandaliwa na wataalamu wa ndani na utaunganisha na mifumo mingine lakini pia tumeanza matayarisho ya kuandaa sera ya MNE pamoja na mkakati wa kuratibu *MNE* zilizopo kwenye wizara nyingine mpaka kwenye ngazi ya halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imekwisha kuelezwa Mheshimiwa Naibu waziri amenisaidia hapa madeni ya wakandarasi tunajitahidi sana sana kulipa, na kwa kweli tunameongeza kasi kama sehemu ya mkakati wetu wa kupambana na gonjwa hili la Corona ili wananchi wetu ambao walitoa huduma kwa Serikali au wakandarasi lakini pia watumishi walikuwa wanaidai Serikali waweze kuwa na nguvu zaidi ya kupambana na kwa mwezi Machi peke yake tumetoa zaidi shilingi bilioni 900 na hizi ni nje ya zile bilioni 500 na ushee ambazo tulikuwa tumelipa awali kwa ajili ya kulipa malimbilikizo yale madai mbalimbali. Kwa hiyo, kwa kweli tunalichulia kwa umuhimu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, niseme pia kuhusu kama anasema tumeinyima fedha *Poverty Monitoring Master Plan* tunapata wapi takwimu za umasikini kwamba unapunguaje? Takwimu za umasikini tunazipata kutoka kwenye *how sold budget survey* ambayo ndio huwa ndiyo *instrument* ya kupima mwenendo wa umasikini katika nchi kwa hiyo asiwe na uwasiwasi taarifa zetu ni thabiti kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda nisema pia kuhusu kuuingunisha Mkoa wa Kigoma na *grid* ya taifa niseme tu kwa kifupi kwamba mtakapoona mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka ujao *North - West Grid*, mradi wa *North - West Grid* kutoka Mbeya Katavi mpaka Kigoma ni moja ya miradi ambayo imepewa kipaumbele kikubwa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema naona sijui kama muda upo upande wangu labda niseme tu kwamba...

**SPIKA**: Naomba umalizie naona muda kama unavyoona tena pale.

**WAZIRI WA FEDHA MIPANGO**: Mheshimiwa Spika, sawa niseme tu moja kwamba tumepewa pongezi kwa ajili ya kupongeza kuonyesha miradi ya Zanzibar kwenye hotuba yetu niseme tu kwamba Wazanzibar ni watanzania kama mimi, kama mtu yoyote na kwa hiyo na sisi tumeapa kudumisha Muungano ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba *document* zetu hizi pia zinagusa upande wa pili wa Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo nashukuru tena kwa nafasi ahsante sana kwa michango yenu na shukrani naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono naomba nimshukuru tena Mheshimwia Waziri kwa kuhitimisha vizuri hoja yake ya Wizara yake ywa Fedha na Mipango kwa Bajeti ya Wizara hiyo.

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama ifuatavyo:-**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

Fungu 7 - Ofisi ya Msajili wa Hazina...................Sh. 25,604,866,000
Fungu 10 - Tume ya Pamoja ya Fedha..................Sh. 2,850,96500
Fungu 13 - Udhibiti wa Fedha Haramu..............Sh. 2,915,586,000
Fungu 21 - Hazina.........................................Sh.1,088,177,812,000
Fungu 22 - Deni la Taifa ............................Sh. 10,487,786,822,000
Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali...............Sh. 63,775,417,000
Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango........Sh. 67,030,512,000

## MATUMIZI YA MAENDELEO

Fungu 7 - Ofisi ya Msajili wa Hazina.....................Sh. 2,300,000,000
Fungu 13 - Udhibiti wa Fedha Haramu................Sh. 500,000,000
Fungu 21 - Hazina.........................................Sh. 641,003,892,000
Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali..................Sh. 3,500,000,000
Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango........Sh. 12,016,431,000

**SPIKA:** Sasa Waheshimiwa Wabunge kiutaratibu natakiwa niwahoji kuhusu kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na takwimu zangu hapa zinaonyesha moja kwa moja kwamba Wabunge walio wengi wameafiki kabisa kwamba bajeti hii ipite. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**SPIKA:** Naomba niseme kwamba tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Katibu Mkuu, ndugu Dotto James na wasaidizi wako wote akiwepo Msajili wa Hazina, akiwepo *CAG* katika eneo hilo la Wizara hii Gavana wa Benki Kuu, Kamishna wa *TRA*, na timu nzima ya Wizara ya Fedha tunasema kazi njema na muendelee kufanya kazi hii nzuri ambayo mmeendelea kuifanya.

Ssisitizo la Mheshimiwa Rais la kutenga 40% ya fedha kwenda kwenye maendeleo ni sisitizo muhimu mmelishikilia limetusaidia sana katika Majimbo yetu na tunaomba muendelee sana kulishikilia hilo tujitahidi sana tunavyoweza tunajua lime-*create* ugumu mahali fulani na mahali fulani lakini ni jema sana utamaduni huu tuendelee kuwa nao na mengine mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyaeleza, Mheshimiwa Kamishna wa *TRA* bado Kongwa kule hatuna ofisi ya *TRA* ya wilaya basi mtukumbuke huko mbele ya safari na sisi. *(Makofi)*

Kamati yangu ya bajeti tunawashukuruni sana mmefanya kazi masaa mengi kwa muda mrefu na Waziri, Naibu Waziri na timu yake yote Kamishna wa bajeti na

wengine lakini mmefika mahali ambapo kazi yetu ni nzuri kwa ujumla wake. Nakumbuka siku moja nilikuwa naangalia nadhani kwenye *you tube* nikawa naangalia Bunge la Nigeria wakati huo Waziri wa Fedha wa kule alikuwa na mama mmoja maarufu sana amewahi kuwa *Deputy Director* wa *World Bank* Nigeria maarufu sana anaitwa mama Ngozi Okonjoi Weala jinsi alivyokuwa anakwenda kwenye Bunge na hasa kwenye kamati ya fedha na anavyofukuzwa utafikiri kibaka na kudhalilishwa *so to say* yaani kabisa.

Kwa hiyo, huwa ni ngumu sana Waziri wa Fedha kuwa na mahusiano mazuri na Bunge lakini tunakushukuru Mheshimwia Waziri umejitahidi kwasababu unasimamia *scarce resources* na mahali penye *scarce resources* lazima pawe na *scramble* sasa penye *scramble* lazima tu utaonekana mbaya.

Kwa hiyo, tunakupongeza sana na Naibu wako kwa kweli kukaa miaka mitano ni historia kubwa na bahati nzuri wewe ulisimamia mipango tena kwa miaka mitano kabla na umesimamia mipango kwa miaka mitano inayofuata kwa kweli unapaswa uandike kitabu sasa cha mipango ya nchi hii na mwelekeo wa tunako elekea una *a very good story to tell in the future*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nina tangazo moja ambapo nawatangazieni linatoka kwa Mheshimiwa Margareth Sitta mwenyekiti wa *TWPG* anaomba niwatangazieni Waheshimiwa Wabunge wanawake kwamba wale wote ambao mlinunua hisa za Benki ya Wanawake *BWB* mnaombwa kuwasiliana na Katibu wa Benki ya Posta, ili kuwasilisha taarifa za akaunti zetu haraka iwezekanavyo ili muweze kulipwa fedha zenu ambazo mlikuwa mmewekeza kwenye Benki ya Wanawake, natumaini mmenisikia wote. *(Makofi)*

Basi baada ya maelezo hayo, nimalizie na jambo moja dogo tu la mwisho kabisa nalo ni linahusiana na haya yanayoendelea ya rafiki zangu kuendelea kupotosha potosha umma kama vile kuna mtu ambaye aliwafukuza

hapa hapana hakuna mtu aliwafukuza ni wao wenyewe waliojifukuza kwasababu ambazo hazina kichwa na mguu lakini wakiwa wamechukua fedha kwa ajili ya kufanya kazi. Kwa hiyo, shughuli yetu iko hapo tu, kuchukua fedha kwamba utafanya kazi ya umma halafu badala yake unaingia mitini ndiyo maana tunataka fedha hizo zirudi.

Baadhi yao wamekuwa wakiropoka ropoka kitu ambacho si kizuri sana na malumbano ambayo hayana kichwa na mguu. Kwa mfano yuko mmoja Mheshimiwa Rhoda Kunchela yeye amemtuhumu Mheshimiwa Nimrodi Mkono kwamba amelipwa fedha za *per diem* kwa kuwa ni Mbunge wa CCM yeye hajatakiwa kurudisha. Sasa tabia za namna hii nimezikemea sana mara kwa mara. Mheshimiwa Nimrodi Mkono kwa Rhoda Kunchela ni baba yake kwa watoto waliolelewa wenye adabu huwezi kufika huko.

Lakini pili Mheshimiwa Nimrodi Mkono hamjamuona hata siku moja hapa angelipwaje hela ya *per diem*? Hela ya kujikimu? Na nyinyi taratibu mnazijua? Mheshimiwa Nimrodi Mkono anaumwa sana ni mtu wa kuombewa kwa Mwenyezi Mungu pale alipo hajitambui leo unasimama binti unamtuhumu mzee wa watu kwamba kaiba hela kachukua hela. Sasa namtaka Rhoda Kunchela ama aombe radhi kupitia taratibu hizo hizo za mitandao alizofanya au la sivyo atakapokuja hapa basi itabidi na siyo tu atakapokuja namtaka *actually* athibitishe maneno haya ama aombe radhi ama athibitishe kwamba mzee wa watu alikuja kinyume nyume hapa sijui namna gani akalipwa hela ambazo hakulipwa mimi Spika nasema hajawahi kulipwa wala hastahili kulipwa sababu hakuwepo.

Tabia hii ya kuropoka ropoka hii Waheshimiwa Wabunge hii nasema kila wakati baadhi ya Wabunge wa Upinzani wanafikiri ukishakuwa Mbunge wa Upinzani wewe unatamka chochote tu yaani chochote tu unaropoka tu jambo ambalo si sawa Rhoda Kunchela ama uombe radhi, ama uthibitishe haya maneno uliyoyasema dhidi ya huyu mzee wetu ambaye kwa kweli anaumwa na niwaombe Waheshimiwa Wabunge tuendelee kumuombea mzee wetu

huyu yanachafua yanamchafua yeye mwenyewe Mheshimiwa yanachafua familia yake yanaondoa amani kwa wapiga kura wake kusikia Mbunge wao amechukua hela ameingia mitini jambo ambalo si kweli hata kidogo.

Sasa baada ya maneno hayo naomba sasa niahirishe shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu saa nane kamili mchana.

*(Saa 12.11 Jioni Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatatu, Tarehe 18 Mei, 2020 Saa Nane Mchana)*